# Nipashe

Jumatatu Januari 21, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579819

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Chadema yamjibu Spika hatima ubunge wa Lissu

UKURASA 2




UKURASA 13

# Kanuni Uchaguzi Serikali za Mitaa sasa kufumuliwa

UK. 4

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MVUA YAHARIBU EKARI 300 ZA PAMBA, MAHINDI

MVUA kubwa ya mawe iliyoambatana na upepo imeharibu zaidi ya ekari 300 za pamba, mahindi, mtama na choroko katika mashamba ya wakulima, huku baadhi yao wakiachwa bila makazi baada ya nyumba zao...

UKURASA WA 26

### WAZIRI AIPONGEZA TAASISI YA MENGI

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Stella Ikupa, amezipongeza Taasisi ya Watu Wenye Ulemavu ya Dk. Reginald Mengi, Kamal Group of Companies and People's Empowerment Fund na Rotary Club kwa kuendelea kusaidia...



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo.

## ASKOFU: KKKT TUNAHUJUMIWA

UKURASA 3

## CAG uso kwa uso Kamati ya Bunge leo

UK. 2



MICHEZO ZAHERA ATOA NENO LA UBINGWA YANGA - UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# CAG uso kwa uso Kamati ya Bunge leo

**Na Gwamaka Alipipi**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, leo anatarajia kuhojiwa katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge dhidi ya kauli yake anayodaiwa kuitoa akiwa ughaibuni kuwa 'Bunge ni dhaifu'.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimtaka CAG, Prof. Assad, kufika mbele ya kamati hiyo leo kujieleza kuhusu kauli yake hiyo aliyoitoa akiwa Marekani.

Akiwa nchini humo, CAG Prof. Assad, alihojiwa na chombo cha habari cha Idhaa ya Amerika juu ya ripoti za ukaguzi ambazo zimekuwa zikifanywa na ofisi ya CAG, lakini hazifanyiwi kazi pamoja na kuonyesha kasoro katika matumizi ya fedha za umma.

Kwenye maelezo yake Prof. Assad anadaiwa kueleza kuwa "sasa hili jambo ambalo kimsingi ni kazi ya Bunge, kama ofisi yake inatoa ripoti inayoonyesha ubadhirifu halafu hatua hazichukuliwi, huo kwake mimi ni udhaifu wa Bunge, Bunge linatakiwa lisimamie na lihakikishe kwamba kwenye matatizo hatua zinachukuliwa."

Kutokana na kauli hiyo, Januari 6, mwaka huu Spika Ndugai aliagiza CAG Assad kufika mbele ya kamati hiyo ili kujieleza kwa nini anaudhalilisha mhimili huo.

Hata hivyo, kwenye mkutano wake na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Prof. Assad alieleza kuwa majibu aliyoyatoa wakati akihojiwa hayakuwa na nia ya kulidhalilisha Bunge.

"Maneno kama udhaifu na upungufu ni lugha ya kawaida sana kwa wakaguzi katika kutoa maoni ya utendaji wa mifumo ya taasisi mbalimbali, ni wazi kwamba watu wengine wanaweza kuchukua tafsiri tofauti ya maneno kama haya," alisema Prof. Assad. Mbali na kueleza hivyo, Prof. Assad, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa atatikia wito wa Spika Ndugai wa kufika katika kamati hiyo leo kuhojiwa.



Rais mstaafu Alhaji Ali Hassan Mwinyi (katikati), akiwaongoza Waislamu kwenye sherehe za kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeiry (kushoto), Mjumbe wa Kamati ya Amani Mkoa wa Dar es Salaam, Shariff Abdulkadir (wapili kulia) na Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilal. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waliokaidi wito wa TRA kupewa kibano

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imesema kuwa ambao hawakuitikia wito wa kulipa kodi bila riba kwa kipindi cha siku 100 wataanza kuilipa kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na Nipashe, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema kwa sasa ambao hawakuitikia wito huo watatakiwa kulipa kodi inavyotakiwa.

"Kwa mujibu wa sheria kamishna amepewa mamlaka ya kusamehe chini ya asilimia 50, sasa kama wapo ambao hawakulipa kwa muda uliotolewa wajue kuanzia sasa kamishna ataangalia kama wanastahili kuondolewa riba au kulipa kwa ukamilifu," alisema.

Alisema kwa sasa TRA inafanya tathmini kujua waliolipa na ambao hawajalipa na kufuatiwa na ufuatiliaji wa kina kuhakikisha malimbikizo yote ya kodi yanalipwa inavyotakiwa.

Julai mwaka jana, TRA ilitangaza vigezo sita kwa wanaostahili kupata msamaha wa riba na adhabu kwenye malimbikizo ya madeni ya nyuma ya kodi.

Tangazo hilo lililokuwa limesainiwa na Kamishna

INAENDELEA UK. 26

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
**40470 DODOMA,**

17 Januari, 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe **24/01/2019** kampuni ya **Raphael Logistics Limited** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es Salaam Port kuelekea Kinyerezi,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **696 DNR / T 459 CBB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 20.0 |
| Upana | - | mita | 4.3 |
| Kimo | - | mita | 5.3 |

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam Port hadi Kinyerezi kupitia Tabata,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215007402

## Chadema wamjibu Spika hatima ubunge wa Lissu

**Na Enock Charles**

SIKU moja baada ya Spika Job Ndugai kumtaka Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu (Chadema), kurejea nchini, uongozi wa chama chake umekosoa uamuzi huo na kusisitiza utapigania haki zake.

Juzi, Spika Ndugai alikaririwa na vyombo vya habari akimtaka mbunge huyo kurejea nchini ili kuendelea na shughuli za Bunge kwa kuwa hana kibali cha kuwa nje ya nchi.

Ndugai alikaririwa akisema Lissu hana ruhusa ya kuwa nje ya Bunge, hivyo anatakiwa kurejea nchini kuendelea na shughuli za ubunge.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alikosoa agizo hilo la Spika Ndugai, akieleza kuwa anayeweza kuthibitisha kupona kwa Lissu ni madaktari wanaomtibu. Mrema alisema kuwa mpaka sasa, hakuna anayejua Lissu amepona ama la.

"Yeye (Spika) si daktari mpaka aseme kuwa Lissu amepona na hajawahi kumtembelea kwa kipindi chote tokea apelekwe hospitali," alisema Mrema na kuongeza:

"Tunakumbuka aliyewahi kuwa waziri wakati wa serikali ya awamu ya nne, Prof. Mark Mwandosya aliugua kwa zaidi ya mwaka, lakini hatukusikia kauli za aina hii."

Alipoulizwa na Nipashe kwa nini Lissu ameanza kutembelea nchi kama Uingereza, aliyoitembelea wiki iliyopita, ilhali bado ni mgonjwa, Mrema alisema Ubelgiji na Uingereza si mbali kwa kuwa ni saa moja tu kwa usafiri wa ndege.

Akizungumzia suala la kile kinachodaiwa njama za kutaka kumvua ubunge Lissu, Mrema alidai zimeshavuja kabla ya kutekelezwa huku akisisitiza kuwa hazitafanikiwa.

"Hiyo ni njama ambayo imeivuja na tuimeinasa kabla haijatekelezwa na itashindwa kama zilivyoshindwa njama zingine," alidai Mrema.

Kwa zaidi ya mwaka, Lissu amekuwa Ubelgiji akipatiwa matibabu ya kibingwa kutokana na kupigwa risasi na watu wasiojulikana alipokuwa anajiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake Area D Septemba 7, 2017 mchana alipokuwa anatoka kushiriki kikao cha Bunge.

Baada ya shambulio hilo, mbunge huyo aliwahishwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, alikopatiwa matibabu ya awali kabla ya kuhamishiwa Hospitali ya Nairobi, Kenya na baadaye kupelekwa Ubelgiji kwa matibabu zaidi.

## HABARI KITAIFA



Soko la Manzese maarufu kama Mahakama ya Ndizi likiwa limejaa tope, ambapo husumbua watu wanaoingia kwa ajili ya kununua bidhaa na hivyo huwabidi kununua maji ya kusafisha miguu yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hasunga awaonya warasimu sekta kilimo

**Na Mwandishi wetu,** TABORA

KUFUATIA hali ya kutowajibika, uzembe na urasimu kwa baadhi ya watendaji katika sekta ya kilimo kusababisha ucheleweshaji wa pembejeo za kilimo, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, amekemea vikali vitendo hivyo na kusema vinakwamisha dhamira ya serikali ya kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo.

Akizungumza katika ziara yake kiutendaji ya kukagua maendeleo ya kilimo mkoani Tabora, Waziri Hasunga, alikemea tabia ya watendaji kuendeleza urasimu katika upatikanaji wa pembejeo kwa wakati.

"Nisingependa kusikia hadithi za ucheleweshaji wa mbolea zikiendelea, huku wakulima wakiendelea kuathirika na hali hiyo, ni lazima sasa tuache kufanya kazi kwa mazoea na kuwasaidia wakulima wafikie malengo ya kuwa na kilimo chenye tija na uhakika," alisema Waziri Hasunga.

Aidha, aliwataka watendaji kuwa wabunifu katika kuhakikisha masoko mapya yanapatikana ili wakulima wapate fursa ya kuuza bidhaa zao tofauti na sasa, ambapo kumekuwa na changamoto kubwa ya soko hususani kwa zao la tumbaku.

"Tusingependa kusikia kwamba tumbaku haijanunuliwa na ikifikia hapo serikali tutachukua hatua kama tulivyofanya katika zao la korosho, hata hivyo tusingependa tufike huko. Hakikisheni tumbaku yote inanunuliwa mwaka huu," alisema waziri na kuongeza:

"Watendaji wazembe ni vyema wakatupisha kwa

INAENDELEA UK. 8

# Mkuu wa KKKT awajia juu wahujumu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, amevunja ukimya kuhusu baadhi ya viongozi wasiolitakia mema kanisa hilo ambao wamekuwa wakiibua chokochoko za kujaribu kuvunja umoja wao kwa kuchochea migogoro inayolenga kuwagawa.

"Kwa nguvu moja, sisi Wakristo tunapaswa kuliombea kanisa, roho wa mifarakano na roho wa mparaganyiko ipate kushindwa. Inasikitisha sana kuona wachungaji na maaskofu kama sisi, badala ya kulikusanya kundi la bwana (Mungu), sisi ndio tunaoligawa. Hakika hawatafanikiwa.

"Kwa sababu tu ya kiburi na nafasi ambayo tumepewa, Mungu atusamehe sana, atuhurumie sana. Hebu tusimame kupingana na kukemea wanaotaka kuligawa kanisa la Mungu."

Alikuwa akitoa salamu zake jana katika ibada maalumu ya kuzindua na kuweka wakfu Kanisa jipya la Usharika wa Kimashuku katika Jimbo la Hai la Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT.

Akizungumza kuhusu migogoro ya ardhi, Dk. Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, alisema hivi sasa kuna watu wanajaribiwa na wanatafuta njia ya kulinyang'anya kanisa ardhi yake.

"Naonya na nakemea kwa nguvu zote, usijaribiwe kusogeza mpaka wa jirani yako. Leo watu wanajaribiwa kwa hila, jambo hili nimeliona kule Vunjo, hata Jimbo la Hai na kule Karatu kumetokea tena jambo hilo. Watu wanajitokeza wanafanya siasa, wakisema ni ardhi ya kijiji, wale ambao wameongoza jambo hili tumekemea na Mungu amewasikia," alieleza Dk. Shoo.

INAENDELEA UK. 8

# Mvua yaharibu ekari 300 za pamba, mahindi

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MVUA kubwa ya mawe iliyoambatana na upepo imeharibu zaidi ya ekari 300 za pamba, mahindi, mtama na choroko katika mashamba ya wakulima, huku baadhi yao wakiachwa bila makazi baada ya nyumba zao kuezuliwa na upepo.

Tukio hil lilitokea juzi usiku katika kitongoji cha Mwaukuliwa katika Kata ya Kilalo wilayani Bariadi na kusababisha nyumba na mazao shambani kuharibika kabisa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakulima wa eneo hilo wameiomba serikali kuwapelekea chakula cha msaada na mbegu za mazao, ili waweze kuendelea na shughuli za kilimo.

Walisema kutokana na mvua hiyo, serikali iwapatie chakula cha kujikimu kwa kipindi hiki, huku wakiendelea na shughuli zao pamoja na kupatiwa mbegu za mazao zinazo komaa kwa muda mfupi.

"Tunaomba serikali ituletee mbegu za muda mfupi ili turudishie mazao yetu, tumeharibiwa mazao mbalimbali pamoja na mifugo imeathirika na mvua ya mawe," alisema Mashili Rozalia ambaye ni mkulima.

Vumilia Jackson, mkazi wa Kata ya Kilalo, alisema nyumba yake iliezuliwa na upepo na watu zaidi ya saba hawana mahali pa kuishi, pia chakula na mazao yao yameharibiwa na mvua hiyo.

Akitoa tathmini ya uharibifu huo, Ofisa Kilimo Kata ya Kilalo, Robert Kipandula, alisema

INAENDELEA UK. 8


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST**

**FOR AERODROME CIVIL CONSTRUCTION WORKS, KIBONDO DISTRICT, KIGOMA REGION**

**Background:**
The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites interested Companies registered by Tanzania Contractors Registration Board, CRB to submit their Request for Expression for Aerodrome Civil Construction Works, Kibondo District, Kigoma Region.

**1. Requirement:**

| TENDER REFERENCE NUMBER | TENDER ITEM DESCRIPTION |
|---|---|
| EOI/19/SUP/001 | Aerodrome Civil Construction Works |

**2. Eligibility:**

To undertake integrated Aerodrome Civil Construction Works – extension of runway with compact marram surface as per ICAO standards, construction of Stone masonry drainage work, supply and pitch on concrete foundation (pit) with perimeter fence of steel column posts fixed with chain link, barbed wire and rolled razor wire.

The complete set of documents can be collected from the following UNHCR Offices:

UNHCR Representation Office Tanzania
Plot 1658 Masaki, Rufiji Street
P.O Box 2666 - Dar es Salaam, Tanzania

UNHCR Field Unit Mwanza
Mwanza Airport
P.O. Box 2273 – Mwanza

UNHCR Sub- Office Kibondo
Kabigwa (Near TANESCO)
P.O. Box 49, Kibondo

UNHCR Field Office Kigoma
Kheri Avenue, Off Bangwe Road
P O Box 1213, Kigoma

UNHCR Field Office Kasulu
Kimobwa (Mlimani Area)
P.O. Box 332 - Kasulu, Kigoma

**CRUCIAL DATE FOR THIS REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST**

| | |
|---|---|
| Deadline for submission of offers | Sunday 17th February 2019 at 16.00 hrs EAT |

215014002

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*

MAHOJIANO MAALUM

# Waziri Jafo: Kanuni Uchaguzi Serikali za Mitaa kufumuliwa

**Na Elizabeth Zaya**


Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo.

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema wizara yake inaendelea na mchakato wa kuzifanyia marekebisho kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kukidhi mahitaji ya demokrasia.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Jafo, alisema wizara yake inasimamia mchakato wa kuboresha kanuni hizo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuimarisha demokrasia nchini.

"Kwa mwaka huu, wizara yangu ina mambo makubwa. La kwanza ni kuimarisha demokrasia,"

"ofisi yangu ndiyo inahusika katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa hivyo, tuko katika mchakato wa maandalizi ya uchaguzi huo.

"Mchakato hivi sasa unaenda vizuri, tumeshaita wadau, hasa katika kanuni zile kuhakikisha uchaguzi unafanyika. Tayari tumeshaita wakurugenzi wa mamlaka husika za serikali za mitaa ambao watakuwa wasimamizi kule.

"Pia tumeshakutana na ma-RAC, wakuu wa mikoa na wadau mbalimbali tunaendelea kukutana nao kwa lengo la kupata kanuni za kutuwezesha kufanya uchaguzi huo.

"Na kanuni hizi mwaka huu 'tunazi-review' kulinganisha na upungufu uliojitokeza huko nyuma kwa kuyafanyia maboresho zaidi.

"Muhimu kwetu ni kuhakikisha tunasimamia uchaguzi huu vizuri zaidi ili watu waweze kushiriki, kwa sababu serikali za mitaa uchaguzi wake ni muhimu, unagusa kila mahali, hasa kule ambako ndiko wananchi wanachukua viongozi ambao wanapanga nao mipango yao ya maendeleo ya kila siku."

**SIRI YA MAFANIKIO**

Mbali na mchakato wa uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu, Jafo alitaja siri ya kung'ara kwake kiutendaji. Tayari Rais John Magufuli ameshaweka wazi kuwa anakoshwa na utendaji wa waziri huyo.

Waziri huyo alisema kung'ara kwake kiutendaji kunatokana na nidhamu aliyonayo katika kuzingatia muda.

"Hii ndiyo siri yangu ya mafanikio, najali sana muda," Jafo alisema, "maisha yangu yote nimekuwa mtumwa wa muda na nikienda 'site' (eneo la mradi) kama mkoani, maana yake nafanya kazi sana mpaka wakati mwingine watu huwa wananishangaa kwanini nafanya kazi hivyo.

"Mfano juzi juzi nilienda Kibondo, niliongea na watu, nikakagua miradi, nikaenda na Kasuru, nikafanya kazi halafu nikaenda na Kigoma. Hiyo ndiyo 'nature' yangu, na mimi niko makini na suala la muda hasa katika kutekeleza dhamana niliyopewa."

Jafo pia alisema huwa anachukia anapoona watendaji wanashindwa kutekeleza ipasavyo majukumu yao na wizi wa fedha za serikali.

**BILIONI 105/-**

Katika mahojiano hayo, Jafo pia alisema wizaya yake mwaka huu imepanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali za wilaya ambao unatarajiwa kuanza wakati wowote.

Alisema tayari Rais Magufuli ameshawapatia Sh. bilioni 105 kwa ajili ya hospitali za wilaya 67 na ameshatoa maelekezo kuwa ifikapo Januari 30, awe amepata picha ya ujenzi wa hospitali hizo.

"Kwanza nimshukuru Rais kwa kuniamini na kunipa dhamana katika wizara hii ambayo ni kubwa, nafurahia kwa sababu 'nature' yangu pia napenda kufanya kazi kwa bidii na nishukuru kwamba tangu tumepata dhamana hii tumefanya kazi kubwa sana katika sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu, miundombinu, afya na mambo mengine yamefanyika kwa ujumla wake," Jafo alisifu.

"Na sasa ninavyozungumza, tumekamilisha na tunaendelea kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya ambavyo mpaka sasa tunaenda na zoezi la ujenzi wa vituo 350 ambavyo vikikamilika, vitafanya ukombozi mkubwa kwa Mtanzania."

Alisema wizara yake mwaka huu pia imepanga kutekeleza miradi ya ujenzi na uboreshaji wa barabara. Alisema wanaendelea kuboresha na barabara zilizoko katika Jiji la Dar es Salaam kupitia mradi wa DMDP na kuboresha barabara zote zilizo katika hali mbaya.

Waziri huyo alisema tayari Sh. bilioni 660 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo na kazi imeshaanza kufanyika.

Alisema kuwa mbali na Dar es Salaam, wanaboresha barabara katika miji mingine saba ikiwamo Arusha, Mbeya, Mwanza, Mikindani na Ilemela ambayo ujenzi unaendelea.

Jafo pia alisema wanaendelea kujenga madampo ya kisasa katika miji ya Dodoma, Arusha, Mikindani, Mwanza na Tanga, akiamini kufikia Desemba mwaka huu, maeneo hayo yatakuwa vizuri.

Alisema kuwa wizara yake mwaka huu imepanga kuboresha miradi ya kuimarisha manispaa na miji, mradi ambao unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 541.

Alisema tayari ujenzi wa barabara za lami unaendelea katika manispaa na halmashauri zote nchini na anaamini mradi huo utakuwa umekamilika kufikia mwakani, huku wakiendelea pia na uboreshaji wa barabara za vijijini.

Jafo alisema mwaka huu wizara yake pia inaendelea kuimarisha sekta ya elimu kwa kuboresha zaidi miundombinu.

"Naona sasa hivi watoto wengi wanafaulu na hiyo inaonyesha imani ya wananchi kwa shule za serikali inarudi kama ilivyokuwa zamani," Jafo alisema na kufafanua zaidi:

"Leo hii unaona kwamba matokeo ya kidato cha nne yakitoka, wazazi wengi, hata kama mtoto alikuwa akisoma shule binafsi, wanataka kuwapeleka kidato cha tano katika shule za serikali, na hii inatokana na kasi kubwa ya uboreshaji wa shule zetu."

Alisema serikali inahakikisha shule zinakuwa na vyumba vya madarasa vya kutosha ili kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu wanaanza masomo kwa wakati.

Alisema tangu serikali ianze kutekeleza ahadi yake ya kutoa elimu bila malipo, kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na waliokuwa wamekata tamaa ya kusoma.

Jafo alisema wizara yake mwaka huu pia imepanga kuendelea kuwawezesha vijana, kinamama na wenye ulemevu kupata mikopo kwa ajili ya shughuli za ujasiriamali. Alisema Sh. bilioni 51 zimetengwa kwa ajili ya kuyawezesha makundi hayo.

"Na bahati nzuri tumepitisha sheria kwamba mikopo hiyo itoke kwa utaratibu maalum, tena bila riba. Eneo hili kwangu mimi ni mtazamo kwamba itasaidia sana hasa katika uanzishwaji wa viwanda vidogo," Jafo alisema.

"Tukumbuke mwaka jana niliitoa agizo kwa wakuu wa mikoa waanzishe viwanda vidogo, vya kati na vikubwa, kila mkoa uwe na viwanda 100, lengo likiwa ni kupata viwanda 2,600.

Faraja niliyonayo ni kwamba kwa ripoti ya awali, viwanda 3,100, kwa hiyo tumepitiliza lengo."

Alisema mwishoni mwa mwezi huu, wanatarajia kutoa ripoti ya tathmini ya viwanda katika mikoa. Alisema ripoti hiyo itaonyesha nani alifanya vizuri zaidi na kwamba ipo mikoa ambayo imefanya vizuri zaidi kuliko mingine.

Alisema ripoti itaorodhesha mkoa wa kwanza mpaka wa mwisho kwa lengo la kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda nchini.

Katika mahojiano hayo, Jafo alisema kumekuwa na mafanikio na mapinduzi makubwa ya maendeleo katika serikali ya awamu ya tano.

"Miaka mitatu ya serikali ya awamu ya tano ni fahari kubwa kwa Watanzania na maana yake imeweka nyota inayong`ara na watu wengine."

## HABARI KITAIFA




Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, akizungumza na wanafunzi wanaotarajia kwenda Ufaransa kujifunza lugha hiyo, wakati wa ufunguzi wa kitivo cha ufadhili wa masomo kiitwacho Campus France jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Wafanyakazi wachachamaa wadai mishahara ya miezi 3

**Na Boniface Gideon,** TANGA

ZAIDI ya wafanyakazi 300 wa kiwanda cha Ngomeni Kamba (Tancord), kinachomilikiwa na Kampuni ya Katani Ltd., wilayani Muheza mkoani Tanga, wameandamana kudai mishahara yao ya miezi mitatu, huku

wakilalamika kutoingiziwa michango yao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa miezi 10.

Mwandishi wa gazeti hili aliyefika kiwandani hapo, aliwakuta waandamanaji hao wakiimba wimbo wa kutaka haki yao na kuchoka kunyanyaswa huku wakisema kampuni hiyo imefilisika, lakini haitaki kusema ukweli.

Baadhi ya wafanyakazi hao walisema kuwa kuanzia mwezi Oktoba, mwaka jana hawajapata mishahara yao, huku wakiambulia ahadi zisizo na mwisho.

Walisema kuwa mpaka sasa wanasikitishwa na uendeshwaji wa kiwanda hicho kwa kuwa wanafanya kazi bila malipo na kueleza kuwa kama mkurugenzi ameshindwa kukiendesha kiwanda, apishe wawekezaji wengine wenye nia ya kukuza uchumi wa viwanda.

Kufuatia adha hiyo, wafanyakazi hao walimwomba Rais John Magufuli kuingilia kati suala hilo kwa kuwa yeye ni mtetezi wa wanyonge na wao dhamira yao ni kuhakikisha Tanzania ya viwanda inafikiwa na wanafanya kazi kama sera yake inavyosema kuwa hapa kazi tu.

"Kila siku ni tarehe, tumechoka mpaka leo hatujapata chochote humu mashambani mihogo tumemaliza kwa kula kila siku mpaka mchango yanageuka kwa ajili ya kula mihogo tumechoka isitoshe tumeshafanya kazi iweje leo watuambie kwamba

INAENDELEA UK. 8

# Sekretarieti yapewa neno mchakato wa ajira

**Na Mwandishi Wetu**

SEKRETARIETI ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imetakiwa kuendelea kutenda haki katika kuratibu mchakato wa ajira, ili kuiwezesha serikali kupata watumishi wenye sifa stahiki na maadili mema, ambao watatoa huduma kwa umma kwa kuzingatia weledi na kuwajali wananchi ambao ndio walengwa wakuu wa huduma zinazotolewa na taasisi za umma.

Hayo yamesemwa jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, alipokuwa akizungumza na watumishi wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi hiyo jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji, kufahamu kwa kina majukumu ya sekretarieti hiyo na kujiridhisha namna inavyotekeleza majukumu yake.

Mwanjelwa alisema Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni chombo ambacho kinatakiwa kutenda haki ili serikali ipate watumishi wenye sifa na vigezo watakaoendana na kasi ya Rais John Magufuli ya kuliletea taifa maendeleo.

Mwanjelwa alisema awali sekretarieti hiyo ilikuwa ikilalamikiwa sana kuwa mchakato wa kuomba kazi serikalini ulikuwa ukichukua muda mrefu kiasi cha waombaji kusahau kama waliwasilisha maombi, hivyo alipongeza kwa kubuni mfumo wa upokeaji wa

INAENDELEA UK. 8

# Katibu Tawala ataka taarifa walioshindwa kuripoti shule

**Na Dege Masoli,** HANDENI

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Handeni, Boniphace Maiga, amewataka watendaji kata, tarafa na vijiji wilayani humo, kuwasilisha taarifa ofisini kwake za wanafunzi walioshindwa kuripoti shuleni kutokana na kupata ujauzito.

Maiga alitoa wito huo wakati wa mkutano wa wadau wa elimu wa halmashauri ya wilaya hiyo uliofanyika mjini Handeni na kuandaliwa na asasi isiyo ya kiserikali ya Tree of Hope nchini kwa ufadhili wa Shirika la Foundatino for Civil.

Alieleza lengo la kuwataka viongozi hao ofisini kwake kuwa ni kueleza namna ya walivyoyashughulikia matukio ya wanafunzi walioshindwa kuripoti shuleni kutokana na tatizo la kuwa na ujauzito ikiwamo hatua walizochukua dhidi ya wahusika wa mimba hizo.

"Waje waniambie pia namna ambavyo wamepambana katika kuyashughulia mambo hayo kwenye maeneo yao, ili kuhakikisha hayajitokezi wakati mwingine na hivyo kutoa fursa kwa wanafunzi kupata elimu," alisisitiza Maiga.

Aidha, aliitaka jamii yenye maeneo ambayo yameguswa kwenye tatizo la mimba kwa wanafunzi ambao walipaswa kuendelea na masomo, lakini

INAENDELEA UK. 8

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya kuzalisha umeme kutoka kwa kampuni mbili. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za waombaji pamoja na aina ya leseni zilizoombwa zimetolewa hapa chini:

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Taarifa za Wana Hisa | Maelezo ya Mtambo na Matumizi | Aina na Muda wa Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Tanzania Cigarette Public Limited Company, P. O. Box 40114, Dar- es- Salaam. | Kitalu Na. 20, Barabara ya Nyerere, Dar-es-Salaam. | 1) JT International Holding B.V14, 14 Chemin Rieu Geneva-1211, Switzerland- 75%. 2) Kingsway Capital Advisors LLP, 8th Floor 6 New Street Square, New Fetter Lane, Lo, United Kingdom- 9.3% 3) General Public, C/o CAD Securities, P. O. Box 23116, Tanzania- 7% | Kutumia gesi asilia kuzalisha Megawati 3.8 kwa matumizi binafsi ya kiwanda. | Leseni ya kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi kwa kipindi cha mwaka mmoja (1). |
| 2. | STAMIGOLD Company Limited, P. O. Box 4958, Dar- es- Salaam. | Kitalu Na.417/418 Barabara ya Umoja wa Mataifa, Dar- es- Salaam. | STAMIGOLD Company Limited- 100% | Kutumia diseli kuzalisha Megawati 6.0 kwa matumizi binafsi mgodi. | Leseni ya kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi kwa kipindi cha miaka kumi na tano (15). |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi kabla ya saa 10 jioni ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Maombi ya leseni yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**

215013102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba kazeni buti bado mna nafasi robo fainali

**WAWAKILISHI** pekee wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, juzi walikubali kichapo cha kwanza katika hatua ya makundi wakiwa ugenini DR Congo.

Simba ambayo ipo Kundi D pamoja na Al Ahly ya Misri, JS Saoura ya Algeria na AS Vita, juzi ilikubali kipigo cha aibu cha mabao 5-0 ugenini kutoka kwa timu hiyo ya DR Congo.

Kipigo hicho kimekuja ikitoka kushinda 3-0 dhidi ya JS Saoura katika mechi yake ya kwanza kwenye hatua hiyo ya makundi.

Hata hivyo, kwa soka ililoonyesha Simba kwenye mechi yake ya awali nyumbani, linatupa imani kubwa ya timu hiyo ya mtaa wa Msimbazi jijini Dar as Salaam, kuendelea kufanya vizuri kwenye mechi zijazo.

Sote tunatambua ugumu uliopo katika michuano hii inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kwa timu kuweza kupata ushindi ugenini, ingawa kipigo cha mabao 5-0 kilikuwa kikubwa mno ukilinganisha na ubora wa Simba wa sasa.

Tumeshuhudia JS Saoura ikichezea kichapo hapa jijini Dar es Salaam kutoka kwa Simba, huku pia AS Vita ikipigwa 2-0 ugenini Misri dhidi ya Al Ahly.

Hivyo matokeo iliyoyapata Simba ugenini dhidi ya AS Vita, si kitu cha kushangaza na wala kukatisha tamaa kwa kuwa hata Brazil iliwahi kuchapwa mabao 7-1 mechi ya nusu fainali ya Kombe la Dunia 2014.

Hivyo katika michuano hii yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, kikubwa ni Simba kuhakikisha kwanza haifanyi makosa kwenye michezo yake miwili ya nyumbani.

Hata hivyo, kupata ushindi ama sare kwenye mechi zake mbili za ugenini zilizobaki dhidi ya Al Ahly Februari 2, mwaka huu na JS Saoura itakuwa ni hatua moja kubwa katika kujihakikisha nafasi ya kutinga robo fainali ya michuano hiyo.

Tunaamini hilo linawezekana endapo maandalizi ya kina nje na ndani ya uwanja yatafanyika kabla ya Simba kuifuata Al Ahly, lakini kubwa likiwa ni kuwajenga wachezaji kisaikolojia zaidi ili kuwarejesha mchezoni.

Kwa soka la Simba, inalolionyesha ikiwa uwanja wa nyumbani wapinzani wake wote wanatambua ni vigumu kuweza kuambulia angalau pointi moja Uwanja wa Taifa.


Kwa mantiki hiyo, Simba inatakiwa kuhakikisha mechi ijayo inapata pointi ugenini Misri ili kujiweka katika nafasi nzuri zaidi ya kufuzu hatua ya robo fainali.

Hiyo ni kutokana na Al Ahly kulazimisha sare ya bao 1-1 ugenini Algeria dhidi ya JS Saoura, hivyo kushika usukani wa Kundi D ikiwa na pointi nne moja mbele ya AS Vita na Simba.

Nipashe kama wadau wakubwa wa soka, tunaahidi kuendelea kuiunga mkono Simba wakati huu ikibeba jukumu la kuipeperusha bendera ya nchi kimataifa.

Tunaitakia maandalizi mema Simba, wakati huu tukiamini huu ni mwaka wa Tanzania kufanya vizuri kimataifa kuanzia ngazi ya klabu hadi timu za taifa, hasa tukizingatia Serengeti Boys itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Afrika, Afcon U-20 itakayofanyika jijini Dar as Salaam Aprili mwaka huu na wakati huo huo Taifa Stars ikiwa katika nafasi nzuri ya kufuzu Afcon 2019 ya wakubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ndemla bidisha 'guu' usirudi soka la Bongo

Na Adam Fungamwangowango

**HUU** ni zaidi ya mwaka wa nne sasa huwa nasikia kiungo wa Simba, Said Ndemla, anatakiwa na timu za Ulaya.

Lakini cha ajabu ni kwamba mchezaji huo aliyetoka kwenye kikosi cha pili cha Simba, ameendelea kubaki hapa hapa, licha ya kila msimu kuwa na habari za kutakiwa kwenda kucheza soka nje ya nchi.

Ndemla mwenye umri wa miaka 22, Novemba mwaka juzi, alikwenda nchini humo kufanya majaribio kwenye klabu ya AFC Eskilstuna, lakini hakuna majibu yenye kueleweka yaliyowekwa wazi, matokeo yake alirejea na kuendelea kuitumikia Simba, tena kwa kusaini mkataba mpya. Wakati kila shabiki wa soka akiwa amechoshwa na stori hizo za kila msimu, kiungo huo mwenye mashuti makali ya mbali yupo nchini Sweden akifanya majaribio mafupi katika klabu ile ile ya AFC Eskilstuna ya Ligi Kuu ya Sweden.

Kwa mujibu wa Meneja wa mchezaji huyo, Said Suleiman Sharrif, tayari kiungo huyo akiwa ameongozana na mshambuliaji mwingine chipukizi wa timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 20, Rashid Chambo wa JKT Ruvu, wameshaanza majaribio.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo Nemanja Miljanovic, amesema hii ni nafasi nyingine ya mchezaji huyo kujiridhisha juu ya uwezo wake kwa majaribio mafupi tu wiki hii.

Baada ya muda mrefu, mimi naiona kama hii ndiyo nafasi pekee ya mwisho kwa Ndemla kudhihirisha ubora wake ili abakie Ulaya na kuanza maisha mapya.

Mashabiki wengi wa soka walikuwa wakimtabiria kuwa hatomaliza soka lake kabla hajacheza nje ya nchi.

Anachotakiwa kufanya ni kutowaangusha mashabiki wake kwa kufanya vema kwenye majaribio hayo.

> **Baada ya muda mrefu, mimi naiona kama hii ndiyo nafasi pekee ya mwisho kwa Ndemla kudhihirisha ubora wake ili abakie Ulaya na kuanza maisha mapya.**

Nadhani Ndemla atakuwa ametoka kambini kwenye klabu ya Simba na kwenda huko, na kama ni hivyo hilo litamsaidia sana kwenye majaribio yake, kwa kuwa wachezaji wengi wa Kibongo wamekuwa wakishindwa majaribio siyo kwa sababu hawana vipaji, bali uwezo wa kuhimili mazoezi magumu ndiyo tatizo.

Wengi wanakwenda kwenye majaribio wakiwa wametokea majumbani, wakiwa wamekaa wiki nzima kwenye maisha ya mtaani, hivyo kwenda huko mwili ukiwa umechoka, hawana nguvu wala stamina, hivyo kuonekana hawawezi kumudu mikikimikiki ya huko.

Kiungo huyo anatakiwa kufanya juhudi zote, ufundi wote na kuonyesha kipaji alichojaliwa nacho kwa sababu kama akifeli hapo, sidhani kama anaweza tena kupata nafasi adhimu kama hiyo.

Kwa sasa anaonekana kupoteza nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Simba ambacho kina viungo kama Claotus Chama, Haruna Niyonzima na Hassan Dilunga, hivyo anatakiwa kutotaka tena kurejea nchini ili kukaa benchi.

Tumeona baadhi ya wachezaji wanaofeli majaribio na kurejea, baadaye wanashindwa kuendelea hata na zile timu walizokuwa nazo na kwenda kwenye klabu za chini yake.

Ndemla aepuke kurejea nchini na baadaye kwenda klabu za Mtibwa, Kagera Sugar, au Ndanda kama baadhi ya wachezaji huko nyuma, bali miguu yake ifanye kazi ya kumshawishi kocha ili amkubali na uwezo huo anao. Huu ndiyo wakati wake sasa wa kucheza Ligi Kuu Ulaya baada ya matarajio ya muda mrefu. Kila la kheri Ndemla.

BARUA/MJADALA

# Barabara Kivule hali mbaya

**Mhariri,**

*HAKUNA shaka, maeneo ya Kitunda na vitongoji vyake ndani ya Jiji la Dar es Salaam, yameshakuwa maarufu kwa mengi sana.*

*Kwa yeyote mzoefu aliye ndani ya Jiji, analifahamu vyema eneo hilo ambalo ni sehemu ya Wilaya ya Ilala na Jimbo la uchaguzi Ukonga, iwe kwa kupahafamu fika au japo kwa kusikia na kupata taarifa zake.*

*Huo ni umaarufu ambao bado unakabiliwa na shida moja kuu, kwamba barabara ya kufika huko usafiri wake ni mtihani mkubwa, hasa katika kipindi cha mvua nyingi.*

*Mathalani, barabara ya lami kuanzia eneo la Ukonga Banana jirani na Shule ya Airwing hadi Kitunda, Njia Panda ya Msikitini, hali ni mbaya kuna mashimo mengi sana.*

*Baada ya hapo si barabara ya lami, kunakoendeleza mashimo hasa katika kipindi hiki mvua zimeanza. Nijumuishe tu simulizi ni hizo hadi kufikia Kitunda Kivule na kwingineko, hali si nzuri kabisa.*

*Hufika wakati fulani msimu wa mvua, wenye magari wanalazimika kuacha vyombo vyao vya usafiri katika eneo la Banana na kukwea bodaboda kwenda majumbani, vivyo hivyo katika utaratibu wa kurudi makazini.*

*Sasa huu nasema ni mtihani. Nakumbuka aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abbas Kandoro, kuna wakati alieleza mikakati ya ujenzi wa barabara ya jijini Dar es Salaam, akitaja mbili muhimu.*

*Moja ni kati ya Banana hadi Mvuti Chanika na nyingine kati ya Majumba Sita, Ukonga na Mbezi, ambayo inatumika na imeshakuwa maarufu kwa umma.*

*Naaamini bado iko katika mipango, ila msisitizo wangu ni kwamba, itekelezwe mapema kuleta nafuu kwa wakazi wa Kitunda wanaotaabika, lakini pia kurahisisha usafiri wa kwenda Chanika, kama ilivyo kwa Mbezi - Majumba Sita.*

**Masru David,**
**Kipunguni Ukonga,**
**Dar es Salaam.**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Ligi ya Wanawake ni mgodi unaotembea




**Na Adam Fungamwango**

KABLA ya mechi ya Simba Queens na Yanga Princess iliyochezwa Januari 13, mwaka huu, si mashabiki wengi wa soka nchini waliokuwa wanajua kuwa kuna Ligi Kuu ya Wanawake ikiendelea.

Ni kama ligi hiyo ilikuwa inachezwa shimoni kwa kificho.

Lakini baada ya mechi hiyo na Simba Queens kuiadhibu Yanga Princess mabao 7-0, katika hali ya kushangaza kumeibuka mashabiki wa soka ambao wameshaanza kuifuatilia ligi hiyo.

Kwanza kabisa baada ya mechi hiyo, mitaani kulizuka ubishi wa hali ya juu kwa mashabiki wa Simba na Yanga wakitaniana kuhusu matokeo hayo.

Mashabiki wa Simba walikuwa wakiwatania wenzao wa Yanga kuwa wamewatundika mabao 7-0, huku wenzao wakijitetea kuwa hiyo ni michuano ya mechi za wanawake.

Hata hivyo, wale wa Simba wanasisitiza kuwa hata kama ni wanawake ni wa Yanga tu, na wamefungwa na wanawake wa Simba, hivyo utani wa jadi ni lazima uendelezwe tu.

Wakati Yanga walipokuwa wakiwatania wenzao wa Simba kufungwa kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam FC, Simba walijibu mapigo kuwa wanafurahia ushindi wa Azam wakati wao wamefungwa mabao 7-0.

Si nia yangu kuleta maneno ya utani wa mashabiki wa klabu hizo kongwe nchini, ila nataka kueleza jinsi wengi walivyoonekana kuhamasika na mechi hiyo ya wanawake, kiasi cha nchi nzima siku hiyo kujua kulikuwa na pambano hilo.

Baada ya hapo waandishi wa habari waliamka na kuanza kufuatilia kwa nguvu zote ligi hiyo, kiasi kwamba mechi zilizofuata zilianza kuandikwa kwa uzito mkubwa, wachezaji wa ligi hiyo nao wakapata fursa ya kuhojiwa na kujulikana kwenye vyombo vya habari na hata mitandao ya kijamii.

Hata mechi ya JKT Queens ilipoifunga Simba bao 1-0, ilifuatiliwa na mashabiki wengi ambao tayari walishaanza kuifahamu ligi hiyo. Hapa tunaona kuwa kama Shirikisho la Soka nchini (TFF) na klabu zitakaa na kupanga mikakati hasa ya matangazo, wanaweza kuvuna pesa kwenye Ligi ya Wanawake ambao inaendeshwa kwa ukata mkubwa.

Inaonekana kabisa kuwa TFF na klabu hasa za Simba na Yanga ambazo zinaweza kabisa kuhamasisha mashabiki kuangalia, kusikiliza au kufuatilia ligi hiyo, haziitilii maanani kama ilivyokuwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nina uhakika kuwa kama kutakuwa na matangazo ya kutosha juu ya ligi hiyo kutoka kwa TFF na klabu zenyewe, basi zinaweza kushawishi mashabiki kwenda viwanjani kuangalia timu zao, lakini pia kufuatilia kinachoendelea.

Hali hii ikiendelea huko mbele ndipo inawezekana kabisa ligi ikapata hata mdhamini wa kuanza kuonyesha mechi kwenye luninga na huo ndiyo mwanzo na kuifanya ligi hiyo kuwa na mvuto na kuingiza pesa TFF na kwenye klabu, hata kama hazitokidhi mahitaji yote, lakini zinapunguza gharama za uendeshaji.

Licha ya kampuni kudhamini ligi, klabu binafsi zinaweza kupata wadhamini binafsi, lakini pia hata wale wa kuweka matangazo kwenye mabango uwanjani.

Kuna kampuni mbalimbali nchini za vipodozi vya kinamama, urembo, vyakula, viungo vya mapishi, nguo za kinadada na watoto na zingine nyingi ambazo huenda zikaja kuwekeza, lakini haziwezi kuja tu hivi hivi mpaka kuwe na hamasa ya kutosha kuwaleta mashabiki uwanjani, lakini pia mechi kuonyeshwa kwenye TV ili na nao wanufaike.

TFF na klabu zisikarir kuwa soka la wanaume tu ndilo linaweza kuwaingizia pesa, wakati mwingine ni lazima wawe na ubunifu wa kutafuta maeneo mengine ya kuweza kukusanya mapato.

Nilivyoona mimi kwenye Ligi ya Wanawake kinachokosekana ni hamasa tu, lakini walewale mashabiki wa soka la wanaume, ndiyo hao hao wanaweza kabisa kugeuzwa kuwa pia mashabiki wa soka la wanawake.

Wakihamasishwa mashabiki wa Simba kwenda kuiangalia timu yao ikicheza na Marsh Academy, basi hata mashabiki wa Yanga watakwenda kuzomea.

Kikubwa ni kwamba mashabiki waelimishwe kuwa timu ya wanaume na wanawake, wote ni klabu moja tu, hivyo wajitoe kwa hali na mali na si kubagua.

Hapa ndipo TFF pamoja na klabu zitakapoanza kuona faida ya ligi hiyo kwa kuwa mashabiki watakwenda viwanjani, lakini pia wanaweza kupata wadhamini hata tu wa kuonyesha mechi na huo ndiyo mwanzo wa kuelekea kwenye mafanikio.

Mfano hivi sasa TFF ingekuwa inahaha kuzungumza hata na mwenye kibali cha kuonyesha Ligi Kuu, waonyeshe hata mechi ya mzunguko wa pili ya Simba na Yanga ya wanawake ili kutoa hamasa.

Ligi ya Wanawake ni mgodi unaotembea kama TFF na klabu zitakaa pamoja na kuangalia fursa.

KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Katibu Tawala ataka taarifa walioshindwa kuripoti shule

INATOKA UK. 5

wameshindwa kwenda kutokana na kupata ujauzito kutoa taarifa kama siyo kufika ofisini kwake ili waeleze changamoto hizo.

Alisema serikali wilayani humo haitakubali kuona mtoto wa kike haendi shule kutokana na ujauzito na kwamba watapambana na kila atakayetajwa kuhusika.

Alisema suala la mimba za utotoni zinachangiwa na ushawishi na kwamba wanaowashawishi ni miongoni mwa watu ambao wanafahamika ndani ya jamii na uongozi huo ulishatoa maelekezo kwa kuwashughulikia wanaoshawishi ili kuwafanya watoto wazingatie masomo.

Hatua ya Katibu Tawala huyo inatokana na taarifa ya mradi huo wa uhamasishaji, uwajibikaji wa jamii na mamlaka zinazohusika katika kuboresha huduma za elimu katika jamii iliyowasilishwa na Mratibu wake, Goodluck Malilo, ikibainisha udhaifu kwa viongozi kwenye uwajibikaji wakati wa ziara yao.

Pia katika taarifa hiyo ilionyesha upungufu huo ikitaka kuchukuliwa hatua ili kufikia matarajio ambayo wanategemea ili kuwaepusha wanafunzi kupata ujauzito na kuacha kuendelea na masomo.

Maeneo yaliyofanyiwa ziara na asasi hiyo ni kwenye vijiji vya Kwedizinga, Michungwani, Kabuku na Komsanga pamoja na kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali na kubaini kuwapo kwa tatizo hilo katika maeneo hayo.

Aidha, Malilo alieleza bado kuna changamoto kwa wazazi kushiriki kutowapa elimu watoto kwa kutotimizia mahitaji muhimu ya shule ikiwamo kuwashirikisha kazi zao za usiku kuuza vitu kwenye magenge kwa kutoona umuhimu wa shule.

Naye Mkurugenzi wa asasi hiyo, Fortunata Manyeresa, alisema tatizo la mimba kwa watoto wa kike linasikitisha kutokana na baadhi ya wazazi na walezi kutuhumiwa kushiriki kuwaficha waliohusika na mimba hizo.



Meneja wa Benki ya Stanbic Tanzania Nyanda za Juu Kusini, Hemedi Sabuni (Kulia) pamoja na Mgeni rasmi, Dk. Samwel Khamad wakifungua jiwe la tawi jipya la Benki ya Stanbic lililopo Mbeya katika hafla fupi ya uzinduzi iliyofanyika jana. Benki ya Stanbic imedhamairia kuongeza upatikanaji wa huduma za kibenki nchini, ili kuwezesha mafanikio ya kiuchumi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyakazi wachachamaa wadai mishahara ya miezi 3

INATOKA UK. 5

pesa hakuna? Huyu mkurugenzi ni sharobaro hatumtaki hawezi kuendesha hiki kiwanda," alisema mmoja wa wafanyakazi hao.

Aidha, walidai kuwa pamoja na mishahara wanadai fedha za Saccos, michango ya mifuko ya jamii na michango kwa ajili ya misiba ambayo hawakuwahi kupatiwa licha ya kuwa na mshahara mdogo wa laki moja kwa mwezi.

Mwenyekiti wa chama cha wafanyakazi (TPAWU), Geofrey Mgorigo, alipozungumza na gazeti hili, alikiri kuwapo kwa madai hayo na kusema kuwa kwa mujibu wa taarifa alizozipata chanzo ni kuyumba kwa uchumi wa kampuni hiyo na kuwa hatima ya suala hilo wameichia kampuni ili ijue nini cha kufanya.

Nipashe ilipokwenda ofisini kuonana na uongozi kujibu lawama zinazowakabili, akiwamo Meneja mwajiri, Mwaita Kinanda pamoja na Mkurugenzi mwendeshaji, Damson Mselela, walikimbia na kujifungia ndani na baada ya kelele za wafanyakazi walilazimika kufungua mlango.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi mwendeshaji Mselela, alisema kuwa suala hilo liko katika mchakato wa kushughulikiwa ili kupata ufumbuzi kwa kuwa wakurugenzi wote wa kampuni mama ya Katani Ltd., wapo jijini Dar es Salaam na kuahidi kuwa majibu ya hatima yao watayapata siku ya Jumanne (kesho).

# Sekretarieti yapewa neno mchakato wa ajira

INATOKA UK. 5

maombi ya kazi na mfumo wa kupanga wasailiwa waliofaulu ambao kwa kiasi kikubwa umepunguza malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na waombaji wa ajira serikalini na kuongeza kuwa, hivi sasa mchakato wa ajira mpya unachukua siku 52 tu licha ya kuwapo taratibu nyingi zinazozingatiwa kukamilisha mchakato mzima.

Mwanjelwa alifafanua kuwa mfumo huo una kanzi data ya waombaji wote waliofanyiwa usaili na kupata ufaulu mzuri, lakini kutokana na uwapo wa fursa chache za ajira, hawakupangiwa vituo vya kazi, hivyo unaiwezesha serikali kupata watumishi kwa wakati wanapohitajika haraka katika Taasisi za Umma.

Katibu wa Sekretarieti hiyo, Xavier Daudi, alisema ofisi yake ilianzishwa kwa lengo mahususi la kukabiliana na changamoto za ajira zilizokuwa zikijitokeza awali, hivyo iliundwa ili kuongeza uwazi, kutenda haki na kuhakikisha kuwa ajira zinapatikana kwa kuzingatia sifa.

Alisisitiza kuwa, ofisi yake kwa kushirikiana na waajiri inazingatia sera ya ajira, sheria, kanuni na taratibu katika kusimamia mchakato wa ajira katika utumishi wa umma kwa lengo la kuiwezesha serikali kupata watumishi wenye sifa na maadili mema watakaoisaidia kufikia malengo yake makubwa iliyojiwekea.

Naye, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Sekretarieti, Mbarak Abdulwakil, alimshukuru Mwanjelwa kwa kuitaka sekretarieti kuzingatia weledi katika jukumu zito la kuwezesha ajira za watumishi wa umma na kumhakikishia kuwa maelekezo yote aliyoyatoa yatatekelezwa kikamilifu.

# Hasunga awaonya warasimu

INATOKA UK. 3

kuwa kilimo sio suala la dharura na kina mahitaji ya kila mwaka, hakuna sababu ya msimu ufike

ndipo tuanze kushughulika na wakulima, hilo sitalivumilia."

Katika hatua nyingine waziri alisema kuwa kilimo lazima kiende sambamba na uwapo wa viwanda, dhamira inayosimamiwa vyema na serikali ya awamu ya tano ili viweze kuchakata bidhaa za kilimo.

"Dhamira yetu ni kuona viwanda vinashamiri nchi nzima, tupo tayari kuingia ubia ili kujenga kiwanda kikubwa cha uchakataji wa tumbuku hapa Tabora, lakini pia nimeagiza mamlaka zilizopo hapa zinaendelea kutafuta wawekezaji wa viwanda vingine hususani vya mbolea

ili kumrahisishia mkulima katika kupata pembejeo," alisema waziri.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa inafanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuagiza pembejeo za kilimo nje ya nchi, ili kuhakikisha mkulima

wa Tanzania anainuka kiuchumi na kufikia azma ya serikali ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

# Mvua yaharibu ekari 300

INATOKA UK. 3

mvua hiyo imeharibu zaidi ya ekari 300 za mazao ya wakulima.

Alisema mazao ya chakula na biashara yameharibiwa na mvua hiyo, ambapo ekari za pamba 161, mtama ekari 47 na mahindi ekari 110.5.

"Wakulima walikuwa wamehamasika kulima mazao ya chakula na biashara, ikiwamo pamba, mahindi, choroko, mtama, lakini leo mazao hayo yameharibiwa na mvua ya mawe iliyoambatana na upepo kwa jumla ya ekari 318," alisema Kipandula.

Kwa upande wake Diwani wa kata hiyo, Benjamini Nyasilu, alisema mvua hiyo ni janga kubwa kwa wakulima hao, janga ambalo limewaharibia chakula na kuwaondolea matumaini tena.

Alisema mvua hiyo imeharibu mazao ya wakulima katika kitongoji cha Mwaukuliwa, ambapo kwa sasa wakulima hao wana hali ngumu kimaisha baada ya mazao na vyakula vyao majumbani kuharibiwa na mvua.

"Wakulima wamelima mahindi na mtama kwa ajili ya chakula, pamba kama zao la biashara, lakini leo mvua imeharibu mazao haya...tunaiomba serikali isikie kilimo chao iwapatie chakula na mbegu ili waendelee na shughuli za kilimo," alisema Nyasilu.

# Mkuu wa KKKT

INATOKA UK. 3

Kabla ya kutoa neno hilo, Askofu Dk. Shoo alizindua na kuweka wakfu jengo la Usharika wa Kimashuku ambalo hadi kukamilika kwake, limegharimu Sh. milioni 495.97.

Kamati ya ujenzi huo iuiongozwa kwa miaka kadhaa na David Mariale ambaye sasa ni marehemu na alifanya kazi kubwa ya kukusanya michango kutoka kwa washarika na marafiki wa KKKT.

Aidha, katika ibada hiyo, Askofu Dk. Shoo aliweka jiwe la msingi nyumba ya mchungaji wa usharika huo ambayo hadi kukamilika kwake itagharimu zaidi ya Sh. milioni 70.

Nyumba hiyo kwa sasa ambayo imefikia hatua ya upauzi, imewagharimu kiasi cha Sh. milioni 20, ambapo nguvu kazi ya wananchi ni Sh. milioni 3.3.

Katika ibada hiyo, Dk. Shoo aliongozana na maaskofu wastaafu wa Dayosisi ya Kaskazini, Dk. Martin Shao na Askofu Dk. Erasto Kweka; Mkuu wa Jimbo la Hai, Aminirabi Swai; Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi hiyo, Elingaya Saria na wachungaji zaidi ya 40.

HABARI KITAIFA

# Takukuru yatoa angalizo trafiki

**Na Margaret Malisa,**
PWANI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewataka madereva wanaotumia barabara za mkoa wa Pwani kutoa taarifa za rushwa wanapoombwa na askari wa usalama barabarani.

Wito huo ulitolewa jana na Naibu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Pwani, Sadik Nombo, wakati akitoa taarifa ya miezi mitatu kwa waandishi wa habari.

Nombo alisema kumekuwapo na malalamiko ya kuombwa rushwa madereva na askari, lakini wanaotoa taarifa hizo sio madereva wenyewe.

Aliwataka madereva kupiga simu au kutumia njia yoyote kufikisha taarifa katika ofisi hiyo, ili kukomesha vitendo vya rushwa vinavyolalamikiwa kila siku.

Aidha, aliwakumbusha askari wa usalama barabarani kutoa taarifa za madereva wanaowashawishi kuwapa rushwa kama walivyokubaliana kwenye kikao cha pamoja kutafuta namna ya kukomesha rushwa barabarani.

Kadhalika, alisema wamepokea malalamiko 93 yanayohusiana na vitendo vya rushwa, ambapo kati ya hayo 20 kutoka serikali za mitaa, ardhi 16, polisi 9, taasisi binafsi 9. mahakama 8, afya 4, ujenzi 4, maliasili moja, TRA moja, Tanesco 2, Sumatra moja.

Malalamiko mengine ni kutoka Dawasa 3, Maendeleo ya Jamii 3, Tasaf moja, Uvuvi moja, Viwanda moja, Ushirika moja, Mipango moja na Manunuzi moja.

Katika kipindi hicho cha miezi mitatu Takukuru ilifuatilia miradi tisa ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.4, ambapo miradi mitatu yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.3 ilitiliwa shaka na uchunguzi unafanyika.

# TADB, NFRA zawatangazia wakulima neema soko mahindi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), kwa kushirikiana na Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula (NFRA), wameingia makubaliano kuongeza thamani ya mnyororo wa thamani wa zao la mahindi kwa kuhakikisha wakulima wa zao hilo wanapata soko la uhakika ili waweze kunufaika na kilimo.

Akizungumza baada ya kumaliza kikao cha pamoja, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema wamekubaliana na NFRA kuhakikisha zao la mahindi linapata soko, jambo litakalompa uhakika mkulima kuendelea na kilimo cha zao hilo.

"TADB ilishatoa zaidi ya Sh. bilioni 3.4 kwa vikundi 22 vya wakulima

katika kufanya kilimo cha kisasa cha zao la mahindi, hivyo kupitia kikao hiki tunawahakikishia wakulima wa mahindi soko la uhakika," alisema Justine.

Alisema kwa msimu wa kilimo uliopita soko la zao la mahindi liliyumba, hivyo kupitia mazungumzo kati ya TADB na NFRA yataibua matumaini kwa wakulima wengi wa mahindi kwa kupata soko la bidhaa hiyo ambayo bei yake ilishuka kutokana na uzalishaji kuongezeka tofauti na mahitaji ya nchi.

"Pamoja na Shirika la Chakula Duniani (WFP) kununua zaidi ya tani 36,000 za mahindi bado shehena nyingi za mahindi zipo kwa wakulima, hivyo kama wadau wa sekta ya kilimo ni wajibu wetu kuhakikisha shehena hizo zinapata soko," alisema.

Hivi karibuni, Rais John Pombe Magufuli alishuhudia utiliaji saini wa makubaliano Ikulu jijini Dar es Salaam kati serikali kupitia Wizara ya Kilimo na WFP kuhusu kununua kiwango kikubwa cha mahindi.

Justine alisisitiza kuwa ili kumfanya mkulima kuendelea na kilimo cha zao hilo ni lazima ahakikishiwe soko la bidhaa yake itakayompa hamasa ya kulima kwa tija ili aweze kupata mavuno kwa wingi na tija inayotakiwa sokoni.

"TADB itaanda mkakati wa pamoja na NFRA utakaoleta mabadiliko makubwa katika mnyororo wa thamani wa zao la mahindi nchini, hii ni kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika msimu wa kilimo uliopita ulifanya zao la mahindi kushuka thamani," alisema Justine.

Aliongezea kuwa kupitia mikataba wanayoingia NFRA na wanunuzi kutoka nje ya nchi itatupa mwongozo wa kuhamasisha kilimo nchini kwa kuwakopesha wakulima kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima wadogo (SCGS) katika kufanya kilimo chenye tija na kukidhi mahitaji ya soko.

Alisema lengo ni kuhakikisha bei ya zao hili sokoni inakuwa ya kumnufaisha mkulima kwa kipindi chote cha msimu hali itakayomfanya mkulima kurudisha fedha yake na kupata faida itakayomsababishia kufanya maendeleo.

"Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli imejipambanua kuboresha mazingira ya wananchi wa hali ya chini wakiwamo wakulima, hivyo TADB kwa nafasi yetu tunaendelea kutekeleza azma ya serikali kwa kuboresha mazingira kwa wakulima nchini," alisema Justine. kwa upande wake Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa NFRA, Vumilia Zikankuba, alisema wamefanya mazungumzo mazuri na TADB ambayo yatawasaidia kama wakala katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha zao la mahindi linapata soko.

"NFRA imejipanga kupunguza utegemezi kwa serikali katika kufanya shughuli zake, hivyo tunashirikiana na wadau wa kilimo na taasisi za kifedha kama TADB kutuwezesha fedha zitakazotusaidia kuendesha shughuli zetu za uhifadhi wa mazao na kujenga masoko," alisema Zikankuba.

Alisema kupitia mazungumzo yetu tunauhakika wa kupata fedha zitakazo tuwezesha kununua mahindi kutoka kwa wakulima, hivyo kutoa uhakika kwa mkulima kuwa soko la zao hili lipo na kama wakala tutajitahidi kuhakikisha tatizo la ukosefu wa soko unapungua au kuisha kabisa.



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula (NFRA), Vumilia Zikankuba (kushoto), akizungumza jambo na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Japhet Justine, baada ya kumaliza kikao kilicholenga kuimarisha mnyororo wa thamani wa mahindi ili kuleta tija na kuwawezesha wakulima wadogo wa zao hilo nchini kwa kuwapatia soko la uhakika. **MPIGAPICHA WETU**

# Waumini watahadharishwa kutoa sadaka noti bandia

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAUMINI wa Kanisa la Advestista Wasabato Shinyanga Mjini, wametakiwa wawe wanazikagua fedha zao ambazo huzitoa sadaka ili kuepuka kumtolea Mungu fedha haramu za noti bandia.

Wito huo ulitolewa na mweka hazina wa kanisa hilo, Amosi Magige, wakati wa matangazo ya kanisa, kuwa wiki iliyopita alipokuwa akipeleka fedha za sadaka benki, alikumbana na changamoto ya kuwapo na noti bandia ya Shilingi 10,000. Alisema wakati akiweka fedha hizo benki, ghafla aliambiwa kuwa katika fedha zake hizo kuna pesa bandia noti ya Shilingi 10,000 kitendo ambacho kilimtia wasiwasi kuwa huenda labda ataitiwa polisi na kutiwa nguvuni.

"Napenda kutoa tahadhari kwenu waumini wa kanisa hili, pale mnapokuwa mnaleta pesa za sadaka jaribuni kuwa mnazichunguza kwanza kama siyo noti bandia, ili kutuepusha kuingia matatizoni na kama pesa hizi zisingekuwa ni za kanisa sijui ingekuwaje," alisema Magige.

"Baada ya kuambiwa katika fedha za sadaka kuna noti bandia kijasho kilianza kunitoka nikajua basi nimekwisha, lakini mfanyakazi huyo wa benki akaishia kusema tu na huko napo zipo hizi, basi ndio ikawa pona yangu na kuamua kutoa pesa nyingine ili kujazilizia, ambazo zilikuwa za michango mingine," aliongeza. Aidha, alisema kwa muumini ambaye hazifahamu noti bandia anaweza kumuona baadaye baada ya ibada kuisha.

Waumini waliitikia wito huo, huku wengine wakidai kuwa hawajui noti bandia, na kueleza kuwa siyo rahisi mtu kwenda kumtolea Mungu sadaka fedha bandia kwa makusudi bali inahitajika elimu ya kuzitambua.

# Wahitimu wanawake shahada ya uzamivu OUT watoa neno

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE nchini wameshauriwa kutumia fursa mbalimbali zinazowazunguka kujiongezea elimu na maarifa ili kujiweka katika nafasi bora ya kukuza vipato vyao na kupunguza utegemezi.

Mmoja wa wahitimu katika Shahada ya Uzamivu (PhD) kwenye Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Dk. Naomi Makota, alitoa wito huo baada ya kutunukiwa shahada hiyo mjini Kibaha mkoani Pwani mwishoni mwa wiki na kuwataka wanawake kuchangamkia fursa hizo ili kujiletea maendeleo.

Dk. Naomi ambaye katika tafiti yake aliangalia 'Athari kwenye Miradi ya Urasimishaji Maeneo ya Mjini' alisema wanawake wana nafasi kubwa ya kuleta mabadiliko katika jamii endapo watazitambua na kuzitumia fursa zilizopo. Alisema wanawake wana mchango mkubwa katika kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kutumia fursa zilizopo ili kujiletea maendeleo na kupunguza utegemezi katika jamii.

"Wanawake tuna mchango mkubwa katika kufanikisha azma ya serikali ya kujenga Tanzania ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2015, wakati umefika sasa tuondokane na imani potofu ya kuwa mwanamke ni tegemezi, na tuchape kazi ili tuongeze vipato vyetu na kupunguza utegemezi," alisema.

Aliongeza kuwa kufanya urathimishaji mwanamke anakuwa na nafasi sawa na mwanaume ya umiliki wa ardhi na miradi ya maendeleo ambayo itamsaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha biashara ndogondogo, ufugaji au kilimo na kuongeza kipato chake.

"Niwashauri wanawake wenzangu kuchangamkia fursa ambazo zinajitokeza, ili kujiongezea kipato na kuchangia pato la nchi ili kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema

Dk. Makota alisema serikali imetoa nafasi kubwa kwa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi, hivyo ni wajibu wao kuwaunga mkono kwa kuendelea kujitoa katika kufanya shughuli mbalimbali ambazo zitawaletea maendeleo.

Kwa upande wake, Dk. Flora Kiwonde, ambaye amefanya utafiti katika masuala ya Tehama jinsi inavyo saidia ufundishaji wa elimu ya mazingira katika shule za msingi ameshauri wanawake kuwa na moyo wa kuthubutu ili kujiletea maendeleo.

"Tunashindwa kufikia malengo yetu kama wanawake na kubaki kuwa tegemezi kwa sababu tumekuwa waoga katika kuthubutu na kupelekea jamii kutudharau, wakati umefika wanawake tuamke na kuwa mfano katika jamii,"alisema Dk. Flora.

Nakuongeza kuwa inawezekana kwa mwanamke kujiendeleza na elimu ya juu, huku akiendelea na shughuli za kifamilia na kijamii kama kawaida kwa kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambacho kinatoa elimu kwa njia ya masafa 'Distance Learning'.



Baadhi ya wahitimu wa Shahada ya Uzamivu (PhD) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), baada ya kutunukiwa shahada kwenye mahafali ya 35 yaliyofanyika mjini Kibaha mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Dk. Naomi Makota na kushoto ni Dk. Flora Kiwonde. **MPIGAPICHA WETU**

# Waathirika wa viboko kulipwa kifuta jasho

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ametoa wiki mbili kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ishughulikie ombi la wanakijiji cha Chunguruma katika Wilaya ya Mafia mkoani Kibaha, la kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyama wakali na waharibifu aina ya viboko.

Hatua hiyo inakuja baada ya viboko kuharibu mazao, mifugo pamoja kusababisha kifo cha mwenyekiti wa kijiji hicho, Abdulahaman Musa, mwaka jana.

Viboko wanadaiwa kuharibu mazao, mifugo pamoja na kutishia maisha ya wanakijiji hao na kwamba wamekuwa wakiingia katika nyumba zao nyakati za usiku.

Akizungumza na wanakijiji hao baada ya kusikiliza kilio chao, Kanyasu, alisema tatizo hilo ni kubwa wakati wizara ikitafuta suluhisho la kudumu, itamhamishia askari wanyamapori katika eneo hilo ili waweze kutoa msaada.

"Niwahakikishie tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha maisha yenu yanakuwa salama na hata pale itakapotulazimu tutawapunguza baadhi ya boko ambao wataonekana wanasumbua zaidi," alisisitiza Kanyasu.

Aliwaeleza kuwa atatuma wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), kujua idadi ya viboko hao kwa kuwa hakuna anayejua idadi yao.

Naye Nassoro Ali ambaye ni mwanakijiji alisema wanyamapori hao ni kivutio cha utalii, lakini wamekuwa kero kwao kwa kuharibu mazao hali inayowasababishia umaskini.

Naye Diwani wa Chunguruma, Hussein Abdi, amemweleza Kanyasu kuwa serikali ifanye haraka kuwalipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa vile ni kilio chao cha muda mrefu.

# Madiwani waagiza mkurugenzi mapato

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MADIWANI wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kuwa na mikakati endelevu ya kuongeza vyanzo vya mapato vya ndani, ikiwamo kujenga uzio katika magulio na minada ili kuwa na uhakiki wa kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Agizo hilo lilifuatia na taarifa ya makadirio ya mpango wa makusanyo ya mapato ya ndani kuonyesha kushuka kwa kasi kutoka Shilingi bilioni 5.5 ya mwaka 2018/19 mpaka Shilingi bilioni 2 ya mwaka 2019/20 na kutoa angalizo kuwa pengo hilo lisipozibwa linaweza kuathiri shughuli za maendeleo.

Flora Sagasaga, Diwani wa Mwalugulu, alitoa angalizo katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani cha kupitisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2019/20, ambapo alisema ili kuongeza mapato ya halmashauri, lazima kuwapo mshikamano baina ya watendaji, madiwani na wananchi.

Naye Diwani wa Segese, Joseph Mayala, alisema kuwa, wataalamu wanatakiwa kwenda kuangalia maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi na kujenga masoko ambayo yatakuwa ni chanzo cha halmashauri hiyo kuongeza vyanzo vyake vya mapato.

"Tunatakiwa kujenga masoko ama magulio katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu wengi na kujenga uzio kwenye magulio ambayo yamekuwa yakiingizia fedha nyingi halmashauri na kuweka kizuizi njiani ili kukusanya ushuru wa usafirishaji wa mazao yanaingia na kutoka," alisema Mayala.

Kaimu Mweka Hazina, Samwel Silutongwe, alisema katika makadirio ya mwaka 2018/19 pato la ndani limepungua kutokana na mgodi wa Bulyanhuru kusitisha uzalishaji kwa kipindi cha miaka miwili, ambapo mgodi huo uliokuwa ukichangia asilimia 75 ya mapato ya ndani katika halmashauri hiyo.

Aidha, alisema kuwa kutokana kutokuwapo kwa mvua nyingi na wakulima kutoitikia mwitikio wa kulima mazao mbala ya kibiashara kama mpunga, mahindi na pamba halmashauri imepunuza makisio ya makusanyo kutoka Shilingi milioni 244 mwaka 2018/19 hadi Shilingi milioni 133 kwa mwaka 2019/20.

Hata hivyo alisema halmashauri imeanzisha mikakati ya kuongeza mapato ya ndani kwa kujenga kituo cha maegesho ya magari Isaka, kituo cha mabasi Segese, ada ya vibali vya ujenzi, ujenzi wa uzio katika minada na magulio, kuhamasisha wakulima kulima mazao ya kibiashara.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido, Toba Nguvila (aliyevaa shati la mistari), akigawa mizinga 116 ya kufugia nyuki kwa kaya maskini 75 za Kijiji cha Kitendeni, zinazonufaika kupitia mpango wa Tasaf wa kuwainua wananchi wenye hali ngumu kiuchumi. **PICHA: ZANURA MOLLEL**

# Tasaf yatoa mizinga 116 kwa kaya maskini

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), wilayani Longido, umekabidhi mizinga 116 yenye thamani ya Sh. milioni 26 kwa kaya 75 maskini katika Kijiji cha Kitendeni, Tarafa ya Enduimet, kwa ajili ya ufugaji wa nyuki.

Akikabidhi mizinga hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido, Toba Nguvila, alisema kipaumbele cha kwanza kwa serikali ni kuwainua wananchi wenye hali ngumu ya kimaisha.

Alisema serikali kupitia Tasaf inashughulika na watu hao wanaotoka kwenye kaya duni.

"Pongezi kwa Tasaf Longido kwa kuwajali watu hawa, mnatekeleza agizo la serikali ipasavyo," alisema.

Alisema awali hali za wanufaika hawa kabla hawajaingia kwenye mradi ilikuwa mbaya, lakini kupitia ruzuku hizo wajikwamue kiuchumi kabla ya mpango huo kufikia mwisho.

"Wanufaika ni wengi mno naomba kubalini kubadilisha maisha yenu kupitia ruzuku hizi mnazopewa, msiende kunywea pombe wala kuongeza mke," alisema.

Alisema wataelekezwa namna ya kuitumia mizinga hiyo ili kuzalisha asali bora ambayo itawaongezea kipato kwa kuiuza katika masoko makubwa.

Hata hivyo, alimtaka mtaalamu wa nyuki kutoka halmashauri, kuwatembelea mara kwa mara wanufaika wa mizinga hiyo na kuwapa elimu.

Alisema endapo mizinga hiyo itashindwa kuzalisha kama inavyotarajiwa, atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Alimtaka Ofisa Ushirika wa Halmashauri kushirikiana na vikundi hivyo kuwafundisha na kuwaelimisha namna ya kuibua fursa za kiuchumi waweze kuinuka na kupiga hatua katika kipato chao.

Aidha, alimtaka Ofisa Biashara kuhakikisha anatafuta soko la kudumu ndani na nje ya nchi, ili watakapofikia kurina asali, wasibabaike kupata soko.

Kwa upande wake, Mratibu wa Tasaf Wilaya ya Longido, Saruni Lobulu, alisema mizinga hiyo imekabidhiwa kwa vikundi vitano kati ya saba vilivyopo katika kijiji hicho ambavyo vipo kwenye mpango wa Tasaf.

Akifafanua alisema mizinga hiyo ina thamani ya Sh. milioni 26 na itagawanywa kwa watu 75 na kila kikundi kitapewa mizinga 15.

"Watu hawa wamegawanywa kwa vikundi vya watu 15, na tutatoa mizinga 15 kwa kila kikundi," alisema.

Alieleza watatoa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa walengwa hao na wanatarajia kuanza ujenzi wa barabara waliyoibua walengwa ya kilomita 4.5 pindi fedha zitakapopatikana.

"Tunatengeneza miradi mingi na hii wanaibua walengwa wenyewe," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Juma Mhina, aliishukuru Tasaf kwa kuendelea kuchangia miradi ya maendeleo ikiwamo ufugaji wa nyuki na kwamba kupitia ufugaji nyuki unaotekelezwa na wakazi wa Kijiji cha Kitendeni, anaamini walengwa hao watajikwamua kiuchumi.

"Lakini kubwa zaidi niseme tu utafiti umefanyika na kugundulika misitu ya Longido inazalisha asali nzuri duniani kote na asali hii haina sumu kwa kuwa huzalishwa na maua ya aina moja.

"Longido kuna miti aina ya acacia (oltepes), miti hii ni mizuri katika uzalishaji wa asali dunia nzima na inapatikana Longido," alisema.

Aliwataka wakazi wa Longido kujitokeza na kuwekeza katika miradi ya ufugaji nyuki, kwa kuwa maeneo mengi wilayani hapo yanafaa kuwekeza katika miradi ya nyuki, misitu ipo ya kutosha.

Mmoja wa wanufaika wa mizinga hiyo, Anna Elisha, alisema Tasaf imemsaidia kuwasomesha watoto wake pamoja na kuhakikisha wanapata milo mitatu kwa siku na kukata bima ya afya.

# Waajiri watakiwa kuripoti matukio ya ajali kazini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha), umewataka waajiri kutoa taarifa za matukio ya ajali mahali pa kazi, ili kutafuta namna ya kupunguza ajali hizo na kuongeza tija.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alisema hayo jijini hapa juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mkutano wao uliowashirikisha waajiri zaidi 70 mkoani hapa.

Alisema, katika mwaka wa fedha 2017/18, kulikuwa na matukio 920 ya ajali mahali pa kazi ambayo yaliripotiwa.

Alisema kuripoti matukio ya ajali kazini kunasaidia waajiri kutafuta namna ya kudhibiti ajali hizo kwa kuweka mazingira au miundombinu rafiki sehemu za kazi. Alisema wanawahamasisha waajiri kusimamia maeneo yao ya kazi kwa hiari bila kuwasubiri wataalamu kutoka Osha kwa lengo la kupunguza ajali, magonjwa na vifo sehemu za kazi.

Kwa upande wake, Meneja wa Usalama, Afya na Mazingira wa A to Z Textile Mills Ltd., Mhandisi Rwehumbiza Rwehumbiza, alisema mafunzo ya usalama mahala pa kazi yanasaidia kupunguza ajali.

Alisema ni muhimu kwa waajiri kuhakikisha mahali pa kazi panakuwa salama kwa wafanyakazi.

"Tunahakikisha wafanyakazi wageni kabla ya kuingia kiwandani tunawapa mafunzo na kuwaelekeza namna bora ya kufanya kazi kwa kuzingatia usalama wao.

"Mafunzo haya yanasaidia kuongeza uzalishaji na kupunguza ajali," alisema.

Kwa upande wake, Meneja Mazingira na Usalama kazini kutoka Tanzania Breweries Ltd (TBL), mkoani hapa, alisema mwajiri ana wajibu wa kuweka miundombinu itakayozuia vyanzo hatarishi kwa usalama wa wafanyakazi.

# TaESA watoa angalizo kwa wahitimu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAKALA wa Huduma za Ajira nchini, (TaESA), umetoa angalizo kwa wahitimu wa vyuo kuepuka matapeli wanaoweza kuwaibia fedha kwa ahadi ya kuwatafutia ajira na badala yake imewataka kutumia huduma zinazotolewa na wakala huo.

Ofisa Kazi Mwandamizi kutoka TaES iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Peter Ugata, alisema hayo alipokuwa akiwajengea uwezo wanafunzi wa Chuo cha Ufundi Arusha, (ATC).

Alisema jukumu kubwa walilokabidhiwa na serikali ni kuhakikisha wanawaunganisha watafuta kazi na waajiri wenye fursa za kazi.

Alisema watafuta kazi husajiliwa TaESA wakiwa na sifa mbalimbali kwa viwango vya elimu zao na kushindanishwa katika fursa zilizopo ili kujijengea uwezo.

"Mtafuta kazi anayetafuta kupitia kwetu huandaliwa, hatupeleki mtafuta kazi ambaye hajaandaliwa kwa mwajiri," alisema.

Katika mafunzo hayo Ugata aliwashauri waajiri kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuangalia uzalishaji na shughuli walizozianzisha.

Alisema serikali imeona suala la kutafuta wafanyakazi na kuandaa wenye sifa na ndiyo maana imetenga bajeti ikiwamo kuanzisha TaESA inayoandaa wafanyakazi wenye sifa kwa ajili ya kujaza soko la ndani na nje.

"Tupo ATC kuwapa mafunzo vijana ya kuwandaa katika soko la ajira wajue linataka nini, bahati nzuri kuna vijana wamemaliza masomo, hawa tumeshawasajili, na kwa bahati nzuri waajiri wamejitokeza kuwahitaji wakafanye kazi," alisema.

Alisema TaESA humjengea kijana sifa za ziada aweze kukidhi mahitaji ya mwajiri ndani na nje katika soko la ajira, kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri. Aidha, alisema serikali inatumia fedha nyingi kuhakikisha Watanzania wananufaika na huduma zinazotolewa TaESA.

"Tunawaomba watumie huduma hizi kwa kujisajiri na wakala, lakini pia wataalamu wa wakala wamejitolea kukutana na waajiri nchi nzima," alisema.

Kwa upande wake, mwanafunzi anayesomea Shahada ya Uhandisi na Umwagiliaji, Maxmilian Ndege, alipongeza hatua ya kuwatengenezea mtandao kama ilivyo kwa nchi za nje ambazo huzunguka vyuoni kuwasaidia wanafunzi.

Naye mkufunzi wa ATC katika idara ya mafunzo viwandani, Dk. Jaffar Mwanza, alisema jukumu lao ni kufundisha vijana wenye ujuzi na si watafutaji.

"Ukiwa na ujuzi lazima utapata ajira sahihi, kazi za ujuzi hazipatikani bila kuwawezesha vijana wajue taratibu na sheria za kazi zinasemaje. "Juhudi tunazofanya kwa ushirikiano na TaESA ni kuhakikisha mafunzo waliyopata vijana hayapotei bure baada ya kupata mafunzo yao, hivyo ni muhimu vijana wakaacha kutumia muda mwingi kwenye mitandao na mambo yasiyo na msingi kwao," alisema.

Alisema kanzidata ya TaESA inawasaidia wao kujua ni fani gani au taaluma gani inahitajika mfano kwa sasa wanahitajika mafundi katika kazi za mabomba ya gesi na uchimbaji wa mafuta.

Aidha, Ofisa Kazi TaESA Kanda ya Dar es Salaam, Emma Mangesho, alisema kuwapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya waajiri wakidai watafuta kazi baadhi hawajui namna ya kuandika barua za kuomba kazi, kujibu maswali ya usaili na kuandika wasifu binafsi.

"TaESA imechukua jukumu hilo la kuwajengea uwezo katika maeneo hayo ili kuhakikisha vijana wanaweza kushindania fursa za kazi," alisema.





# Watendaji wakwamisha PETS kiutekelezaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI wadau wa maendeleo wakipambana kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika miradi mbalimbali inayotekelezwa Wilaya ya Moshi, changamoto kuhusu baadhi ya watendaji wa serikali kudai posho kwanza, ndipo watoe taarifa, inatajwa kuwa kikwazo kikubwa kwa Kamati za Ufuatiliaji Rasilimali za Umma (PETS).

Taarifa kuhusu hali hiyo iliwekwa wazi jana na wajumbe wa kamati hizo wanaofanya kazi na Asasi ya Indigo Women Links (T) na Mtandao wa mashirika yanayojihusisha na masuala ya maji na usafi wa mazingira (Tawasa Net).

Akizungumza katika kikao cha siku tatu kilichojumuisha kamati zote zilizopo katika Wilaya ya Moshi, mmoja wa wajumbe wa kamati hizo, Janeth Kessy, alisema changamoto kubwa inayopaswa kufanyiwa kazi ni ya baadhi ya viongozi wa ngazi za vijiji na kata zinazotekeleza miradi, kudai kwanza posho ndipo watoe taarifa, jambo ambalo amedai linaathiri kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Achalia mbali kudai posho, kuna changamoto nyingine tunayokutana nayo ya kukosekana kwa taarifa za miradi husika, mfano ni mradi wa maji Kirima, kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya viongozi na wananchi na ugumu wa kufika kwenye miradi kama ya vyanzo vya maji," alisema Janeth.

Aidha, Christopher Maleko, kwa upande wake, alidai kuwa changamoto ya kunyimwa taarifa sahihi na viongozi wa miradi husika, kwa kigezo cha kutokujua hatima yao kutoka kwa wadau wa ufuatiliaji wa fedha za umma pamoja na viongozi kutokuweka wazi taarifa za matumizi ya fedha za mradi ni mambo yanayohitaji kushughulikiwa na serikali ili kuwafanya wananchi kufahamu gharama za miradi na matumizi ya fedha za umma.

Ofisa Uhusiano wa Asasi hiyo ya Indigo, Charles Lyimo, alisema serikali imekuwa ikitenga fedha kwenye sekta mbalimbali kwa ajili ya shughuli za maendeleo, lakini zimekuwa zikiibuka changamoto kadhaa ambazo wakati mwingine zinakwamisha kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Sasa hivi wananchi kule vijijini wamekuwa na uwezo wa kujua kumbe ni haki yao kuhoji matumizi ya fedha zilivyotumika, pia ni haki yao kufuatilia na kupewa taarifa ya mradi wowote ambao umetekelezwa au ambao unatarajiwa kutekelezwa, tofauti na zamani vile vipaumbele vilikuwa vinawekwa na kutekelezwa tu na viongozi, lakini sasa hivi vipaumbele vinaanzia chini kwa wananchi na wanafuatilia wao wenyewe," alisema Lyimo.

Kutokana na changamoto hizo, Mkurugenzi wa Indigo Women Links (T), Dk. Rosemary Daniel, alisema wamechukua hatua kwa kuanza kuwapa wajumbe hao ujuzi wa kutumia kadi maalumu ya kutathmini miradi ya wananchi kwa ajili ya kupima kiwango cha kuridhika katika ujumla wa miradi inayotekelezwa.

Alieleza kuwa kadi hiyo inaonyesha uchambuzi wa kiwango cha uridhikaji wa wananchi ngazi ya kijiji na kata na kwamba baada ya kupewa mafunzo, watatumia kadi hizo kupima miradi ya ujenzi wa vyoo, ujenzi wa mifereji, majisafi na usafi wa mazingira, uchimbaji wa visima, uwekaji wa mfumo wa utunzaji taka, ujenzi wa mifumo ya mabomba ya maji na uwekaji wa mifumo ya majitaka.



Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, akiweka jiwe la msingi katika jengo la nyumba ya Mchungaji wa Usharika wa Kimashuku, Hai ambalo litagharimu Sh. milioni 70 hadi kukamilika. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Zahanati yaelemewa wagonjwa wa nje

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ZAHANATI ya Anne Kiulu iliyoko Moshi Vijijini, yenye wataalamu wawili pekee ambao ni maofisa wauguzi, inabeba mzigo mzito wa kuhudumia wagonjwa wa nje zaidi ya 230 kutoka vijiji vitano vya kata za jirani.

Wagonjwa hao ni tofauti na wanaotakiwa kuwahudumia ambao ni wananchi wa Kijiji cha Kimochi.

Ofisa muuguzi wa zahanati hiyo, Heillen Ndossi, alieleza kuwa hivi sasa wanapokea wagonjwa wa nje kwa siku 18 hadi 20 na kwa mwezi ni zaidi ya 230.

Aliyasema hayo juzi, baada ya Mbunge wa Moshi Vijijini, Anthony Komu, kutembelea zahanati hiyo kujua changamoto zinazoikabili katika utoaji huduma.

"Ukiacha huduma ambayo tunatakiwa kutoa kwa wananchi wa Kijiji cha Kimochi, kuna vijiji ambavyo vinapata huduma kwenye zahanati hii na tunawapokea kutoka vijiji vya Mdawi, Kisaseni, Mowo, Shia na Kidia," alisema.

Zahanati ya Anne Kiulu ilijengwa na mwanasheria mbobezi wa masuala ya haki za binadamu na mazingira wa Norway, Marius Reikeras, kama shukurani kwa wakazi wa Kijiji cha Kimochi, baada ya mfadhili huyo kumuoa mkazi wa kijiji hicho.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, Zahanati Anne Kiulu pamoja na kuwa na wataalamu wawili pekee, lakini pia haina mhudumu wa afya, licha ya kutoa huduma ya wagonjwa wa nje, wajawazito, watoto, chanjo, kupima maambukizi ya virusi vya Ukimwi, malaria kwa kipimo cha haraka cha MRDT na huduma ya ushauri nasaha.

Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kila kijiji kiwe na zahanati na kata kuwa na kituo cha afya chenye watumishi wa kutosha.

Mbunge Komu akizungumza muda mfupi baada ya kupewa taarifa hiyo, alisema amepokea changamoto hizo na atakutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Tatu Kikwete, kumweleza tatizo hilo na kutafuta ufumbuzi wake.

## Mwanamitindo Mmarekani ataka ubalozi wa utalii Tanzania

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HATIMAYE mwanamitindo na mwigizaji maarufu wa Marekani aliyewahi kung'ara katika taji la Miss Universe, Marisela De Montecristo, amemaliza ziara yake katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, huku akiahidi kwa serikali ya Tanzania kutaka kuwa balozi wake wa utalii.

Jana, Marisela alianza ziara yake ya pili katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Bonde la Ufa la Ngorongoro (Ngorongoro Creator).

Akizungumza na Nipashe muda mfupi baada ya kuondoka Tarangire, mwanamitindo huyo alisema: "Kuna utajiri mkubwa wa maliasili nchini Tanzania, mbuga za wanyama zinatosha dunia kuijua Tanzania, mnayo kazi kubwa sana ya kutangaza utalii wenu na mimi nataka kubeba jukumu hili katika kazi zangu nazofanya kwenye mataifa mbalimbali."

Marisela ambaye ni raia wa El Salvador, aliyehamia Los Angels, Marekani, kabla ya ujio wake nchini, alinukuliwa na gazeti hili akisema, dunia kwa sasa imebadilika na kila fursa inapojitokeza ni lazima kuitumia kukuza uchumi na hasa utalii wa mataifa mengine katika nchi zinazoendelea kama Tanzania.

Mwanamitindo huyo ameeleza mpango wake wa kuitangaza Tanzania, kuwa safari hii amekuja kujifunza baadhi ya vivutio anavyotaka kuvitumia kimataifa.

Baada ya kumaliza ziara yake Ngorongoro, atarejea katika mji wa Moshi kutembelea moja ya kituo cha watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuona namna ya kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Mwaka jana, Merisela alishiriki pia mashindano ya ulimbwende nchini El Salvador na kufanikiwa kutwaa taji hilo.

Pia aliwahi kushiriki mashindano ya Best National Costumes na kufanikiwa kushika nafasi ya pili, huku nafasi ya kwanza ikichukuliwa na Brazil na ya tatu Panama. Merisela anamiliki taasisi binafsi ya kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu nchini Marekani.



KILICHOIMALIZA SIMBA CONGO UK.15

## PAMBANA...



Viungo wa Arsenal, Granit Xhaka na Mohamed Elneny, wakipambana kumdhibiti mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa kwenye Uwanja wa Emirates juzi usiku na wenyeji kushinda 2-0. **HABARI UK. 28**

### ISIKUPITE

KIPA wa Crystal Palace, Julian Speroni, mwenye umri wa miaka 39 na siku 246, ndiye mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi aliyecheza Ligi Kuu England msimu huu hadi sasa. Aidha, ndiye mkongwe zaidi aliyecheza mechi ya kimashindano tangu Shay Given (miaka 40 na siku 151) alipocheza Septemba 2016.

## MICHEZO

# ATAKAPOIBUKIA OZIL BAADA YA ARSENAL



**LONDON,** England

KIUNGO Mesut Ozil, hajaichezea Arsenal tangu siku ya Kufungua Vifurushi vya Zawadi ('Boxing Day') ukiacha mechi za mwishoni mwa wiki hii. Kumekuwa na ripoti kwamba Ozil alikuwa akisumbuliwa na majeraha, lakini ni wazi kwamba kocha, Unai Emery, haridhishwi na mchango wa mchezaji huyo anayelipwa paundi 350,000 kwa wiki.

Emery amejitokeza na kusema kwamba, bodi ya Arsenal inajiandaa kumtoa kwa mkopo wakati huu wa dirisha dogo la usajili la Januari, na Gazeti la Sun limedai kwamba Emery anataka fedha kwa ajili ya kununua wachezaji wengine.

Akiwa na mabao mata tu na pasi ya mwisho moja katika mechi 13 alizocheza msimu huu, Arsenal wanaweza wasipate fedha za kutosha kutokana na kiwango cha mchezaji huyo, lakini ukweli unabaki kwamba Ozil ana kipaji cha juu kwa timu yoyote kuichezea. Kama Arsenal wataweka wazi kutaka kumuuza Mjerumani huyo, hapa tunakuchambulia sehemu 4 ambazo zinamfaa mchezaji huyo kwenda...

**Kwingineko England**

Bodi ya Arsenal kwa uhakika hawataki kumuuza mchezaji kwa wapinzani wao. Majina ya wachezaji yote yaliyosajiliwa na wapinzani wao kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, ilionekana kuwakasirisha mashabiki wa Arsenal, kwa wachezaji kama Nasri, Sagna, Clichy, Van Persie, Oxlade-Chamberlain na Sanchez.

Kama Arsenal wanataka kupata fedha kwa mauzo ya Ozil na abakie kwenye klabu za nchini humo, inaweza kuleta gumzo tena kwa mashabiki. Hata hivyo, ni vigumu kwa yeye kuweza kusajiliwa na klabu za Ligi Kuu ya England.

Inawezekana kwamba Pep Guardiola au Jurgen Klopp wangeweza kumhitaji, lakini ni vigumu kwa Ozil kuwa na nafasi ya kucheza kwa vikosi vya sasa vya Manchester City au Liverpool. Kwa David Silva na Kevin de Bruyne, Manchester City wana mawinga wenye vipaji vya hali ya juu zaidi na kwa namna yoyote wasingeweza kuhitaji mwingine.

Safu ya kiungo ya Liverpool iko fiti zaidi, lakini pengine Klopp angeweza kumtafutia nafasi ya kucheza Mjerumani mwenzake huyo. Kwa upande wa Tottenham ni vigumu kwa kuwa tayari wana viungo wazuri kama Eriksen na Alli na mwenyekiti wao, Daniel Levy asingekuwa tayari kumudu mshahara wa Ozil ambao ni mara tatu zaidi ya nyota wao Harry Kane.

Timu pekee ambazo Ozil anaweza kufiti ni Manchester United na Chelsea. Ozil anaweza kufiti kwa timu hizo mbili, kwa sababu zote zinamhitaji mchezaji aina yake ambaye anaweza kusaidia zaidi katika kusukumiza mashambulizi mbele. Hata hivyo, mfumo pekee utakaomwezesha Ozil kucheza ni ule wa Maurizio Sarri wa 4-3-3 pale Chelsea. Manchester United wana nafasi kwa mchezaji huyo namba 10, lakini kwa sasa tatizo lao kubwa zaidi ni safu ya ulinzi.

**Paris Saint-Germain**

Kwa staili yao ya "lipa kwanza uliza maswali baada ", PSG inaweza kuwa sehemu nzuri zaidi ya kutua kwa Ozil. Ozil mwenyewe atakuwa na nafasi nzuri ya kuwalisha mipira nyota kama Neymar na Kylian Mbappe. Hata hivyo, kuna sababu mbili zinasimama kuhusu uhamisho wake.

Kwanza, PSG wako pointi 13 zaidi kileleni mwa ligi, wakifunga mabao 21 mengi zaidi kuliko timu yoyote, huku kukiwa na wachezaji kama Marco Veratti, Angel di Maria na Julian Draxler wakiing'arisha safu ya kiungo. Haionyeshi kama kuna uhitaji wa kiungo kwenye kikosi chao, kwa kuwa mabingwa hao wa Ufaransa wana uwezo mzuri wa kutengeneza nafasi za kufunga.

PSG tayari wanaonekana kukaribia kukamilisha dili na kumsajili kiungo wa Ajax, Frenkie de Jong na ni wazi kwamba kutoa fedha kwa ajili ya usajili wa Ozil linaweza kuwa jambo lisilowezekana.

**Bayern Munich**

Ukisikia kwa mara ya kwanza inaonekana haiwezekani. Bayern Munich ni maarufu kwa kutotumia fedha nyingi kwenye usajili, kwa sababu hadi sasa mchezaji wao aliyenunuliwa kwa fedha nyingi zaidi ni Corentin Tollisso, ambaye aliwagharimu paundi milioni 38. Kiuhalisia klabu za Monaco na Everton zote zimetumia fedha nyingi kwa usajili mmoja kuliko miamba hao wa Ujerumani. Kwa nyongeza, Ozil ana suala kubwa ambalo bado limesimama baada ya kutangaza kustaafu kuichezea Timu ya Taifa ya Ujerumani kwa madai ya kubaguliwa kwa sababu yeye ni mtu mwenye asili ya Uturuki. Rais wa Bayern Munich, Uli Hoeness, hajaonyesha bado kuwa na mpango wa kumsajili Ozil.

Hata hivyo, Bayern ambayo imeshinda taji la Ligi Kuu ya Ujerumani kwa miaka mitano iliyopita, inahitaji kujengwa upya. Kwa sasa imepitwa pointi sita na vinara Dortmund, kocha wake, Niko Kovac yupo kwenye presha kubwa kutokana na matokeo hayo. wachezaji wa daraja la juu duniani kama Ozil huwa hawatokei mara kwa mara, na Kovac anaweza kumchukua mchezaji huyo mwenye kipaji cha hali ya juu, ambaye anaweza kuwachezesha vizuri wachezaji kama Thomas Muller.

**China**

Hatimaye amepatikana tembo ambaye anaweza kuwa suluhisho la usajili unaosuasua. Ligi ya China hivi sasa inaonekana kama kivutio cha wachezaji ambao wanaonekana kukosa nafasi ya kucheza barani Ulaya. Kifedha uhamisho wa Ozil utawanufaisha wote pamoja na klabu.

Hata hivyo, swali litakuja kama Ozil atakuwa tayari kucheza soka kwenye ligi inayoanza kukua au la. Katika umri wake wa miaka 28, Ozil bado anaweza kutoa mchango mkubwa kwa timu kubwa zilizopo daraja la juu. Kwa mfano hajawahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na ameshinda taji la Ligi Kuu akiwa na Real Madrid. Hivyo kuhamia China kutamfanya kuzidi kupotea kwenye daraja la juu.

**JE, WAJUA?**

OLE Gunnar Solskjaer ni kocha wa tatu katika historia ya Ligi Kuu England kuweza kushinda mechi zake sita za kwanza akiiongoza klabu, baada ya Carlo Ancelotti wakati akiwa na Chelsea na Pep Guardiola akiwa na Manchester City.



## NJE YA UWANJA



## SALAH AWAFUATA SHEARER, HENRY MWENDO KASI EPL

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Mohamed Salah, amefunga bao lake la 50 kwenye Ligi Kuu England na kuiwezesha timu yake kushinda 4-3 dhidi ya Crystal Palace Jumamosi.

Kwa mantiki hiyo, sasa Salah anajiunga na wachezaji wengine wanne ambao wamefikisha idadi hiyo mapema zaidi katika historia ya ligi hiyo.

Kikosi cha Jurgen Klopp kilikuwa nyuma kwa bao moja wakati wa mapumziko kwenye mechi hiyo ambayo ilikuwa ni ya 72 kwa Salah kucheza Ligi Kuu England, ambapo dakika ya 46 tu alitupia bao lake la 49 na kufanya ubao wa matangazo uwanjani hapo kusomeka 1-1.

Na kisha nyota huyo wa kimataifa wa Misri aliyatumia makosa ya kipa wa Palace, Julian Speroni, kuiweka Liverpool mbele kwa mabao 3-2 ikiwa ni dakika 15 kabla ya mechi kumalizika. Roberto Firmino na Sadio Mane pia walitupia moja moja.

Andy Cole ndiye kinara wa kufikisha mapema nusu karne hiyo ya mabao kwenye EPL, ikiwa ni baada ya kushuka dimbani mara 65 mechi moja zaidi ya Alan Shearer na zikiwa tatu kwa mchezaji mwingine wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy.

Salah anajiunga na wachezaji wengine wa Liverpool waliofikisha nusu karne hiyo ya mabao mapema zaidi, akiwamo Fernando Torres na Luis Suarez.

Kumi bora ya kufikisha mabao 50 mapema zaidi EPL na idadi ya mechi zao kwenye mabano ni; 10. Luis Suarez (86), 9. Diego Costa (85), 7. Kevin Phillips (83), 7. Thierry Henry (83), 6. Sergio Aguero (81), 4. Fernando Torres (72), 4. Mohamed Salah (72), 3. Ruud van Nistelrooy (68), 2. Alan Shearer (66) na kinara Andrew Cole (65).




Baadhi ya wachezaji wa timu ya soka ya Simba

# KILICHOIMALIZA SIMBA CONGO

**Na Adam Fungamwango**

KILIKUWA ni kipigo kizito cha mabao 5-0 ilichokipata Simba dhidi ya AS Vita mjini Kinshasa nchini Congo DR.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Jumamosi walikutana na kipigo hicho wiki moja tu baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 nyumbani dhidi ya JS Saoura ya Algeria.

Huo ni mchezo wa pili wa Kundi D wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba iliondoka nchini ikiwa na matumaini kibao ya kupata ushindi, lakini ilikuwa inajua kuwa inakwenda kupambana na wanafainali wa Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliomalizika.

Ni kitu gani kilichosababisha Simba kupoteza mechi hiyo? Lakini pia ni kwa nini imepoteza kwa idadi kubwa ya mabao?

### Woga wa mechi

Ni kama vile wachezaji wa Simba waliingiwa na woga kutokana na sifa na rekodi ya AS Vita.

Rekodi ya kufika fainali ya CAF, pamoja na kutopoteza mechi nyumbani kwao tangu mwaka 2017, iliwafanya wachezaji wa Simba kuanza mechi kwa taratibu kuonekana kuwahofia wapinzani wao kinyume na ilivyozoeleka.

Hiyo ilisababisha kufungwa bao la kwanza na lilipofungwa la pili, tayari wachezaji wa Simba walionekana kuondoka mchezoni na kuchanganyikiwa kiasi cha kuanza kufanya makosa madogo madogo yaliyowagharimu.

### Wengi hawakuwa kwenye ubora

Wachezaji wengi wa Simba kwenye mechi hiyo hawakuwa kwenye ubora uliozoeleka. Ndiyo maana haikushangaza kuona Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, akimtoa Clautous Chama na kumwingiza Haruna Niyonzima.

Chama kwa sasa ni kama moyo wa timu ndani ya uwanja. Yeye ndiye anayeongoza timu icheze vipi, iende kushoto au kulia. Kitendo cha kutolewa, kilionyesha kuwa hakuwa kwenye ubora wake na maji yalizidi unga.

### Manula, Gyan, Niyonzima waling'ara

Cha kushangaza kwenye mechi dhidi ya AS Vita, mchezaji ambaye anapigiwa kelele sana na mashabiki wa Simba kuwa huwa hachezi vizuri, Nicolaus Gyan ndiye aliyekuwa kwenye ubora wa hali ya juu kwenye mechi hiyo.

Ndiye mara nyingi alionekana akifanya vitu kwa usahihi, tofauti na wengine ambao mashambulizi yao walikuwa yakizuiwa kirahisi na mabeki wa upinzani.

Hata kwenye kukaba alijitahidi zaidi kuliko hata Mohamed Hussein Tshabalala.

Kipa Aishi Manula ambaye naye huwa analaumiwa sana na mashabiki wa Simba kwa kufungwa baadhi ya mabao ya kizembe, aliiokoa timu yake isibebeshwe kiroba cha mabao.

Aliokoa hatari nyingi ambazo mastraika wa AS Vita walikuwa wakibaki wao na yeye, huku mashabiki wao wakiwa wameinuka kushangilia wakitegemea kabisa kuwa lingekuwa bao. Aliokoa kiasi cha hatari tano hivi ambazo zilitakiwa kuwa mabao.

Kiungo Haruna Niyonzima alipoingia aliituliza timu na kuanza kucheza soka lao lililozoeleka, lakini tatizo lilikuwa ni muda. Tayari Simba ilikuwa imeshapoteza mechi kwa idadi kubwa ya mabao, hivyo wachezaji walionekana wameshakata tamaa.

Huenda kama angeingia mapema wakati AS Vita inaongoza kwa mabao mawili, mambo yangeweza kuwa tofauti. Labda mabao matano yasingefika.

### Mabeki Simba bado majanga

Kama alivyowahi kunukuliwa kocha wa Nkana FC, Beston Chambeshi kuwa kitakachowakwamisha Simba kwenye hatua ya makundi ni mabeki.

Akasema haoni kama ina walinzi imara watakaoweza kupambana na mastraika na mawinga wa timu zingine, hasa Waarabu. Kabla hata haijacheza na timu ngumu kutoka Uarabuni hususan Al Ahly, majibu yameshaanza kupatikana.

Mabeki wa Simba wa kati na pembeni wote ni rahisi mno kupitika. Si wabishi, na wanaruhusu sana mastraika kuingia kwenye eneo la hatari kirahisi, pia mawinga kupiga krosi watakavyo.

Simba Jumamosi ilikutana na timu ambayo inaweza kutumia udhaifu huo kupata mabao.

Mastraika wa AS Vita alikuwa akiipita beki wa Simba wapendavyo na mawinga walikuwa wakipiga krosi kila wanapojisikia, kitu kilichokuwa kikiliweka goli la timu hiyo kuwa mashakani muda wote wanapokwenda kushambulia.

Simba waliwazuia mara chache sana kuliko wao kupita na kwenda kumsalimia Manula.

Mabeki wa kati Simba walikuwa hawaruki kuzuia mipira ya krosi ilipita na kuwakuta wapinzani wao. Kati ya mabao matano yaliyofungwa, mawili ya kona yalikuwa ni uzembe na mabeki kutoruka kuokoa.

Wafungaji walikuwa wakiruka peke yao na kukwamisha mpira wavuni wakiwa kwenye rundo la mabeki wa Simba waliokuwa wamesimama tu wakiutazama mpira ukiwapita juu ya vichwa vyao bila jitihada zozote.

### AS Vita ni bora zaidi

Kiuwezo AS Vita ilionekana ni timu iliyokamilika zaidi kuliko Simba. Kila idara ilikuwa iko imara kuanzia golini, mabeki wa pembeni, wa kati, viungo wakabaji na washambuliaji, hata mawinga, tofauti ya Simba ambao ina baadhi ya wachezaji tu ambao ni bora. Hata waliokuwa wakiingia kipindi cha pili walionekana kuwa na uwezo mkubwa wakati mwingine zaidi kuliko hata aliyetoka.

Extra Time



# Mechi zitakazoamua hatima ya Solskjaer Manchester Utd

**MANCHESTER,** England

KATIKA mchezo dhidi ya Tottenham, Ole Gunnar Solskjaer alionekana kama amepagawa. Aliweza kuwabana wapinzani wake kwenye kipindi cha kwanza kwa mbinu zake, ambazo baadaye zilimwezesha kupata bao lililowapa ushindi.

Hata hivyo, wakati Spurs walipokuwa wanalishambulia zaidi goli lao kipindi cha pili, Solskjaer alionekana kuogopa. Alijaribu kuchanganya vitu, lakini golikipa wake, David De Gea alikuwa msaada mkubwa kwake na kwa United.

Ushindi kwenye dimba la Wembley umewafanya United sasa kuwa kwenye mbio za kuwania kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye ligi.

Huku Solskjaer akiwa amepewa nafasi hiyo ya ukocha kwa muda hadi mwishoni mwa msimu baada ya kufukuzwa kwa Jose Mourinho, sasa anaonekana kuitaka nafasi hiyo moja kwa moja.

Pamoja na yote, hapa tunakuchambulia michezo mitano inayomkabili raia huyo wa Norway ambayo inaweza kumtengenezea majaliwa yake mazuri zaidi ya kupewa kazi hiyo kwa mkataba wa kudumu.

**5. Arsenal (ugenini) - Ligi Kuu: 09/03/2019**

Wakati ambao Manchester United watasafiri kwenda kwenye Uwanja wa Emirates kuikabili Arsenal, msimamo wa Ligi Kuu ya England unaweza kuwa tofauti kwa pande zote mbili. United kwa sasa wamecheza mechi saba bila kufungwa na wamecheza na Liverpool tu kati ya timu kubwa tano kabla ya kuwavaa 'Washika Bunduki' hao.

Kwa upande wa Washika Bunduki, wamepoteza mechi zao tatu kati ya sita kwenye Ligi Kuu, na kabla ya kuwakaribisha United hapo kwenye dimba la Emirates, watakuwa na kibarua dhidi ya Tottenham na Manchester City.

Wakati ikiwa ni vigumu kufikiri kwamba United inaweza kuendelea na kiwango chake hiki hadi Machi, ni upuuzi kudhani kwamba Arsenal haitaweza kuanza kushinda. Katika mchezo huo, unaweza kuwa kwenye utawala wa mabao na hakuna anayeweza kudhani.

Solskjaer atakabiliwa na mchezo mgumu kwa sababu United akili zao wamezielekeza kwenye kuwania nafasi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ili wamalize nafasi nne za juu. Na Arsenal ni miongoni mwa timu zinazowania nafasi hiyo. Kasi ya ushambuliaji ya kikosi hicho cha Emery itahitaji mbinu mpya dhidi ya raia huyo wa Norway.

**4. Chelsea (nyumbani) - Ligi Kuu: 27/04/2019**

Mchezo dhidi ya Chelsea umepangwa mwishoni mwa Aprili, na mbio za kuwania nafasi nne za juu zitakuwa zimekwisha. Hata hivyo, Blues kwa sasa wapo nafasi ya nne, nafasi ambayo Solskjaer lazima aipiganie kwa ajili ya kuendelea kubakia kuwa kocha wa Manchester United mwishoni mwa msimu.

Chelsea kwa sasa wana pointi 47 katika mechi 23 walizocheza na wamefunga mabao 40, huku wakiruhusu mabao 19. United kwa sasa wana pointi 44, pointi tatu nyuma yao na wamefunga mabao 46 na kuruhusu mabao 33. Na kwa kuwa ukweli ni kwamba United imeizidi Chelsea kwa mabao ya kufunga tangu Solskjaer achukue mikoba, ina maana kwamba wamefanya vizuri.

Kikosi cha Maurizio Sarri kilianza Ligi Kuu England kwa kucheza mechi 12 bila kufungwa, ambapo walifunga mabao 27 na walishinda michezo nane. Hata hivyo, Chelsea tayari imepoteza mechi nne. United walipocheza pale Stamford Bridge walitoka sare ya 2-2 chini ya Mourinho, hata hivyo, Solskjaer atakuwa na nafasi nzuri ya kuifanya timu yake icheze kwa kiwango cha juu.

**3. Arsenal (ugenini) - Kombe la FA: 25/01/2019**

Kiufundi michuano ya Kombe la FA ndiyo nafasi ngumu zaidi kwa United ya kupata taji msimu huu. Ingawa United bado wapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA ndio nafasi nzuri zaidi kwa Solskjaer kuwa na nafasi ya kumaliza msimu huu akiwa na taji litakalomwezesha bodi ya United kuwa na nafasi nzuri ya kumpa mkataba wa kudumu katika kikosi hicho.

United imeanza Kombe la FA chini ya uongozi wa raia huyo wa Norway msimu huu, kitu ambacho kitampa Solskjaer hamasa ya kuweza kupata mafanikio. United imeshinda mchezo wake wa raundi ya tatu dhidi ya Reading mwanzoni mwa mwaka huu na wamepangwa kucheza na Arsenal kwenye raundi ya nne, ambapo mchezo huo utapigwa mwishoni mwa Januari hii.

Washika Bundiki hao wameshinda mashindano hayo kwa rekodi yao mara 13, moja zaidi ya United, kitu kinachofanya mchezo huo kuwa wa kuvutia zaidi. Msimu uliopita, United walikuwa na nafasi nzuri kwenye mashindano hayo, walifungwa na Chelsea kwenye fainali Mei. Wakati huu, Solskjaer atakuwa akicheza michuano hiyo kwa umakini mkubwa, hii itakuwa ni moja ya nyakati za kuvutia zaidi akiwa kocha wa United.

**2. Manchester City (nyumbani) - Ligi Kuu: 16/03/2019**

Wakati linapokuja suala la Manchester 'Dabi', inaonekana wazi kwamba United wamekuwa wanaonewa zaidi kwa siku za hivi karibuni. Manchester United inachukia kufungwa na Manchester City, hasa wakiwa nyumbani na watu wachache wanajua zaidi kuliko Ole Gunnar Solskjaer. Kuibuka kwa Man City katika siku za hivi karibuni kumewafanya Mashetani Wekundu kunyanyaswa, hivyo mchezo huu utakuwa na kila aina ya upinzani, huku Man United wakitaka kumaliza ubabe kwa vijana wa Pep Guardiola.

United ilikwenda kwa City Novemba mwaka jana walichapwa 3-1 na tofauti ya ubora wa timu hizo mbili ilionekana wazi. Na mchezo huu utakuwa mtihani mkubwa kwa Solskjaer kuhakikisha kwamba anaibuka na ushindi. Lakini kucheza dhidi ya kocha mwenye uzoefu wa kutosha kama Guardiola, kunahitaji mbinu za ziada kuweza kufanikiwa kumfunga.

Mchezo wa kwanza wa 'Dabi' ya Manchester kwa Solskjaer unaweza kuwa mtihani utakaompa mafanikio au kumporomosha. Matokeo mazuri hapa yatamfanya kuwa na uhakika wa kupewa mkataba wa kudumu.

**1. Liverpool (nyumbani) - Ligi Kuu: 24/02/2019**

Moja ya mchezo wenye upinzani mkubwa kwenye Ligi Kuu ya soka Ulaya ni huu. Mchezo wa kwanza United ilichapwa na kikosi hicho cha Jurgen Klopp wakati wakiwa chini ya kocha Jose Mourinho. Ulikuwa ni mchezo wa mwisho wa Mreno huyo kukaa kwenye benchi la United na ndio ulikuwa moja ya sababu ya kutimuliwa hapo Old Trafford.

Wakati kwa sasa wakiwa wamepitwa pointi 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, hakuna kitu ambacho Solskjaer atakuwa akikitarajia zaidi ya kuhakikisha anaibuka na ushindi dhidi ya Liverpool.

Solskjaer sio mgeni kwa timu hizi mbili zinapokutana uwanjani, kwa kuwa hata wakati wake wa uchezaji anaujua vizuri upinzani mkubwa uliopo. Kwa vyovyote atakuwa akichukia kuwa kocha kwenye mchezo huu dhidi ya Liverpool. Solskjaer atakuwa na hamasa kubwa ya kuhakikisha anapata matokeo mazuri kwenye mchezo huo.

Liverpool hadi sasa imepoteza mchezo mmoja tu kwenye ligi na imefungwa mabao 13 katika mechi 23 walizocheza. Wamefunga mabao nane zaidi ya United na washambuliaji wao watakuwa na kitu fulani cha kuhitaji kufunga zaidi.

Lakini Solskjaer amethibitisha kwamba anaweza kutoa changamoto kwa kuiwezesha United kupata matokeo mazuri msimu huu, hivyo ni mchezo unaotarajiwa kuwa na upinzani mkubwa zaidi.

## NUKUU

"Falsafa yangu inategemea. Ningependa kwenda kwenye klabu na kuwa na hali sawa na [Kocha wa Liverpool] Jurgen Klopp na kocha wa [Manchester City] Pep Guardiola wanavyofanya. Tayari nimekataa kazi tatu kwa sababu si hisi ni ile ninayoitaka," **Jose Mourinho akieleza alivyokataa ofa tatu tangu atimuliwe Manchester United.**



"Nilistahili kabisa kuonyeshwa kadi nyekundu. Huwezi kuingia uwanjani, ilikuwa mechi ambayo kila mtu alifurahia matokeo. Ilikuwa ni mechi ya soka ya kushangaza na timu mbili ambazo ukweli zilitaka kucheza na kushinda," **Kocha wa Wolves, Nuno Espirito Santo akikiri kadi nyekundu alioonyeshwa ni sahihi kufuatia kuingia uwanjani kushangilia wakati Diogo Jota akikamilisha hat-trick kwa kufunga bao la nne dakika za majeruhi wakishinda 4-3 dhidi ya Leicester City juzi.**



"Nimekasirika sana kwa namna ambavyo tumecheza leo. "Ninatambua kuwa dhidi ya timu imara unaweza kujikuta mwenyewe katika hali ngumu muda hadi muda, lakini unapaswa kujibu zaidi kwa ubora. Ni mchezo ambao hatuwezi kuukubali. Ilikuwa hivyo hivyo dhidi ya Tottenham, tulidhani tumemaliza matatizo lakini inaonekana ni vigumu sana kuhamasika, sijali kuhusu kupoteza ila sipendi kupoteza kwa namna hii," **kocha wa Chelsea, Maurizio Sarri baada ya timu yake kuchezea kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Arsenal juzi.**



## Michezo




Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo, akizungumzia kuhusu udhamini wa Tigo katika mbio maarufu za Tigo Kili Half Marathon, zitakazofanyika mjini Moshi Machi 3, mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**

# UHONDO MBIO ZA TIGO KILI HALF MARATHON

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

NI zaidi ya faida kwa wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro, hususan mji wa Moshi na vitongoji vyake, kwa kuwa Machi 3, mwaka huu itakuwa ni fursa ya kipekee kunufaika kupitia mbio fupi za Tigo Kili Half Marathon wakati zitakapotimua vumbi mkoani hapo.

Mbio hizo za kilometa 21, mwaka huu zinatarajiwa kuleta fursa nyingi kwenye sekta ya utalii na kukuza vipato vya wananchi wa mjini Moshi.

Ikumbukwe kwa mwaka wa nne sasa, Tigo inakutanisha Watanzania zaidi ya 5,000 mjini Moshi kushiriki mbio hizo ambazo zimekuwa zikijizolea umaarufu mkubwa ulimwenguni mwaka hadi mwaka.

Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo, akizungumza kwenye hafla ya kutangaza kuanza kwa usajili mjini Moshi juzi, alisema kupitia udhamini huo pamoja na mambo mengine utasaidia kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii.

"Kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, mbio hizi zitaongeza idadi ya wageni watakaotembelea mji wa Moshi na vivutio vya utalii vilivyopo. Tigo Kili Half Marathon inalenga kukuza vipato vya wananchi.

"Hapa tutaibua fursa mbalimbali za hoteli, wauza vinywaji, chakula, kumbi za starehe, vocha za simu, sekta ya usafirishaji; mabasi, daladala, bodaboda, teksi na biashara nyingine zitafaidika kutokana na uwepo wa mbio hizi," anasema Mwalongo.

Meneja huyo anaongeza kuwa, kampuni ya Tigo inadhamini mbio hizo kama njia mojawapo ya kuchangia juhudi za serikali kuinua viwango vya michezo na kujenga afya bora za Watanzania kupitia ushiriki wao katika michezo.

"Katika eneo hili tunatarajia kuwa na wanamichezo wa kimataifa, kitaifa, wapenzi wa mchezo wa riadha na pia wanafamilia watakaoshiriki katika mbio hizi za Tigo Kili Half Marathon," anasema Mwalongo.

Anazitaja zawadi za fedha taslimu kwa washindi 10 wa kwanza, tuzo za medali, vyeti vya ushiriki na fulana za kumbukumbu kwa washiriki wa kwanza 5,500 watakaomaliza mbio hizo.

Meneja huyo wa Kanda alisema Tigo inawahakikishia washiriki wa mbio hizo kupata mawasiliano ya uhakika kwa kuwa tayari kampuni hiyo kwa kutambua, imepanua huduma ya Tigo 4G kufikia miji zaidi ya 22 nchini ukiwamo mji wa Moshi.

"Kupitia mtandao wetu wa 4G+, washiriki wote wa Tigo Kili Half Marathon watakuwa na fursa ya kutuma picha, video na kumbukumbu zao kupitia mtandao wenye kasi ya juu," anasema Mwalongo.

Akizindua mchakato wa kujisajili, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema Tigo Kili Half Marathon huleta wageni kuanzia 12,000 hadi 15,000 wanaoutembelea mji wa Moshi.

"Hii ni njia muhimu ya kuimarisha utalii na uwekezaji wa kibiashara unaofanywa na wananchi wetu," anasema RC Mghwira.

Naye Mratibu wa mbio hizo, John Bayo, alisema mbio za Tigo Kili Half Marathon zimekuwa na mvuto wa aina yake kutokana na kushirikisha watu zaidi 5,000.

"Niwaombe Watanzania waanze kujisajili huko huko walipo kwa kutumia Tigo Pesa wanamaliza kila kitu kwa kubonyeza *149*20# itawaletea maelezo yote.

"Mwaka huu usajili umekuwa tofauti, miaka iliyopita ulifanyika mpaka siku ya Jumamosi, hatua iliyosababisha kukosekana namba kwa baadhi ya washiriki.

"Kwa mwaka huu tumerahisisha zaidi mfumo wa kujisajili, Mtanzania mwenye kushiriki atalipia kwa mtandao wa Tigo Pesa ili kufanya usajili wake.

"Tigo wataturahisishia kujua mahitaji kamili ya washiriki wa Tigo Kili Half Marathon mapema, usajili utafungwa Februari 7, mwaka huu ili kuandaa namba na fulana za washiriki.

"Tunashukuru washiriki wengi wameanza kujisajili kupitia Tigo Pesa na tunaomba waendelee kujitokeza. Utaratibu wa kufunga mapema usajili unafanywa duniani kote kwenye mbio za kimataifa ili kurahisisha kukamilisha maandalizi yote," alisema Bayo na kufafanua zaidi:

"Usajili kwa njia ya Tigo Pesa ulianza Oktoba Mosi kwa bei ya punguzo yaani Sh. 12,000 mpaka Desemba 7, mwaka jana. Kuanzia Desemba 7 mpaka Januari 7 ilikuwa ni Sh. 15,000 na baada ya hapo hadi kufikia Februari 7, mwaka huu Kilometa 21 itakuwa ni Sh. 20,000.

"Licha ya burudani, mbio hizi zitakupa wakati mzuri kuepuka magonjwa kama sukari, shinikizo la damu, wengi wanashauriwa kufanya mazoezi niombe waje kushiriki Tigo Kili Half Marathon wapunguze mafuta na sukari mwilini."

Aidha, Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, amewapongeza Tigo kwa kudhamini Tigo Kili Half Marathon kwa sababu zimeufanya mji wa Moshi na Kilimanjaro kupaa kimataifa.

"Kilometa 21 zimekuwa na mwitiko mkubwa wa wageni pamoja wazawa, ni dhahiri si wote wanaokuja kukimbia bali wengine huja kwa ajili ya kujiburudisha.

"Ujio wa watu zaidi ya 5,000 ni neema kwa mji wetu na mkoa kwa sababu wafanyabiashara watauza bidhaa, hoteli zitapokea na kulaza wageni maeneo yote yatafanya biashara," alisema Meya Mboya na kuongeza:

"Tigo wamefanya jambo jema, niwapongeze, lakini niwaombe waongeze kitu kingine kipya cha tofauti mfano kuwapo mbio za wazee kuanzia miaka 60 kwenda juu.

"Hao wawe na fungu lao la kukimbia, hii italeta kitu kingine kipya kitakachohamasisha zaidi watu kujitokeza. Kwa upande wangu nitajitahidi kukimbia Tigo Kili Half Marathon."


Katika hatua nyingine kwenye uzinduzi huo, Mwenyekiti wa Chama cha Riadha Mkoa wa Kilimanjaro (KAA), Listone Metacha, anasema kwa mbio za Tigo Kili Half Marathon tegemeo la Watanzania kushinda ni kubwa.

"Vijana wanaendelea na mazoezi mbalimbali, lakini pia wameshiriki mashindano tofauti ndani na nje ya nchi, nina hakika wanariadha wetu kina [Emanuel] Giniki, Gabriel [Geay], Fabian Nelson na wachezaji wengine watafanya vizuri Kilometa 21.

"Changamoto kubwa iliyopo ni ufadhili, niwaombe Tigo wakiweze kutoa msaada wa kuwaweka vijana wakimbiaji wetu kambini, hakika tunaweza kuleta matunda wanayoyatarajia Watanzania katika riadha," anasema Metacha.

**NAJUA WAJUA**

TANGU Jurgen Klopp alipotua kuinoa Liverpool Oktoba 2015, Roberto Firmino, amehusika moja kwa moja katika mabao 69 kwenye mechi za Ligi Kuu England, zaidi ya mchezaji yeyote hapo Anfield (amefunga mabao 45, pasi za mwisho 24).



# MAKIPA WA3 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI

**LONDON,** England

UGOLIKIPA ni moja ya nafasi ngumu zaidi na yenye msongo wa mawazo mengi kwenye mchezo wa mpira wa miguu na bado huwa haitambuliki zaidi. Makosa ya golikipa ndio huwa yanachukua vichwa vingi vya habari kwenye vyombo vya habari kuliko hatari alizoziokoa.

Hata hivyo, magolikipa hivi sasa wameanza kutambuliwa na klabu zinakuwa tayari kutoa kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuwasajili. Kipindi kilichopita cha majira ya joto, iliwekwa rekodi ya golikipa aliyesajiliwa kwa fedha nyingi zaidi.

Kwanza Liverpool walivunja rekodi kwa kumsajili, Alisson Becker, kutoka AS Roma kwa euro milioni 73. Baadaye, Chelsea wakaenda hatua mbele zaidi kwa kutumia euro milioni 80 kumsajili golikipa raia wa Hispania, Kepa Arrizabalaga.

Kutokana na hilo, hapa tunakuchambulia magolikipa watano wenye thamani kubwa zaidi duniani kwa sasa.

**Thibaut Courtois & Alisson Becker - Euro milioni 65**

Baada ya kuwa na mafanikio makubwa na Chelsea kwenye Ligi Kuu ya England, Thibaut Courtois, aliondoka Uingereza na kwenda kujiunga na Real Madrid kwa euro milioni 38.8, wakati wa dirisha la majira ya joto mwaka jana.

Courtois alicheza mechi 154 kwenye michuano yote wakati wa kipindi chake pale Chelsea na aliisaidia kushinda mara mbili taji la Ligi Kuu na moja la FA na lile la ligi.

Hata hivyo, uhamisho wake kwenda Real Madrid haukuenda kama ulivyokuwa umepangwa na sasa yupo kwenye wakati mgumu kutokana na kushuka kiwango. Ameruhusu mabao 22 kwenye mechi 16 za Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, hadi sasa msimu huu na aliweza kucheza bila kufungwa katika mechi sita tu.

Pamoja na yote yeye bado ni golikipa wa daraja la juu na kwa sasa atakuwa anapambana kurudi kwenye kiwango chake. Courtois alitwaa tuzo ya golikipa bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka jana na pia alijumuishwa kwenye kikosi cha wachezaji 11 bora wa michuano hiyo, FIFA FIFPro World XI ikiwa ni kwa mara ya pili.

Liverpool walitumia kiasi cha euro milioni 73, ili kukamilisha usajili wa golikipa wa Brazil kutoka AS Roma wakati wa kipindi cha majira ya joto, Alisson . Hata hivyo, alizoea haraka maisha mapya kwenye klabu yake mpya kwa kuonyesha kiwango cha juu zaidi dimbani.

Uwezo wa kipa huyo mwenye umri wa miaka 26, umewasaidia 'Wekundu' hao kuwa na safu imara zaidi ya ulinzi hadi sasa. Liverpool imeruhusu kufungwa mabao 10 katika mechi 22 za Ligi Kuu msimu huu na ndio wanaoongoza msimamo wa Ligi Kuu.

Kipa huyo raia wa Brazil kwa sasa anaongoza katika mbio za kuwania kuwa kipa bora wa mwaka, kwa kuwa amecheza mechi 13 bila kufungwa katika mechi 22 na amekuwa nguzo kubwa kwa klabu hiyo inayowania kutwaa taji la Ligi Kuu msimu huu.

**David de Gea- Euro milioni 70**

Kwa soko la sasa, De Gea anawekwa kwenye thamani ya euro milioni 70, na golikipa huyo wa Manchester United anashika nafasi ya tatu kuwa mmoja wa makipa wenye thamani kubwa duniani.

Mhispania huyo alijiunga na Manchester United kutoka Atletico Madrid mwaka 2011 kwa ada ya uhamisho iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni 25. Amejiimarisha mwenyewe kwa miaka michache baada ya klabu yake kuanza vibaya. Amecheza mechi 259 za Ligi Kuu kwa 'Mashetani Wekundu' hao hadi sasa na alishinda tuzo ya Sir Matt Busby ya mchezaji bora wa mwaka mara nne.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 28 ameshinda taji moja la Ligi Kuu, moja la Ligi ya Europa, moja la FA, moja na EFL, pamoja na ngao ya jamii mara tatu akiwa na Manchester United. David de Gea alikuwa sehemu ya kikosi bora cha FIFA FIFPro World XI mwaka 2018 na pia alijumuishwa kwenye kikosi bora cha Ligi Kuu ya England kwa misimu sita iliyopita.

De Gea mkataba wake wa sasa hapo Old Trafford utamalizika mwishoni mwa msimu huu na kwa sasa Man United inafanya kila jitihada za kumbakisha kwenye kikosi chao hicho.

**1. Jan Oblak & Marc-Andre Ter Stegen - Euro milioni 80**

Soko la sasa linawapa thamani ya euro milioni 80, makipa Jan Oblak na Marc-Andre Ter Stegen, ambao ndio wanatajwa kuwa bora zaidi duniani kwa sasa.

Jan Oblak alijiimarisha yeye mwenyewe kuwa golikipa bora duniani wakati alipokuwa nguzo muhimu ya mafanikio kwa klabu yake ya Atletico Madrid kwa kipindi cha miaka michache iliyopita.

Baada ya kujiunga na Los Colchoneros hao mwaka 2014, Oblak alishinda taji moja la Europa, moja na Supercopa na Uefa Super, na pia aliwasaidia kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2015-16.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 26, alitwaa tuzo ya golikipa bora wa La Liga mara mbili na alijumuishwa kwenye kikosi bora cha Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili.

Marc-Andre Ter Stegen alijiunga na Barcelona kutoka Borussia Monchengladbach mwaka 2014 na amekuwa chaguo la kwanza kwa kikosi hicho tangu msimu wa 2016-17.

Mjerumani huyo amecheza jumla ya mechi 166 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo hadi sasa na kushinda mataji mengi, ikiwamo mara tatu La Liga, mara nne Kombe la Mfalme ('Copa Del Rey') na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Kipa huyo mwenye umri wa miaka 26, alikuwa sehemu ya kikosi bora cha Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2015-16 na pia alijumuishwa kwenye kikosi bora cha mwaka cha Uefa mwaka 2018.




Marc-Andre Ter Stegen

**NDANI YA 18**

LAURENT Koscielny amekuwa beki wa kwanza Arsenal kuweza kufunga mabao 20 Ligi Kuu England. Mfaransa huyo amefunga katika kila msimu kati ya tisa aliyoichezea, ni Dennis Bergkamp (misimu 11), Aaron Ramsey na Theo Walcott ( misimu 10 kila mmoja) waliofunga zaidi yake hapo 'The Gunners'.





KATIKA mchezo dhidi ya Tottenham, Ole Gunnar Solskjaer alionekana kama amepagawa. Aliweza kuwabana wapinzani wake kwenye kipindi cha kwanza kwa mbinu zake, ambazo baadaye zilimwezesha kupata bao lililowapa ushindi.

Uk. 16-17



# MAJINA MAKUBWA YATAKAYOSHTUA DIRISHA DOGO

**LONDON,** England

KAMA tukizungumzia moja ya jambo muhimu zaidi kwenye mpira wa miguu kwa hivi sasa, usajili ni moja wapo, kwa kuwa inaipa nafasi klabu kufanya tathmini na kuimarisha vikosi vyao, na pia timu zikiweza kusajili wachezaji wanaowataka ili kuleta upinzani kwenye mashindano wanayoshiriki.

Soko la dirisha dogo la usajili limefunguliwa na sasa linakaribia kufungwa, uvumi umekuwa mwingi kuhusu wachezaji gani wanaotakiwa na kusajiliwa.

Kila usajili mara zote huwa unahusishwa na majina makubwa, na pia inaweza kutokea wakati huu wa dirisha dogo.

Hapa tunayaangalia majina makubwa manne ambayo yanaweza kuwa gumzo kwenye usajili...

**4. Adrien Rabiot**

Kiungo huyo wa Paris Saint-Germain, Adrien Rabiot, ni mmoja wa nyota wakubwa wanaoweza kuhama kwenye klabu zao kipindi hiki, huku Mfaransa huyo akiwa amekataa kusaini mkataba mpya na kwa sasa yupo huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote.

Kama ripoti zinavyosema kwamba, Rabiot mahaba yake yapo kwa miamba wa Catalunya, Barcelona, na taarifa zaidi zinasema kwamba tayari ameshasaini mkataba wa awali na mabingwa hao wa La Liga wenye thamani ya euro milioni 10 ukiwa ni mshahara wake kwa mwaka.

Barcelona imekuwa ikimwinda kiungo huyo kwa muda mrefu, na hata kushuhudia ofa zake mbili zikataliwa na Paris Saint-Germain. Hata hivyo, ni wazi kwamba Barcelona wanakaribia kumsajili Rabiot hapo Camp Nou.

**3. Alvaro Morata**

Chelsea walifanya usajili wa fedha nyingi kwa Alvaro Morata wakati wakimsajili kutoka kwa Real Madrid na kutua hapo kwenye dimba la Stamford Bridge wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2017, na nyota huyo wa Los Blancos alianza vizuri kwenye Ligi Kuu ya England, akifunga mabao 10 katika mechi zake za mwanzo.

Hata hivyo, mambo yamebadilika haraka, na sasa Morata ana wakati mgumu katika maisha yake ya soka hapo Chelsea. Kwa sasa raia huyo wa Hispania anaonekana kutokuwa kwenye mapenzi ya mashabiki wa Chelsea.

Gonzalo Higuain

Kama mambo yakiwa hivyo kama yalivyo, ambapo kocha Maurizio Sarri amekuwa akimtumia zaidi Eden Hazard kama namba tisa wake, kuna uwezekano mkubwa mchezaji huyu akaondoka.

Na matokeo yake Morata mara kadhaa ameripotiwa kwamba anataka kuondoka hapo Stamford Bridge, na klabu kadhaa kubwa barani Ulaya zimekuwa zikiwania saini yake zikiwamo AC Milan na Juventus.

**2. Christian Eriksen**

Hali ya Christian Eriksen pale Tottenham Hotspur haieleweki. Mchezaji huyo wa zamani wa Ajax, amekataa kuongeza mkataba na miamba hao wa Ligi Kuu ya England na inaonekana kwamba anataka kumaliza muda wake wa kukaa na Spurs.

Raia huyo wa Denmark amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu kadhaa barani Ulaya zikiwamo Barcelona na Real Madrid na kocha wake, Mauricio Pochettino, alikoleza moto kwenye hali hiyo wakati alipotoa kauli kuhusiana na mchezaji huyo.

Alinukuliwa akisema: "Bila shaka Christian Eriksen ni mchezaji muhimu kwa Tottenham na kwa kocha yeyote atataka kuwa na aina ya mchezaji kama yeye. Lakini mwisho wa siku kila mmoja anakuwa na mawazo tofauti juu ya hatima yake kwenye timu.

"Litakuwa jambo zuri zaidi kama Christian Eriksen ataongeza mkataba wake na sisi, na kama hataki ana haki ya kuamua lolote analolitaka."

**1. Gonzalo Higuain**

Nyota mwingine anayeweza kuondoka wakati huu wa dirisha la Januari ni mshambuliaji wa AC Milan, Gonzalo Higuain, huku kukiwa na uvumi mwingine kuhusu hatima yake hapo kwenye dimba la San Siro.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Argentina aliondoka pale Juventus kwenda kwa 'Rossoneri' hao wakati wa kipindi cha majira ya joto baada ya kucheza kwa miamba hao wa Serie A kwa miezi sita.

Na sasa amekuwa akihusishwa kumaliza kufanya mazungumzo na Chelsea na kuna uwezekano mkubwa akatua pale Stamford Bridge.

Higuain amekuwa akiwaniwa na Maurizio Sarri kwa muda mrefu na ameripotiwa kuishawishi bodi ya Chelsea ili mchezaji huyo asajiliwe hapo Stamford Bridge, wakati kocha akiwa kwenye harakati zake za kuimarisha kikosi chake hasa kwenye safu ya ushambuliaji.

**USILOLIJUA**

ARSENAL haijapoteza katika mechi 13 za 'London dabi' kwenye Ligi Kuu England ikiwa uwanja wake wa nyumbani; imeshinda 10 na sare tatu (W10 D3), huku ikishinda sita mfululizo zilizopita.



**HABARI MBEYA**

## Waweka kando itikadi za vyama, wachangia ujenzi kituo cha afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Igoma, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameungana bila kujali itikadi za vyama vyao kuchangia fedha kwa ajili ya upanuzi wa kituo cha afya, ili waondokane na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

Katika harembee hiyo walijitokeza wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 70 ambao walisema wanaunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha huduma za afya kwenye maeneo wanayoishi hasa ya pembezoni.

Wakizungumza wakati wa harambee hiyo juzi, wananchi hao waliiomba serikali kuwaunga mkono katika kukamilisha upanuzi wa kituo hicho ambacho wanachokitegemea kwenye kata hiyo. Mmoja wa wananchi hao, Maria Timoth (71), alisema wamejitokeza kuchangia kwa sababu shida za matibabu wanazozipata hazichagui itikadi wala umri wa mtu.

Alisema wazee ndio wanaopata shida zaidi za matibabu kutokana na mazingira ya eneo hilo kutokana na kutokuwa na uwezo wa kusafiri kwenda mpaka katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Ifisi au katika hospitali ya mkoa.

"Hapa ni jirani kwetu, hata ikitokea nikaugua usiku au mtoto wangu inakuwa rahisi hata kukimbia kuja kupata matibabu ndio maana tumeona tuboreshe kituo chetu kwa kushirikiana wote," alisema Maria.

Naye Ndegelina Mwakalila, alisema wajawazito wanapata shida wakati wanapotaka kujifungua kwa kusafiri umbali mrefu kwenda kupata huduma hali inayohatarisha maisha yao.

Aliiomba serikali kuwaunga mkono wananchi hao ili wafikie malengo ya kukamilisha kituo hicho na hatimaye waondokane na changamoto zinazowakabili. Diwani wa Kata ya Igoma, Fredy Mwankenja, alisema awali kituo hicho kilikuwa ni zahanati ya kijiji, lakini kutokana na mahitaji ya sasa wameamua kuipanua ili iwe kituo cha afya. Alisema uamuzi huo ulifikiwa na Baraza la Kata hiyo na kisha kuwashirikisha wananchi ambao waliafiki na kuanza michango ili kufanikisha ujenzi huo ambao unahitaji fedha nyingi.

Mwankenja alisema ili kufanikisha ujenzi huo, wanaiomba Serikali Kuu chini ya Rais Dk. John Magufuli, iwasaidie kama ilivyosaidia kwenye maeneo mengine nchini na kwamba wananchi wake wapo tayari kuchangia nguvu zao. Alisema katika harambee hiyo, wananchi walichanga Sh. milioni 28.8, huku wengine wakiahidi kusaidia mifuko ya saruji na mchanga.

"Tunatarajia kuanza na jengo la huduma ya mama na mtoto ambalo litakuwa ni jengo mama na litaunganisha pia kitengo cha upasuaji, jengo la kusubiri wajawazito, chumba cha kupumzika waliojifungua na jengo la kufulia nguo," alisema Mwankenja.

Alisema wananchi wake wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwenda kupata huduma za afya jijini Mbeya kwa kukodi magari na wengine kulipa nauli hali inayowaumiza.

# Zaidi ya watoto 1,000 wahitimu mafunzo ya malezi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya watoto 1,200 wa mikoa ya Mbeya na Dar es Salaam, wamehitimu mafunzo ya miaka miwili ya makuzi na malezi kwa njia ya michezo yanayotolewa na Shirika la Maendeleo la BRACK Tanzania kupitia mradi wake wa Play Lab.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo hayo mkoani hapa, Kaimu Meneja wa Mradi wa Makuzi na Malezi kwa Watoto kutoka BRACK, Ramadhan Ismail, alisema mradi huo ulikuwa unafanyika katika vituo mbalimbali vya shirika hilo.

Alisema mafunzo hayo yalianza mwaka 2016 na yalikuwa yanafanyika katika vituo vya BRACK na kwamba katika Mkoa wa Mbeya yalikuwa yanafanyika katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na kwa Dar es Salaam Halmashauri ya Temeke.

Ismail alisema mradi huo ambao ulikuwa unafadhiliwa na Shirika la LEGO kutoka nchini Denmark, ulikuwa unawahusisha watoto kwenye michezo ya Sayansi, Hisabati, kusoma, kuandika, sanaa za kazi za mikono na michezo huru.

Alisema mradi huo umewasaidia watoto kwenye makuzi ya kiakili na kimwili, kuijua lugha ya mawasiliano na hata kukua kihisia, huku pia ukiwasaidia wazazi na walezi malezi sahihi ya watoto ikiwamo kujua umuhimu wa michezo.

"Mafunzo haya yanatolewa kwa sababu utafiti mbalimbali wa wataalamu unaonyesha kuwa kupitia michezo, watoto wanajifunza masuala mbalimbali ambayo huchochea na kuimarisha maendeleo yao na miongozo yake inaonyesha michezo 232," alisema Ismail.

Alisema katika Jiji la Mbeya watoto waliomaliza mafunzo hayo ya miaka miwili walikuwa 630 na Temeke walikuwa 570 na kwamba wazazi walifundishwa namna ya kutengeneza vifaa vya asili vya michezo kwa ajili ya watoto pamoja na ulinzi na usalama wa watoto.

Alisisitiza kuwa kupitia mradi huo wa play lab BRACK, ikishirikiana na serikali ipo katika mchakato wa awali wa kupendekeza kuwapo kwa mwongozo wa kufundishia vituo vya makuzi na malezi kwa watoto umri kati ya miaka mitatu hadi mitano ambao ndani yake mbinu kuu itakayotumika kuwafundisha itakuwa michezo.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ambaye alikwa mgeni rasmi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alilipongeza shirika hilo kwa ubunifu wa mradi huo kwa madai kuwa unaisaidia serikali kuwaandaa watoto.

Alisema serikali itaendelea kutafuta wadau mbalimbali yakiwamo mashirika kama BRACK kwa ajili ya kusaidia jamii na kwamba katika ngazi za wilaya wanawatumia maofisa ustawi wa jamii ambao wanatakiwa kufuatilia miradi inayoanzishwa.



Watoto wakionyesha michezo mbalimbali waliyofundishwa na wataalamu kutoka Shirika la Maendeleo la BRACK Tanzania katika Jiji la Mbeya kupitia Mradi wa Palay Lab. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Must chaanzisha kozi ya uhandisi vifaa tiba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must), kimeanzisha kozi maalumu ya uhandisi vifaa tiba, ili kuzalisha wataalamu watakaoisaidia serikali kupunguza gharama za uagizaji wa wataalamu kutoka nje ya nchi kuja kutengeneza hivyo vinapoharibika.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Joseph Msambichaka, wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyetembelea chuo hicho kwa ajili ya kukagua shughuli za maendeleo.

Prof. Msambichaka alisema chuo hicho kilianzisha kozi hiyo kwa ngazi ya stashahada baada ya kubaini kuwa kuna uhaba wa wataalamu hao nchini na hivyo kuifanya serikali ilazimike kuagiza wataalamu kutoka nje ya nchi na kwa gharama kubwa.

Alisema kozi hiyo ni mara ya kwanza kuanza kutolewa nchini.

"Tatizo la wataalamu hawa ni kubwa sana, kwa mkoa wetu wa Mbeya tunaye mtaalamu mmoja ambaye anategemewa na hospitali zote kwa hiyo huwa wakati mwingine vifaa vinachelewa kutengenezwa kwa sababu ya uhaba wa hawa watu," alisema Prof. Msambichaka.

Alisema kwa ngazi ya taifa tatizo hilo ni kubwa kwa kuwa wataalamu hao wanatoka wizarani na bado hawakidhi mahitaji hali inayoilazimu serikali kuagiza kutoka nje ya nchi.

Alisema pamoja na kwamba kozi hiyo ni mpya na ni kwa mara ya kwanza kutolewa na chuo hicho, mwitikio wa wanafunzi wanaojitokeza kwa ajili ya kuisomea ni mkubwa.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila, alipongeza uongozi wa chuo hicho kwa utendaji kazi mzuri ambao alisema utalisaidia taifa kusonga mbele kimaendeleo kutokana na kuzalisha wataalamu.

Alisema uanzishaji wa kozi hiyo ya uhandisi wa vifaa tiba utalisaidia taifa kuondokana na tatizo la upungufu wa wataalamu hao ambao ni muhimu katika uboreshaji wa huduma za afya.

Chalamila alisema kwa takwimu alizozipata ni wataalamu hao ni wachache na hawazidi 100 ambao wana elimu ya ngazi ya stashahada na kuutaka uongozi wa chuo hicho kuongeza juhudi katika utoaji wa mafunzo hayo.


"Mnafanya kazi nzuri sana, lakini kutokana na umuhimu wa kozi hii nawashauri msiishie kwenye stashahada, mwendelee mpaka zipatikane shahada za kwanza na shahada za uzamili za kutosha hapa nchini," alisema Chalamila.

Alisisitiza kuwa kwa sasa serikali inaendelea na uboreshaji wa huduma za afya ya msingi kwa kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati na kila kata inakuwa na kituo cha afya na kutaka uzalishaji wa wataalamu hao uwe wa kasi kutokana na mahitaji kuongezeka.

Baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho waliiomba serikali kuboresha miundombinu hasa ya barabara kutokana na zilizopo kuchakaa na kutoendana na hadhi ya chuo kikuu.

Rais wa Serikali ya wanafunzi wa Must, Deogratius Machupa, alisema tangu chuo hicho kilipojengwa mwaka 1982 mpaka sasa barabara zake hazijawahi kufanyiwa marekebisho.

Katika ziara yake Chalamila alitembelea maeneo mbalimbali ya chuo hicho pamoja na kukagua jengo la maktaba linalojengwa chuoni hapo na kuwataka wasimamizi waendelee kusimamia vizuri ili likamilike haraka na kwa viwango vilivyokusudiwa.





# Marekebisho Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa yaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), imesema ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290, ili kuongeza usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Sheria hiyo inaainisha mamlaka na taratibu mbalimbali zinazohusu usimamizi wa fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na pia vyanzo mbalimbali vya mapato.

Hayo yalibainishwa juzi na Waziri wa Nchi wa Ofisi hiyo, Selemani Jafo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo kuhusu taarifa ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kipindi cha nusu ya mwaka (Julai-Desemba) 2018/19.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondokana na changamoto za ukusanyaji mapato ya ndani kwa mamlaka hizo.

"Sheria hiyo imetumika kwa muda mrefu tangu 1982 hivyo, marekebisho hayo yanalenga kuweka uhalisia wa utendaji wa sasa katika namna bora zaidi ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa," alisema.

Aidha, Waziri Jafo alisema katika kipindi cha nusu mwaka, halmashauri zimekumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo baadhi ya wanunuzi kuchelewa kulipa ushuru kwa halmashauri na kusababisha kuonekana zimekusanya chini ya kiwango.

"Pia baadhi ya halmashauri kutegemea zaidi chanzo kimoja na kushindwa kukusanya kutoka kwenye chanzo hicho kunaweza kusababisha halmashauri hizo kushindwa kujiendesha," alisema.

Kadhalika, alisema kuna matumizi mabovu ya mifumo ya kukusanyia mapato kwa njia za kielektroniki kwa baadhi ya halmashauri, kutumia takwimu za makisio zisizo uhalisia na kushindwa kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vipya vinavyobuniwa na halmashauri.

Aidha, Waziri Jafo alisema wameweka mikakati mbalimbali ya kutatua changamoto hizo na kusisitiza ofisi yake itaendelea kuzisimamia kwa karibu halmashauri zote zinazoonyesha kusuasua katika suala la ukusanyaji wa mapato.

Aliitaka mikoa na halmashauri kusimamia utoaji wa taarifa kupitia mifumo ya kielektroniki ikiwamo kazi za usuluhisho na kusafisha takwimu chafu kwenye mfumo wa Epicor 10.2, ili kuwezesha kuwa na takwimu sahihi kwenye 'Dashboard' ya mapato ya ndani na kwa wakati.

Pia alisema ofisi yake imeandaa mwongozo wa ukusanyaji mapato ya ndani ili kuzisaidia halmashauri kuwa na uelewa wa pamoja kwa watu wote ya masuala ya ukusanyaji wa mapato kuanzia suala la kupanga, kukadiria, kukusanya, kutumia, ukaguzi wa nje na ndani na kutoa taarifa.



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu (kushoto), akiongozana na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, walipotembelea eneo la Medeli, jijini Dodoma, zinapojengwa nyumba 100, kwa ajili ya makazi ya askari polisi. **PICHA: WMN**

# Mavunde awataka wana Saccos kubuni miradi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeutaka uongozi wa Kazi Saccos kubuni miradi yenye tija ili kuboresha mfuko wao na kuleta manufaa kwa wanachama wake.

Rai hiyo ilitolewa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa kwanza wa wanachama wa Saccos hiyo, jijini hapo.

Alisema uongozi wa chama hicho unatakiwa kubuni miradi ya kimkakati inayotekelezeka na kuendana na mazingira, na hali ya kiuchumi ya eneo husika.

"Ni vyema uongozi kuangalia fursa za kiuchumi zilizopo Dodoma, ili kuanzisha miradi itakayoendana na hali halisi ya kiuchumi pamoja na kukikwamua chama chenu kuendelea kuwa na tija," alisisitiza Mavunde.

Aidha, aliwaambia uwepo wa vyama hivyo ni kisheria na kikanuni za utumishi wa umma na kuwataka kuviheshimu ili kuendelea kuwa wanachama hai.

"Ieleweke kuwa ukiwa katika chama hiki, bado upo katika utaratibu na kanuni za utumishi wako, hivyo mwendelee kufanya vyema katika chama ili kujipatia heshima ndani na nje ya ofisi yako," alisema Mavunde.

Aliwapongeza viongozi pamoja na wanachama wote kwa mchango wanaoutoa kwa ofisi yake kuzingatia mchango wa chama kwa watumishi wote.

"Ninashawishika na kuona mchango wenu kwetu kama ofisi, kwa kuwa mmechangia kutatua changamoto zinazowakabili watumishi wetu, ambao vinginevyo wangeshindwa kutoa huduma bora yenye tija kwa wadau wetu kutokana na changamoto za kifedha huenda ingechangia kuwaingiza katika matendo ya utovu wa nidhamu kama vile rushwa," alisisitiza Mavunde.

Pia aliwataka viongozi wa ofisi yake kuendelea kuunga mkono jitihada hizo ambazo chama kimezionyesha hususani uanzishwaji wa miradi ikiwamo kuwekeza katika viwanda.

Naye, Mwenyekiti wa chama hicho, Omari Sama, aliahidi kutekeleza maelekezo ya waziri huyo kwa kuanzisha miradi endelevu itakayoleta maendeleo ya kiuchumi kwenye chama, kuongeza wanachama na kukifanya chama hicho kitambulike zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa ofisi hiyo, Peter Kalonga, aliuasa uongozi mpya kuendelea kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama, ili kutatua changamoto wanazokabiliana nazo.

# PM kufungua mkutano wa maofisa ustawi jamii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajia kufungua mkutano wa kiutendaji wa maofisa ustawi wa jamii mikoa na halmashauri nchini unaolenga kujadili utendaji kazi, utoaji huduma za ustawi wa jamii na mifumo ya utendaji kazi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ustawi wa Jamii Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Rashid Maftaha, mkutano huo unatarajia kuanza Januari 29 hadi 31, mwaka huu jijini hapa.

"Mkutano utakuwa na washiriki takribani 370 na pia umeshirikisha wizara za kisekta ambazo zinahusiana na utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, kama Wizara ya Elimu, Afya, Katiba na Sheria, Viwanda na Biashara, Madini na Kilimo," alisema.

Alisema kaulimbiu ya mkutano huo ni "Weledi, uadilifu, uwajibikaji ni nguzo ya msingi katika kuleta ustawi wa makundi maalumu kuelekea katika uchumi wa kati wa viwanda."

Maftah alisema wanaamini watendaji kwenye halmashauri na mikoa wakifanya kazi zao kwa kuzingatia uadilifu, weledi, wakifuata sheria, kanuni na taratibu, makundi yenye uhitaji maalumu wanaweza kufikiwa inavyotakiwa na mchango wao ukaongezeka katika uchumi wa viwanda.

"Huu ni mkutano wa kwanza ikiwa ni takribani miaka 15 baada ya kutokea mabadiliko ya kuiondoa Idara ya Ustawi wa Jamii kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa," alisema.

Alisema serikali ya awamu ya tano imekuwa ikifanya kwa vitendo katika kuwahudumia wananchi hususani wanyonge ikiwamo wazee, wenye ulemavu, watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu, wanawake wenye mahitaji maalumu kama wajane, wenye magonjwa sugu na walio katika kaya maskini.

"Huu mkutano ni wa kutoa mrejesho wa utekelezaji wa huduma za jamii katika maeneo ya serikali za mitaa, utendaji kazi na namna mfumo inavyofanya kazi, pia tutaangalia mafanikio na changamoto na kwa upamoja na kuja na mapendekezo ya kutatua changamoto stahiki za kiutendaji," alisema.

Aliwaasa wananchi kuendelea kuwalinda watoto kwa kutoa taarifa haraka kwa mamlaka pale panapokuwa na viashiria au dalili au kitendo cha ukatili kwa mtoto.

HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vicent Mashinji, akitoa maoni kuhusu muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2018, katika kikao cha Kamati ya Katiba na Sheria kilichofanyika katika ukumbi wa Msekwa jijini Dodoma. **PICHA: BUNGE**

# Balozi Iddi ahamasisha wasomi elimu ya juu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema ni wajibu kwa wahitimu wote wa ngazi ya stashahada kujipanga upya katika mwelekeo wa kutafuta elimu ya juu zaidi, ili kujijengea mazingira mazuri ya ajira.

Alisema ni ukweli usiopingika kwamba elimu ya stashahada katika ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia bado ni ndogo katika soko la ajira.

Balozi Iddi alitoa nasaha hizo kwenye mahafali ya sita ya Chuo cha Afya Zanzibar (Zanzibar School of Health - ZSH) yaliofanyika mjini hapo.

Alisema watu wanaofanikiwa katika maisha yao ya kila siku ni wale wanaokubali kwenda na wakati, kitu ambacho wahitimu hao wanapaswa kukizingatia vyema kwa kukubali mabadiliko hayo yatakayowawezesha kupata mafanikio katika maisha yao ya baadaye.

Balozi Iddi aliwataka wahitimu watakaojaribu kutafuta ajira baada ya kukamilisha mafunzo yao ya stahahada wajenge ustahamilivu katika changamoto hiyo iliyokabiliwa na ushindani wa kiwango cha elimu.

Aidha, aliwasihi wahitimu wa kada ya uuguzi watakaobahatika kupata ajira serikalini au hata kwenye hospitali binafsi wajitahidi kuwa wauguzi wa kuigwa kwa kuwapa faraja pamoja na matumaini wagonjwa watakaowahudumia.

Alisema lazima wawe wauguzi wa kuwajibika wenye kuepuka kuahidiwa chochote wakati wa kutekeleza wajibu wao.

Balozi Iddi aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa jitihada za kukiwezesha kusajiliwa na NACTE ikiwa ni hatua inayopaswa kupongezwa kipekee.

"Hongera kwa walimu na wafanyakazi wote wa Zanzibar School of Health chini ya Mkurugenzi wake mahiri mwana mama Aziza Hamed, kwa ushirikiano na kazi nzuri ya kutuyarishia vijana wetu ambao ndio nguvu kazi ya taifa letu," alisema Balozi Iddi.

Akisoma risala ya uongozi, Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Haji Hassan Mkoko, alisema inatia moyo kuona taasisi hiyo ya kitaaluma ya afya imeungwa mkono na wananchi wengi licha ya kipindi kifupi toka kuasisiwa kwake mwaka 2010.

Dk. Mkoko alisema uongozi wa chuo hicho umelenga kuanzisha mafunzo ya kukabiliana na maafa katika kipindi kifupi kijacho yatayokwenda sambamba na ujenzi wa hospitali ya kufundishia wanafunzi katika miaka saba ijayo.

Hata hivyo, alisema zipo changamoto zinazokwaza ufanisi wa majukumu ya chuo, ikiwamo uhaba wa majengo, viwanja vya michezo pamoja na ukosefu na bweni kwa wanafunzi hasa wanapokuwa katika matayarisho ya mitihani yao.

Aliiomba serikali kutia baraka zake katika kuhamasisha baadhi ya taasisi za ndani na nje ya nchi kufikiria wazo la kuunga mkono chuo hicho katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo.

# Huduma za afya zaboreka Mnazi Mmoja

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya, Hamad Rashid Mohammed, amesema upatikanaji wa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya umepiga hatua kubwa kutokana na juhudi zinachukuliwa na serikali kupitia wizara hiyo.

Waziri Hamad aliyasema hayo katika mkutano wa majumuisho ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, wizarani kwake Mnazi Mmoja.

Alisema huduma za matibabu, vifaa tiba pamoja na dawa muhimu zimekuwa zikipatikana katika vituo mbalimbali vya Unguja na Pemba kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma hiyo.

Alisema upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umeimarika katika vituo hivyo, jamii imenufaika na upatikanaji wa huduma hiyo jambo lililopunguza tatizo la usumbufu wa huduma ya afya.

Alisema wizara yake itaendelea kutoa huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya kwa wananchi wote kwa kuwapatia huduma muhimu na matibabu yaliyo bora. Hata hivyo, aliitaka kamati hiyo kuielimisha jamii kuendelea kutumia huduma zinazotolewa serikalini kwa utaratibu uliopo na pale panapohitajika kuchangia waweze kusaidia ili kupata huduma hiyo.

Alisema kuna changamoto ya upatikanaji wa baadhi ya dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya kukosekana au kuharibika na kusababisha kufuata huduma hiyo sehemu nyingine hali inayolazimu wananchi kuchangia huduma hiyo kwa lengo la kupata vipimo sahihi vya matibabu.

"Uwezo wa serikali wa kutoa huduma sio kwa asilimia mia moja pale ambapo panahitajika kuchangia basi wananchi wanatakiwa kuchangia ili kupata huduma na kuondoa changamoto zilizopo," alieleza Hamad.

Aidha, aliwapongeza watendaji wa wizara hiyo kwa juhudi kubwa wanazozifanya za kutoa huduma za afya kwa jamii licha ya changamoto nyingi wanazokabiliana nazo na kufanikisha upatikanaji wa huduma ya afya.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mwanaasha Khamis Juma, alisema utaratibu wa kufanya ziara ni njia ya kuondoa changamoto zinazoikabili taasisi husika na kuzipatia ufumbuzi wa haraka na kuleta maendeleo kwa jamii.

## UWT Zanzibar yaja na mikakati ya ushindi 2020

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Tanzania, upande wa Zanzibar, umezindua rasmi kamati ndogo nne zitakazokuwa na majukumu mbalimbali ya kufanikisha kwa ufanisi kazi za umoja huo kwa mwaka 2019/2020.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa, Thuwayba Kisasi, alizitaja kamati zilizozinduliwa kuwa ni pamoja na Uchumi, Mipango na Fedha, Mawasiliano kwa Umma, Elimu, Malezi na Mafunzo pamoja na Uhusiano na Taasisi za Wanawake ndani na nje ya nchi.

Alisema kuanzishwa kwa kamati hizo ni matarajio makubwa zaidi kuwafikia wanawake na vijana pamoja na makundi mbalimbali katika jamii na watoto ili kushinda uchaguzi ujao wa mwaka 2020.

Katika maelezo yake Makamu Mwenyekiti huyo aliwasisitiza wajumbe wote wa kamati hizo kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya UWT pamoja na CCM kwa ujumla.

"Wanawake ni jeshi kubwa tena la ukombozi ndani ya Chama Cha Mapinduzi, nasaha zangu kwenu ni kwamba tutumie nafasi hii kuhakikisha tunawafikia wanawake wote hasa waliopo vijijini na pembezoni kwa nia ya kuwaweka karibu na kufanya nao shughuli zetu za kisiasa," alisema Kisasi.

Aidha, alieleza kuwa wanawake wa UWT lazima wapaze sauti kila mmoja kwa nafasi yake ndani ya umoja huo ili kuyasema mambo mema yanayotekelezwa na CCM chini ya viongozi wa chama hicho akiwamo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, wanaoendelea kusimamia kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020.

Aidha, aliwataka wanawake nchini kushirikiana katika malezi ya watoto ili waweze kukua wakiwa katika malezi na maadili borayatakayowasaidia kupambana na changamoto za mmong'onyoko wa maadili.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa UWT Zanzibar, Tunu Juma Kondo, alieleza kuwa UWT imejipanga kufanya kazi zake kisayansi zaidi kwa lengo la kufanikisha kwa wakati malengo waliyojiwekea ndani ya umoja huo.

Alisema kamati hizo zilizozinduliwa zitakuwa ni chachu ya kubuni miradi mipya ya kiuchumi itakayoongeza kipato ndani ya UWT pamoja na kupatikana fursa ya uhusiano mzuri na taasisi mbalimbali za wanawake duniani.

# Mahakama yamthibitisha Tshisekedi mshindi urais

**KINSHASA,** Congo

MAHAKAMA ya kikatiba ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo jana, ilimtangaza Felix Tshisekedi kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais na kutupilia mbali madai ya Martin Fayulu kwamba uchaguzi huo ulikuwa na udanganyifu.

Katika uchaguzi huo Tshisekedi alipata kura kwa asilimia 38.57 ya kura zote zilizopigwa na Fayulu alipata kura asilimia 34.8.

Hukumu hiyo imethibitisha kuwa Tshisekedi ndiye aliibuka mshindi wa kinyang'anyiro cha uchaguzi huo wa urais baada ya kupinga kesi iliyowasilishwa na kiongozi wa muungano wa upinzani wa LAMUKA, Fayulu.

Kwenye madai yake ya msingi na kufungua kesi, Fayulu alidai kuwa Tshisekedi na Rais Joseph Kabila walifanya mpango wa siri baada ya matokeo ya awali kuonyesha kwamba mgombea ambaye alikuwa akiungwa mkono na Kabila, Emmanuel Shadary, ameshika nafasi ya tatu katika uchaguzi huo.

Uamuzi huo wa mahakama umemaanisha kuwa kwa sasa Tshisekedi anaweza kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo muda wowote.

Kadhalika, Fayulu ambaye amejitangaza kuwa Rais wa Congo ameitaka Jumuiya ya Kimataifa kupinga ushindi huo wa Tshisekedi kwa kutotambua mamlaka yake aliyoyataja yasiyoungwa mkono na Wacongo.

Vyombo kadhaa vya habari vya kimataifa mwanzoni mwa wiki viliripoti kuwa data zilizovujishwa za uchaguzi wa Congo zilionyesha kuwa Fayulu ndiye aliyeshinda na sio Tshisekedi.

Kanisa lenye ushawishi mkubwa nchini Congo la Kikatoliki pia limeunga mkono hoja ya Fayulu kuwa Tshisekedi hakushinda.

Hata hivyo, nchi za magharibi bado hazijamtumia salamu za pongezi Tshisekedi, huku nchi ya Ufaransa ikieleza wasiwasi wake juu ya matokeo hayo.

Gazeti la Financial Times na vyombo vengine vya habari vya kimataifa vimethibitisha kuona nyaraka zinazoonyesha kuwa Fayulu ndiye mshindi wa uchaguzi huo.

Kambi ya Fayulu iliusifu Umoja wa Afrika (AU) kwa kutoa ombi la kutaka matokea ya mwisho yaahirishwe, lakini kambi ya Tshisekedi ilisema ni ombi litakaloleta kashfa.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wameeleza kuwa mvutano huo umezua wasiwasi kwamba mgogoro wa kisiasa ulioanza baada ya Rais Joseph Kabila kukataa kuachia madaraka mwishoni mwa muhula anaoruhusiwa kikatiba kumalizika miaka miwili iliyopita unaweza kusababisha umwagaji damu mkubwa.

Congo mojawapo ya taifa kubwa barani Afrika ambalo limekosa utulivu kwa muda mrefu, lilitumbukia katika vita vya kikanda kuanzia mwaka 1996 hadi 2003, na chaguzi mbili zilizopita, 2006 na 2011 zilighubikwa na mapigano ya umwagaji damu.

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), awali ilitoa wito wa kura kuhesabiwa tena pamoja na kuundwa kwa serikali ya umoja wa muungano. **DW**




Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu (kulia), akisalimiana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Chad, Mahamat Zene Cherif (kushoto). Netanyahu yupo nchini Chad kwa lengo la kufufua uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi hizo mbili uliopooza tangu miaka 50 iliyopita. **PICHA AFP.**

# Wanawake kuandamana wakitaka haki sawa

**WASHINGTON,** Marekani

MAELFU ya wanawake watakusanyika katika miji mikubwa nchini Marekani na duniani kote Jumamosi ya wiki hii kwa maandamano ya kila mwaka yanayofanyika kwa mara ya tatu yakishinikiza haki sawa za kijinsia.

Pia wataandamana kutaka dunia itafakari juu ya wasiwasi ulioko juu ya uharibifu wa mazingira na suala la haki za wahamiaji, kati ya vitu vingine vingi.

Maandamano hayo yalianza kufanyika mwaka 2017 na wanawake siku moja baada ya Donald Trump kuapishwa kuwa Rais wa Marekani.

Siku ya kwanza ya utawala wa Rais Trump, mamia ya maelfu ya wanawake walienda jijini Washington kuonyesha upinzani wao mkubwa dhidi ya utawala mpya na sera zake.

Maandamano kama hayo yaliwahi kufanyika katika maeneo zaidi ya 600 nchini Marekani na duniani kote kuunga mkono maandamano yaliyokuwa yanafanyika mjini Washington.

Kaimu mkuu wa polisi Washington, Peter Newsham, kwa wakati huo alisema kuwa maandamano hayo katika mji mkuu wa Marekani ni makubwa.

Wengi wa wanawake hao walikuwa wamevaa kofia zilizofumwa katika umbile la paka ikiwa na masikio madogo kuonyesha kuunga mkono hisia zilizoko dhidi ya Trump na kukosoa maoni ya Trump yenye lugha chafu aliyokuwa ameyatoa miaka kadhaa huko nyuma kabla ya kuingia katika medani ya siasa. **RFI**

## Bilionea agundua analea watoto wasio wake

**LONDON,** Uingereza

"NILIPOGUNDUA, nilihisi kama nimegongwa na nyundo kichwani." Ni maneno ya mfanyabiashara mashuhuri nchini Uingereza, Richard Mason (54).

Anasema kilichomshtua zaidi ni baada ya daktari kumfahamisha kuwa alikuwa na ugonjwa unaofahamika kama cystic fibrosis uliomfanya kupoteza nguvu ya kuzalisha tangu alipokuwa mdogo.

Hali iliyomaanisha kuwa yeye sio baba wa watoto wake watatu aliyodhani amezaa na mke wake wa zamani, Kate.

"Nilifahamishwa kuwa wanaume wote wanaougua cystic fibrosis hawana uwezo wa kuzalisha," alisema Mason na kuongeza.

"Nilidhani pengine nimepewa majibu ambayo si sahihi, lakini daktari alinihakikishia kuwa ana uhakika kuhusu uchunguzi wake na kwamba nahitaji kuzungumza na mtalaka wangu kuhusu baba wa watoto wetu."

Mason alienda kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu baada ya mke wake wa sasa aitwaye Emma, kushindwa kushika mimba.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa alijadiliana kuhusu suala hilo na Kate aliyekuwa mke wake wa zamani mwaka 2007 baada ya miaka 20 ya ndoa, alimwambia mapacha wake Ed na Joel, 19, na Willem (23) ni wanawe.

Hata hivyo uchunguzi wa DNA umeonyesha kuwa watoto hao siyo wa kwake.

"Kwa muda mrefu ugunduzi huo umenipatia usumbufu wa kimawazo," alisema Mason na nimekuwa nikijiuliza ni nani baba wa watoto wangu, sikuwaza lingine," alisema Mason.

Richard alimshtaki mtalaka wake kwa utapeli mwezi Novemba mwaka jana na amekubali kumlipa dola za Marekani 320,000 kwa kumharibia sifa kutokana na dola zaidi ya milioni tano alizolipwa walipoachana.

Hata hivyo jaji aliyeendesha kesi hiyo alimkubalia Kate kutomtambulisha baba wa watoto wake.

"Kate (mtalaka wa Mason) amekataa kumtaja baba watoto, lakini kwa nini ameamua kufanya hivyo kwa kweli hatuelewi hilo kabisa," alisema wakili Roger Terrell.

"Kuna wakati vijana hawa watataka kumjua baba yao mzazi na wakati huo ukifika nitawafahamisha. Sijui kama baba yao ni mmoja wa marafiki wangu wa karibu," alisema Mason na kuongeza.

"Huenda ni mtu wa karibu sana na mimi, mawazo hayo hunijia kila nikiwaangalia vijana wangu wakicheza mpira wa miguu au magongo. Kwa kweli sijui."

"Ukipita katika hali kama hii ambayo inaathiri maisha yako kwa kiwango kikubwa hivi, bila shaka ungelipenda kumjua mhusika mkuu," alisema Masoni.

Mfanyabiashara huyo sasa ameahidi zawadi ya dola 6,400 kwa mtu yeyote atakayemsaidia kubaini baba mzazi wa watoto wake.

## Waliokaidi wito wa TRA kupewa kibano

INATOKA UK. 2

Mkuu wa TRA, Charles Kichere, lilibainisha kuwa uamuzi huo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais John Magufuli dhidi ya malalamiko ya wafanyabiashara nchini.

Katika Mkutano wake na Baraza la Taifa la Wafanyabiashara (TNBC) Machi 20, mwaka jana, walilalamikia kuwapo kwa malimbikizo makubwa ya madeni ya kodi za nyuma yakijumuisha riba na adhabu.

Vigezo vilivyotajwa ni kuwa ni wafanyabiashara waliowasilisha ritani za kodi, lakini bado wanadaiwa kodi yote au sehemu ya kodi zitokanazo na ritani hizo.

Wafanyabiashara ambao hawajawasilisha ritani za kodi na wana madeni ya kodi ambao walikuwa wanafanyabiashara bila kusajiliwa na kupatiwa namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN), namba ya usajili wa kodi ya ongezeko la thamani (VRN) (VAT Registration Number) au usajili mwingine wa kodi kwa mujibu wa sheria zinazosimamiwa na TRA.

Wengine ni waliowasilisha pingamizi za kodi kwa Kamishna Mkuu na ambao pingamizi zao zinashughulikiwa katika ofisi za TRA na siyo kwenye mahakama za kikodi.

Kwa mujibu wa Kichere, wafanyabiashara ambao wamewasilisha pingamizi katika mahakama za kikodi na mashauri yao bado hayajatolewa maamuzi; na ambao wana madeni ya nyuma ya kodi ambayo hayatokani na kesi za jinai za kodi, utakatishaji fedha, usafirishaji wa binadamu au shughuli nyingine haramu.

"Mlipakodi atastahili kupata msamaha wa riba na adhabu endapo yeye binafsi au mwakilishi wake aliyeidhinishwa kisheria atawasilisha maombi ya msamaha kwa kujaza fomu maalum," alifafanua.

Wafanyabiashara hao walitakiwa kuambatanisha maelezo ya kuonyesha kiasi anachodaiwa pamoja na kukubali kwa hiari kulipa deni lake la msingi; kukubali kwa maandishi kulipa kiasi chote cha kodi bila riba na adhabu ndani ya mwaka wa fedha 2018/19 ikiwa na maana kabla au ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Aidha, wafanyabiashara hao walitakiwa kukubali deni la kodi alilokadiriwa na kuwa tayari kutoendelea na pingamizi au shauri husika la kodi lililowasilishwa kwa Kamishna Mkuu, Bodi ya Rufani za Kodi au Mahakama ya Rufani.

Tangazo hilo lilibainisha kuwa msamaha wa riba na adhabu utahusu kodi zote zinazotozwa kwa mujibu wa sheria zinazosimamiwa na TRA isipokuwa ushuru wa forodha chini ya sheria ya ushuru kwa mujibu wa sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

Kadhalika, mapato mengine yasiyo ya kodi ambayo TRA imepewa jukumu la kisheria la kuyakusanya kama vile kodi za majengo na ada za matangazo.

# Ufaransa yawekeza bil. 26/- kusaidia wanafunzi

**Na Salome Kitomari**

UBALOZI wa Ufaransa nchini, umesema serikali yao imetenga Euro milioni 10 (Sh. bilioni 26.2) kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wa kigeni kusoma nchini humo.

Katika kuhakikisha Tanzania inanufaika na fursa hiyo iliyopewa jina la 'Karibu Ufaransa', kimefunguliwa kituo cha kuwasaidia wanaotaka kwenda kusoma nchini humo kutafuta vyuo na wafadhili mbalimbali.

Kadhalika, ubalozi huo umesema kuwa milango ya wanafunzi wa Tanzania wanaotaka kusoma nchini humo iko wazi na watasaidia huduma mbalimbali za kuwezesha masomo yao.

Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier, aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kituo cha kusaidia wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma Ufaransa (Campus France), jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali ya Ufaransa imetengeneza mazingira rafiki kwa watu wanaotaka kusoma nchini humo hususani kutoka nchi za Afrika na Tanzania kwa kuhakikisha wanapata vyuo, maeneo mazuri ya kuishi na mahitaji mengine ya msingi.

"Hivi karibuni Rais wetu Emmanuel Macron, alieleza matumaini yake kuwa Ufaransa itakaribisha wanafunzi 500,000 wa kigeni ifikapo mwaka 2027. Kwa sasa kuna wanafunzi wa kigeni 320,000 wanaosoma fani mbalimbali," alisema na kuongeza:

"Katika kuhakikisha tunaongeza idadi ya wanafunzi wa kigeni dawati la utawala litawasaidia kutafuta vyuo bora vilivyopo Ufaransa, tunaanzisha mfumo rahisi kwao kuomba hati ya kuishi humo (Visa), wanafunzi watapewa kipaumbele kwenye maombi na kwa Dar es Salaam kuna dawati maalum siku ya Jumatano kila wiki kuhudumiwa wanafunzi."

Clavier alisema Ufaransa imeongeza mara tatu idadi ya ufadhili kwa wanafunzi wa kigeni, lengo ni kuwakaribisha wanafunzi wa kesho ambao leo hawajaweza kwenda kusoma Ufaransa.

"Jumla ya nafasi 15,000 za ufadhili kwenda Ufaransa zitatolewa kwa Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi. Ufadhili huu utakuwa mahususi kwa wanafunzi kutoka Maghreb na Afrika," alifafanua.

Mkuu wa ofisi ya kusaidia wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma Ufaransa (Campus France), jijini Dar es Salaam, Karima Allaoui, alisema alipata ufadhili wa kusoma nchini humo kuanzia shahada ya kwanza.

"Shahada yangu ya kwanza nilisomea masuala ya uchumi na usimamizi huko Paris, nilisoma tena shahada ya uzamili ya usimamizi na ufuatiliaji wa kiuchumi wa sera za kijamii katika chuo kikuu kilichopo Grenoble, pia ninayo shahada ya Kifaransa kama lugha ya kigeni," alisema.

"Kilichonivutia nchini humo ni utamaduni wa Kifaransa, ubora wa masomo yake kwa gharama nafuu kwa kuwa serikali ya Ufaransa huchangia zaidi ya theluthi mbili ya gharama za masomo na pia kuna huduma za matibabu kama wanavyopata wanafunzi wa Kifaransa na unaruhusiwa."

Naye, Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekonolojia na Ufundi, Dk. Kenneth Hosea, aliiomba Ufaransa kuangalia uwezekano wa kuisaidia Tanzania kupata wataalamu kwenye miradi ya ujenzi.

Aidha, alisema Ufaransa ni nchi kubwa na yenye uwekezaji wa kutosha katika eneo la teknolojia, hivyo ni vyema kuisaidia Tanzania kuzalisha wataalamu wa kutosha.




Ofisa Mawasiliano wa TBL Group, Amanda Walter (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma na Usalama Barabarani, Mrakibu wa Jeshi la Polisi (ASP) Abel Swai, jezi zitakazotumika katika mashindano ya usalama barabarani zilizozinduliwa mwishoni wa wiki. Katikati ni Mkaguzi wa Elimu kutoka kikosi cha Usalama Barabarani, Bahati Nzundi. **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aipongeza Taasisi ya Mengi kusaidia walemavu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Stella Ikupa, amezipongeza Taasisi ya Watu Wenye Ulemavu ya Dk. Reginald Mengi, Kamal Group of Companies and People's Empowerment Fund na Rotary Club kwa kuendelea kusaidia watu wenye ulemavu nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kupokea viungo bandia kwa ajili ya walemavu vilivyotolewa na taasisi tano, Ikupa alisema amefurahi kuona taasisi zinasaidia watu wenye ulemavu na kuwapa fursa ya kuonyesha uwezo wao.

Alisema ameshaongea na taasisi, zikiwamo People's Empowerment Fund na Kamal Group ambao wamemwambia wanao uwezo wa kutengeneza viungo bandia kwa Watanzania wengi zaidi wenye uhitaji huo.

"Serikali inayoongozwa na Rais John Magufuli, Makamu wa Samia, Suluhu Hassan na wizara yetu, ambayo iko chini ya Waziri Mkuu, inatambua na kuthamini mchango wenu katika kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu," Ikupa alisema baada ya kupokea viungo kutoka Mwenyekiti wa IPP, Dk. Mengi.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inaendelea kutatua changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu, akiwataka wasiwe na wasiwasi na wajiamini ili wajitegemee kiuchumi.

Kwa upande wake Dk. Mengi aliwataka watu wenye ulemavu kujiamini kwamba watafanikiwa katika maisha yao.

"Unapofikiria kuwa tajiri, usifirie kuwa mtu fulani kama Mengi. Badala yake, fikiria kuwa mtu tajiri zaidi ya Mengi kwa sababu unaweza kufanya hivyo... Rai yangu ni kwamba mnaweza," alisema.

Alisema anawapenda watu wenye ulemavu na ndiyo maana hivi karibuni alifungua kampuni itakayotengeneza simu na bidhaa za kielektroniki itakayoajiri watu wengi wenye ulemavu.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**HUDUMA MBALIMBALI**

**GARI HONDA CRV YA MWAKA 2007 INAUZWA.** INATEMBEA NA IKO KATIKA HALI NZURI SANA. BEI MAELEWANO PIGA 0755834730 AU 0755260247

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**MAOMBI YA SHAURI LA KAZI NA.13/2018**
**ADAMU HUSSEIN KAPERA ..........................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**DAALO MEAT & FOOD STUFFS CO LTD.......... ...MJIBU MAOMBI**
**KWA: DAALO MEAT & FOOD STUFFS CO LTD**

**POPOTE PALE ULIPO**

YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA MAOMBI YA SHAURI LA KAZI NA.13/2018 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA-DODOMA

MNAFAHAMISHWA KWAMBA; shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania,kanda ya Dodoma,mbele ya MHE.JAJI G.M.MASAJU, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 14/3/2019.

HIVYO; Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hamtafika nyinyi wenyewe au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo nyinyi au Wakili wenu kuwepo.

**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 27/11/2018.

**D. R. LYIMO**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
P.O.BOX 943
DODOMA

215015402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**MAOMBI YA SHAURI LA ARDHI NA.3/2018**
**MAULIDI ITOHE...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. SHABANI HASSANI BANTU**
**2.BEYA MATEI ....................WAJIBU MAOMBI**
**3. AKWII ANDREA**
**4. LUCAS BUNG'EE**
**KWA: 1. AKWII ANDREA**
**2. LUCAS BUNG'EE**

**POPOTE PALE WALIPO**

YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA MAOMBI YA SHAURI LA ARDHI NA.3/2018 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA-DODOMA

MNAFAHAMISHWA KWAMBA; shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania,kanda ya Dodoma,mbele ya MHE.JAJI G.M.MASAJU, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 14/3/2019.

HIVYO; Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

NA ENDAPO; Hamtafika nyinyi wenyewe au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo nyinyi au Wakili wenu kuwepo.

IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 27/11/2018.

**D. R. LYIMO**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
P.O.BOX 943
DODOMA

215015302

**CHETI KIMEPOTEA**



**NEEMA P. MATINDIKO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2153/0014** katika shule ya **AQUINAS SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2010 na cheti cha kidato cha sita chenye **namba S.0276/0667** katika shule ya **IFUNDA GIRLS SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2013,

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:MT/RB/730/2019**

215015802

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SOLSKJAER: Rashford ni bora EPL kwa sasa

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford (pichani chini), anaweza kuwa mshambuliaji bora kwenye Ligi Kuu ya England wakati Harry Kane akiwa majeruhi, kwa mujibu wa kocha Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer.

Rashford alifunga wakati United ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Brighton and Hove Albion Jumamosi na kufikisha mabao matano katika mechi saba tangu kuwasili kwa Solskjaer mwezi mmoja uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, huo ulikuwa ni mchezo wake wa 150 kwa klabu hiyo na amefikisha mabao 41 aliyoifungia timu hiyo hadi sasa.

Na bosi huyo wa United anaamini kwamba kutokuwapo kwa nyota wa Tottenham, Kane, ambaye atakuwa nje ya uwanja hadi Machi mwaka huu kutokana na kuumia kifundo cha mguu, kunaweza kumfanya Rashford kuwa mshambuliaji bora zaidi.

"Unaweza kuwazungumzia washambuliaji wengi, lakini jambo la muhimu ni kwamba yupo kwenye timu yangu," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Harry Kane yupo (chumba) cha majeruhi pengine inaweza kumfanya yeye kuwa bora zaidi kwa wakati huu.

"Hakuna anayeweza kumfikia kwa kiwango chake kwa sasa na ninapenda mtazamo wake kwa timu na vile anavyoweza kucheza kwa kujiamini na kufunga mabao.

"Anajua kumalizia vizuri, huwa hafikirii mara mbili anapokaribia goli na hivyo kumfanya kuwa mfungaji wetu mzuri zaidi kwa sasa."

Kiwango cha Rashford kimekuwa kikiimarika zaidi tangu kuwasili kwa Solskjaer hapo Old Trafford, akichukua mikoba ya Jose Mourinho aliyetimuliwa na sasa amefikisha mechi saba bila kufungwa.





# EMERY ataka Arsenal ikaze buti na ugenini

**LONDON,** England

UNAI Emery amebainisha kwamba kuna tofauti kubwa ya kiwango cha Arsenal wakati wanapocheza nyumbani na ugenini, baada ya kuifunga Chelsea kwenye Uwanja wa Emirates.

Mabao ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Alexandre Lacazette na Laurent Koscielny, yaliinyanyua Arsenal kwenye nafasi ya tano katika msimo wa Ligi Kuu ya England juu ya Manchester United kwa tofauti ya bao moja na wakipitwa pointi tatu na Chelsea.

Arsenal haijafungwa nyumbani kwenye mchezo wa Ligi Kuu England tangu ilipochapwa na Manchester City 2-0 katika mechi ya ufunguzi ya ligi hiyo msimu huu.

Lakini katika mchezo wa Jumamosi, walionyesha kiwango cha juu zaidi, wakitoka kufungwa hivi karibuni na Southampton, Liverpool na West Ham.

"Tulitaka kushinda kwa ajili ya mashabiki wetu na kufanya kitu fulani maalumu kwenye mchezo dhidi ya Chelsea," alisema Emery akinukuliwa na BT Sport.

"Tofauti kwenye msimamo ilikuwa ni pointi sita na ushindi unaweza kutusaidia kupunguza pengo hilo. Ni vigumu kuendelea kwa hali hii, lakini tunaweza kuwa na furaha kwa namna tulivyocheza leo (juzi).

"Tunatakiwa kutafuta usawa tunapocheza nyumbani na ugenini, kwa sababu nyumbani tunakuwa imara zaidi. Tuliwaonyesha mashabiki wetu kuwa tuko imara.

"Lakini tukiwa ugenini tunahitaji kucheza kwa kiwango kama hiki. Tofauti kati ya mechi iliyopita na ya sasa ni kwamba tumeimarika."

# Tuchel ashangaa PSG kushinda 9

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, aliachwa akishangaa wakati timu yake ikiibomoa Guingamp mabao 9-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Ufaransa juzi Jumamosi.

Kylian Mbappe na Edinson Cavani kila mmoja alifunga mabao matatu 'hat-trick', huku Neymar akifunga mara mbili wakati PSG ikiitendea vibaya Guingamp mjini Paris.

PSG iliweka rekodi ya ushindi kwenye ligi hiyo ya Ufaransa maarufu kama Ligue 1, wakimwacha kocha huyo raia wa Ujerumani akishangaa.

"Natakiwa kufikiri kuhusu hilo, lakini sikufikiria kwamba timu inaweza kushinda 9-0 kwenye mchezo wa ligi," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Hakika tulitaka kushinda, tulicheza soka la ubora. Tuliimarika wakati wa kipindi cha pili na tulicheza kwa soka la kuvutia. Kulikuwa na mashambulizi mengi, wachezaji walikuwa wengi. Tulikuwa na nafasi ya kufunga na tulitengeneza nafasi za kutosha.

"Baada ya bao la kwanza, la pili na la tatu, tulicheza kwa kujiamini. Tulifanya vitu rahisi, lakini kwa haraka. Tuliridhika na kuwa na furaha kubwa."

Mfungaji wa Hat-trick, Cavani, ambaye alifikisha mabao 100 alisema: "Jambo la msingi lilikuwa ni kuifunga Guingamp baada ya kutolewa kwenye Kombe la Coupe de la Ligue.

"Ilionyesha timu ilitaka kufanya kitu kikubwa na hakika mambo yalienda kama yalivyopangwa.

"Nina furaha kubwa kufunga mabao 100 na lile la 101 kwa PSG. Nipo kwenye historia ya klabu na nataka kuendelea kufunga na kuisaidia timu."



## HABARI MICHEZO

# LAMPARD AMSAJILI ASHLEY COLE

**LONDON,** England

KOCHA Frank Lampard ameushtua ulimwengu wa soka baada ya kutangaza kumsajili rafiki yake, Ashley Cole (pichani), mwenye umri wa miaka 38.

Cole amekubali kupokea kitita cha pauni 15,000 kwa wiki kujiunga na klabu ya Derby County inayonolewa na rafiki yake, Lampard ili kuisaidia kufanya vema kwenye Ligi ya Championship nchini Uingereza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, ameushtua ulimwengu wa soka baada ya kutangazwa kurejea kwenye soka la ushindani la Uingereza kufuatia uamuzi wa swahiba wake ambaye hapo awali waliwahi kucheza pamoja ndani ya klabu ya Chelsea.

Utambulisho rasmi wa Cole utafanyika leo Jumatatu baada ya kufanyiwa vipimo vya afya saa 48 zijazo.

Beki huyo wa kushoto atajiunga rasmi na Derby kwa mkataba wa miezi sita akiwa kama mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake kwenye klabu ya Los Angeles Galaxy inayoshiriki Ligi ya MLS nchini Marekani Oktoba mwaka jana.

Cole ambaye ni mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya England, amewahi kuichezea klabu ya Arsenal (1999-2006) na kwenda kwa mkopo Crystal Palace (2000), kisha kutua Chelsea (2006-14), Roma (2014-16), LA Galaxy (2016-18), huku akifanikiwa kunyakuwa vikombe kadhaa vikiwamo Champions League mara moja, Europa League mara moja, Ligi Kuu mara tatu, FA mara saba, Kombe la Ligi mara moja.






Washiriki wa mbio za Airtel Tunakujali FUN RUN, wakishiriki mbio za kilomita 10 zilizoandiliwa na kitengo cha masoko cha kampuni hiyo kwa lengo la kukusanya fedha na kusaidia vijana kujipatia elimu ya ufundi stadi kutoka VETA kupitia mfumo wa 'aplikesheni' ya kimtandao maarufu kama VSOMO. Mbio hizo zilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Muuaji Yanga afunguka

**Na Faustine Feliciane,** SHINYANGA

NAHODHA wa Stand United, Jacob Massawe, amesema ushindi walioupata juzi dhidi ya Yanga ulitokana na morali ya wachezaji kufuatia kupoteza mchezo wao uliopita dhidi ya Biashara United ya Mara.

Massawe ndiye aliyeifungia timu yake bao pekee kwenye mchezo huo na kuipa Stand United ushindi wa bao 1-0.

Akizungumza na Nipashe juzi, alisema walifahamu Yanga ni timu kubwa na ina rekodi ya kutofungwa, hivyo walijipanga kuhakikisha hawapotezi mchezo huo.

"Yanga si timu ya kubeza, ni timu nzuri na wale wanaoibeza wanakosea...walicheza vizuri leo (juzi), lakini sisi tulikuwa bora zaidi yao, nashukuru kwa ushindi huu ambao ulitokana na maelekezo ya kocha wetu, ila pia morali yetu kama wachezaji," alisema Massawe.

Alisema sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo ujao na wanasahau matokeo hayo.

Stand United imeweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kuifunga Yanga msimu huu ambayo kabla ya mchezo wa jana ilikuwa imecheza michezo 20 bila kufungwa, huku ikitoka sare michezo miwili.

# Mbio za 'Tunakujali FUN RUN' za Airtel kuwainua vijana

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inaunga mkono mpango wa serikali wa kuipeleka Tanzania katika uchumi wa kati, Kampuni ya Simu za Mkononi ya Airtel Tanzania kupitia kitengo cha masoko imeandaa mbio za kilomita tano na 10 zinazojulikana kama "Airtel Tunakujali FUN RUN" zikiwa na lengo la kukusanya fedha na kusaidia vijana kujipatia elimu ya ufundi stadi kutoka VETA kupitia mfumo wa utumiaji wa kimtandao maarufu kama VSOMO.

Mbio hizo za Airtel Tunakujali FUN RUN ambazo zilifanyika jana kwa mafanikio makubwa, zilianzia na kumalizika kwenye viwanja vya The Green vilivyopo mtaa wa Toure Drive Oysterbay jijini Dar es Salaam na kuhusisha wadau wa Airtel pamoja na wafanyakazi wake kwa kununua tiketi zao za ushiriki kwa Sh. 20,000, ili kuwezesha zaidi ya vijana 1,000 wenye umri kati ya miaka 18 na 24 watakaopata nafasi ya kujiunga na masomo ya ufundi stadi kupitia 'aplikesheni' ya VSOMO.

Akizungumza jijiji Dar es Salaam jana wakati wa mbio hizo, Mkurugenzi wa Masoko Airtel Tanzania, Isack Nchunda, alisema wamekuwa wakisaidia sana jamii kwa muda mrefu kwa kuwa wanaamini imekuwa ni moja kati ya nguzo muhimu ya wao kuendelea kuwa karibu nayo.

"Jamii hii inayotuzunguka ina maana kubwa sana kwetu sisi Airtel, pia wote tunaamini kusaidia jamii ambayo inaishi kwenye mazingira magumu ni kitu ambacho kinatuumiza sana, hivyo ndio maana mwaka huu tumeamua kuwawezesha vijana ambao wanazo sifa za kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi VETA kupitia 'aplikesheni' ya VSOMO, lakini wamekwama kwa kukosa fedha za kujilipia karo," Nchunda alisema.

"Tunaelewa kwamba umasikini Tanzania unachangiwa sana na ukosefu wa ajira ambao unatokana na kukosa elimu au stadi za kufanya kazi kwa kuwa utafiti mbalimbali wa serikali unaonyesha zaidi ya asilimia 70 ya vijana Tanzania wenye umri kati ya miaka 16-30 hawana ajira, na zaidi ya asilimia 50 ya hao hawana sifa za kupata ajira au kujiajiri.

"Kwa kusaidia vijana kupata mafunzo ya ufundi stadi ni imani yetu kuwa tunasaidia kuzalisha ajira, lakini zaidi ni kuunga mkono juhudi za serikali yetu ya kuwa na uchumi wa viwanda," alisema Nchunda, huku akiongeza kuwa "ili nchi kuwa na viwanda imara, ni vizuri kuwa na wataalumu waliobobea kwenye mafunzo ya ufundi stadi."

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel, Beatrice Singano, alisema 'aplikesheni ya VSOMO' inatoa mafunzo ya ufundi stadi kupitia mtandao ambao mafunzo hayo hutolewa na VETA kwa kushirikiana na Airtel.

Alisema tangu kuanzisha kwake 2016, vijana zaidi ya 39,000 wameweza kupakua 'aplikesheni' hiyo huku wengine 12,000 wakiwa wamejisajili kwa ajili ya mafunzo na 115 tayari wamemaliza mafunzo na kupatiwa vyeti vyao.

"Nachukua fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wenzangu kwa kujitokeza kwa wingi kwenye mbio hizi za Airtel Tunakujali FUN RUN ambazo kwa kweli zitaweza kubadilisha maisha ya vijana wetu," alisema Singano, huku akiongeza kuwa mbio hizo zimekuwa na mafakio makubwa kutokana na ushirikiano kati ya Airtel Tanzania, maji ya kunywa ya Dasani pamoja na Benki ya Letshego Tanzania.

Naye Mkurugenzi Mtendaji VETA, wanaoisimamia 'aplikesheni ya VSOMO', Dk. Panacras M. S. Bujulu alisema: "Mafunzo haya yanayotolewa kwa njia ya mtandao, imekuwa ni moja kati ya mbinu ya kiubunifu ambayo VETA tunaitumia ili kufikisha mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana wengi zaidi hapa nchini."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MODRIC: NATAKA KUBAKI MADRID

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa Real Madrid, Luka Modric, amesema anataka kubaki La Liga na kuendelea kuitumikia miamba hiyo ya Hispania kwa zaidi ya mkataba wake wa sasa.

Modric, ambaye alihusishwa na miamba ya Serie A, Inter mwanzoni mwa msimu huu, ana mkataba na Madrid hadi 2020.

Lakini mshindi huyo wa tuzo ya mchezaji bora ya duniani ('Ballon d'Or') mwenye umri wa miaka 33, ni mwenye furaha hapo Santiago Bernabeu na anatupia macho kuongeza mkataba wake.

"Nina mwaka mmoja na nusu uliobaki katika mkataba wangu na ni mpole, kama ilivyo kwa muda mrefu," Modric aliwaambia wanahabari.

"Matamanio yangu ni kubaki hapa kwa muda mrefu. Ni mwenye furaha kama nilivyokuwa siku ya kwanza."

Modric alikuwa akizungumza baada ya Madrid kushinda 2-0 nyumbani dhidi ya Sevilla kwenye mechi ya La Liga juzi.

Casemiro aliifungia Madrid bao la kuongoza kwa mkwaju wa mbali katika dakika ya 78 kabla ya Modric kufunga dakika ya mwisho na kuipa timu yake ushindi.

Ushindi huo uliifanya Madrid kuishuka Sevilla hadi nafasi ya nne na yenyewe ikikaa ya tatu huku ikibaki pointi saba nyuma ya vinara Barcelona.

"Ni mwenye furaha na nadhani tumecheza mchezo mzuri," alisema. "Tuwenye furaha kwa uchezaji wetu na furaha kwa pointi tatu.

"Tunahitaji kufuata njia hii. Kila mchezaji alikuwa na mchezo mzuri na mashabiki wetu wanataka kutuona kama hivi.

"Tunahitaji mechi kama hii kutoa baadhi ya furaha yetu kwetu wenyewe na kwa mashabiki. Binafsi, ninajisikia vizuri na nilijisikia vizuri kwa mwezi mmoja na nusu uliopita."

Kuhusu mbio za ubingwa, Modric aliongeza: "Hatuhitaji kuifikiria Barcelona ama kuhusu kiasi cha pointi tulizonazo. Tunahitaji kwenda mechi baada ya mechi.

"Tunahitaji kupigana na kuona ni wapi tutakuwapo mwishoni mwa msimu. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya, si kuhofu kuhusu wengine."

## KWA UFUPI

### HIGUAIN KUFUNIKA MSHAHARA

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Gonzalo Higuain, 31, atajiunga na Chelsea kwa mkopo wiki hii hadi mwishoni mwa msimu, kwa mkataba utakaomwezesha kulipwa pauni 270,000 kwa wiki, ambao utamfanya kuwa miongoni mwa wachezaji watano wanaolipwa dau kubwa zaidi Ligi Kuu England. **(Star on Sunday)**

### COUTINHO AULIZIWA CHELSEA

CHELSEA imeulizia Barcelona kuhusu dau la pauni milioni 100 inalomthaminisha kiungo wa zamani wa Liverpool, Philippe Coutinho, 26. **(Express)**

### HAZARD AVIZIWA MADRID

REAL Madrid inatumai inaweza kumsajili Eden Hazard kwa chini ya euro milioni 100 zinazotakiwa na Chelsea kwa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 28 ambaye mkataba wake unamalizika Juni 2020. **(Marca)**

### BATSHUAYI AWANIWA EVERTON

EVERTON inapanga kutoa ofa ya pauni milioni 40, ili kumpata mshambuliaji wa Chelsea, Michy Batshuayi, 25, anayeonekana kutohitajika. **(Sun)**

### MBAPPE AFUNGUKA MADRID

STRAIKA wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 20, amesema anaweza kujaribiwa kutua Real Madrid hapo baadaye. **(AS, via Mirror)**

### POCHETTINO HATAENDA SOKONI

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino, amesema inauwezekano zaidi wa kumtafuta mbadala wa majeruhi Harry Kane, 25, katika shule yao ya vipaji kuliko kwenda sokoni. **(London Evening Standard)**

### SUAREZ ANUKIA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, bado ana matumaini ya kupokea sura mpya wiki hii kufuatia taarifa ya klabu hiyo kuhusishwa na kiungo wa Barcelona, Denis Suarez, 25. **(Star)**

### SILVA AKATA TAMAA USAJILI

KOCHA Marco Silva amerudia matumaini yake kwamba Everton hatasajili mchezaji yeyote mwezi huu. **(Liverpool Echo)**

### NAPOLI YAMGOMEA DIAWARA

Napoli imekataa ofa ya mwanzo kutoka AC Milan kwa kiungo wao, Amadou Diawara, 21, ambaye amekuwa akihusishwa na Tottenham na Wolves. **(Inside Futbol)**

### GODIN ATAKA KUTUA INTER

MTENDAJI Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amedai kuwa nahodha wa Atletico Madrid, Diego Godin, 32, ambaye hivi karibuni amekuwa akihusishwa na Manchester United, anataka kujiunga na klabu hiyo ya Italia. **(Calciomercato)**

### MOURINHO AANZA MANENO UTD

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, amesema alijua tangu mwanzoni mwa msimu kuwa hawatakuwapo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu. **(Manchester Evening News)**

### SPURS YAMTEGA MALCON

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, amekubali kwamba Malcom anahitaji nafasi ya kucheza zaidi wakati huu winga huyo wa kimataifa wa Brazil akiwindwa na Tottenham, Everton na klabu za **China. (AS)**

### GUARDIOLA AICHOKONOA SCHALKE

KIUNGO wa Schalke, Sebastian Rudy, ameingia katika rada za Manchester City baada ya kocha wa klabu hiyo, Pep Guardiola kumtaka kwa mkopo ili kumsaidia Fernandinho. **(The Sun)**

HABARI MICHEZO

# AJIBU: SABABU KIPIGO YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI na nahodha wa Yanga, Ibrahim Ajibu (pichani), amesema hakuna mtu wa kulaumiwa kufuatia kipigo cha bao 1-0 walichokipata kutoka kwa Stand United juzi.

Wakiwa kwenye Uwanja wa Kambarage juzi, Yanga walipokea kipigo hicho cha kwanza msimu huu kwenye Ligi Kuu na kuhitimisha rekodi yao ya kucheza michezo 19 bila kufungwa.

Ajibu alisema katika mchezo huo walitengeneza nafasi nyingi, lakini hawakuwa makini kuzitumia wakati wapinzani wao walipata nafasi na kuitumia vizuri.

"Tumefungwa kimchezo hakuna wa kumlaumu... kocha atakuwa kaona makosa yetu, tunaenda kuyafanyia kazi," alisema Ajibu.

Aidha, alisema kila wanapomaliza mchezo mmoja wanajipanga kwa michezo inayofuata, hivyo wanasahau matokeo hayo na wanaelekeza nguvu kwenye michezo mingine.

Baada ya mchezo huo wa juzi, Yanga sasa wanarejea Dar es Salaam kujiandaa na michuano ya Sportpesa Cup inayotarajiwa kuanza kesho.

Hata hivyo, matokeo ya juzi bado yanaendelea kuiweka Yanga kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikibakiwa na pointi zake 53 ikifuatiwa na Azam yenye pointi 47.



## Kikwajuni yapigwa tafu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kiwajuni inayoshiriki Ligi Daraja la Pili, imepigwa tafu ya vifaa vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni mbili na mfanyabiashara na Mwakilishi wa Jimbo la Uzini visiwani Zanzibar, Mohammed Raza.

Vifaa walivyokabidhiwa ni jezi pea 18, viatu pea 20, soksi, mipira, koni, vibendera vya waamuzi, filimbi, kadi na nyavu.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi vifaa hivyo, Raza alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuisaidia timu hiyo kukabiliana na changamoto walizonazo na kuweza kufanya vizuri katika ligi yao.

**Alisema timu ya Kikwajuni ina historia kubwa katika soka la Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, hivyo hatua iliyofikia timu hiyo ipo haja ya viongozi na wapenzi wa michezo kusaidia timu pale zinapohitaji msaada wao.**

Alisema vifaa hivyo vitaweza kuwasaidia wachezaji pamoja na viongozi kupunguza gharama na bajeti waliyojiwekea katika kununua vifaa vya michezo hususan vile vya mazoezi.

"Timu ya Kikwajuni ni timu kubwa hakuna asiyeijua timu ambayo katika miaka ya nyuma kwenye soka la Zanzibar iliweza kufanya vizuri,"alisema.

Kwa upande wake Katibu wa Klabu ya Kikwajuni, Ali Sheha, alisema kwa sasa uongozi wa timu ya Kikwajuni umedhamiria kufufua timu hiyo ili iweze kurejea makali yake ya awali.

Naye mwenyekit wa klabu hiyo, Burhani Himid Msoma, alimtaka Raza kuendelea kuisaidia timu hiyo ili lifikie lengo lililokusudiwa la kuhakikisha timu hiyo inarejea Ligi Kuu ya Zanzibar.



Nahodha wa timu ya kikapu ya NMB, Danford Kisinda, akimtoka mlinzi wa DTB, Abdulkadir Seif, wakati wa mechi ya fainali ya michuano ya benki (BBL 2018/19), iliyopigwa jana kwenye Uwanja wa Gymkhana, jijini Dar es Salaam. DTB ilishinda kwa pointi 90-73. **MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatoa Mfungaji Bora BBL 2018/19

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa kikapu wa kikosi cha Benki ya NMB, Kaikai Leka, ameibuka Mfungaji Bora (Best Scorer) wa Ligi ya Kikapu kwa Taasisi za Fedha (Bankers Basketball League - BBL 2018/19), baada ya kufunga pointi 160 katika mechi za michuano hiyo iliyofikia tamati jana, jijini Dar es Salaam.

Katika fainali ya kukata na shoka iliyopigwa kwenye Uwanja wa Gymkhana, Dar es Salaam jana, Benki ya DTB iliibuka mshindi baada ya kuifunga NMB kwa pointi 90-73, huku Leka akifunga zaidi ya nusu ya pointi zao, hivyo kutangazwa Mfungaji Bora akifuatiwa na Acram Majid wa DTB, aliyefunga pointi 129.

Leka alizawadiwa Tuzo ya Mfungaji Bora, kama ilivyokuwa kwa Mchezaji Bora (MVP) Leonard Benedict wa DTB, Beki Bora Frank Mwemezi wa DTB na kinara wa kufunga pointi tatu kwa mtupo mmoja (Leading Three Pointer), Acram Majid aliyefanya hivyo mara 13 katika michuano yote.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi na kufunga mashindano, Mratibu wa BBL 2018/19, Gozbert Boniface, alizipongeza timu sita zilizoshiriki michuano hiyo kwa upande wa mpira wa kikapu na kuzitaka kujiandaa kwa ajili ya msimu ujao, utakaoanza baadaye mwaka huu.

"Tunaipongeza DTB kwa kutwaa taji, lakini pia kwa NMB kwa kutwaa medali za fedha za ushindi wa pili na pia kwa kutoa Mfungaji Bora wa michuano hii, iliyoshirikisha benki sita za NMB, DTB, Azania, CRDB, TADB na NBC," alisema Boniface wakati akitoa neno la shukrani.

Kwa upende wake, mgeni rasmi wa fainali hiyo, Juma Kimori, ambaye ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa NMB, aliwapongeza waratibu kwa wazo zuri la kuanzisha michuano hiyo, iliyoimarisha uhusiano baina ya taasisi za kifedha nchini, huku akiwapongeza mabingwa na washindi wa pili.

# Michezo

Jumatatu Januari 21, 2019

Nipashe


## Modric: Nataka kubaki Madrid




HABARI UK. 30

HUNIWEZI...



Beki wa kulia wa Arsenal, Hector Belleren, akipata upinzani mkali wa kumiliki mpira dhidi ya beki wa kushoto wa Chelsea, Marcos Alonso (kulia), wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa kwenye Uwanja wa Emirates juzi na 'Gunners' kushinda 2-0. **HABARI UK. 28**



## Kilichoimaliza Simba Congo

**Na Adam Fungamwango**

KILIKUWA ni kipigo kizito cha mabao 5-0 ilichokipata Simba dhidi ya AS Vita mjini Kinshasa nchini Congo DR. Simba iliondoka nchini ikiwa na matumaini kibao ya...

INAENDELEA UK 15



## Mechi zitakazoamua hatima ya Solskjaer

**MANCHESTER,** England

KATIKA mchezo dhidi ya Tottenham, Ole Gunnar Solskjaer, alionekana kama amepagawa. Aliweza kuwabana wapinzani wake kwenye kipindi cha kwanza kwa mbinu...

INAENDELEA UK 16



# ZAHERA ATOA NENO LA UBINGWA YANGA

●●● Awataka mashabiki kusubiri kwanza michuano ya SportPesa kisha wataona...

**Na Faustine Feliciane,** SHINYANGA

LICHA ya kushindwa kujizuia na kuishia kuangua kilio wakati akihojiwa na Azam TV baada ya kupoteza mechi yake ya kwanza msimu huu, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera (pichani), amesema kipigo hicho dhidi ya Stand United hakijawachanganya na kwamba wataendelea kupambana na mechi zijazo ili kufikia malengo yao.

Zahera aliliambia Nipashe jana, kuwa kuna ugumu mkubwa kucheza kwenye viwanja vya mikoani na wachezaji walipambana lakini bahati haikuwa yao.

Alisema anafahamu kwa sasa ligi itasimama kwa baadhi ya timu kwa ajili ya kupisha michuano ya SportPesa na kwamba wataitumia kujipanga kwa ajili ya michezo ijayo ya Ligi Kuu.

"Haukuwa mchezo mwepesi, wachezaji wangu walipambana, lakini hatukuwa makini kuzitumia nafasi tulizozitengeneza, nawapongeza Stand kwa ushindi," alisema Zahera na kuongeza,

"Kwetu bado mapambano yanaendelea, hatujakatishwa tamaa kupoteza mchezo huu... tutapambana kutimiza lengo letu la kutwaa ubingwa msimu huu," alisema.

**Awatuliza Mashabiki**

Aidha, Zahera aliwataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuendelea kuisapoti na kutokatishwa tamaa na matokeo waliyoyapata juzi.

Alisema kufanya vizuri kwa Yanga kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na sapoti ya mashabiki wa timu hiyo.

Yanga inarejea leo Dar es Salaam tayari kushiriki michuano ya SportPesa inayoanza kesho hapa nchini.

Michuano hiyo itashirikisha timu nane, nne kutoka kila nchi, Tanzania na Kenya, ambapo bingwa mbali na kombe na fedha taslimu, hupata fursa ya kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Everton inayoshiriki Ligi Kuu England.

Gor Mahia ndiyo bingwa mtetezi wa michuano hiyo, ambayo imeutwaa ubingwa huo mara mbili mfululizo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >